

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 5 Aprili, 2011**

*(Mkutano ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina mashaka watu wengi leo wameshindwa kuingia humu ndani, vile vibandiko, sijui waandishi wa habari walipewa, kama kuna mtu atakayekuwa hajapewa ile kadi, (*Smart Card*) utaratibu upo pale nje jinsi ya kupata na ukiwa na hiyo *Smart Card* uwe nayo wakati wote, kwa sababu ni ya kufunga na kufungua milango.

Kwa hiyo, unaweza kuwa pekee yako ukajifungia hakuna wa kukufungulia. Utaratibu kwa wale waandishi wa habari kuititia Idara yetu ya Habari wajiandikishe majina yao kusudi watengenezewehi *Smart Card* kwa sababu mnawenza kushindwa kuingia katika maeneo fulani. Siku ya kwanza leo itakuwa na usumbifu, lakin baada ya muda mtakuwa mmezoea. Tunaendelea.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakaewila swali la kwanza katika Bunge hili la Tatu ni Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa niaba yake ni Mheshimiwa Iddi Azzan.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

### **Tatizo Kubwa la Ajira Nchini**

**MHE. IDDI M. AZZAN (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU)** aliliza:-

Mwaka 2008/2009 dunia ilikumbwa na tatizo kubwa la mtikisiko wa uchumi ambao uliathiri Mataifa mbalimbali Tanzania ikiwemo ambayo ilitenga shilingi trilioni moja na milioni mia saba kukabili ana na hali hiyo. Lakini leo nchi inakabiliwa na tatizo kubwa la kukosekana kwa ajira hasa kwa vijana kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga kiasi kama hicho cha fedha kuwaezesha vijana kujajiri katika shughuli za kilimo na ujasiriamali?

### **WAZIRI WA NCHI,OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka 2008/2009 Serikali ilitenga fedha ili kunusuru uchumi wa Tanzania kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani. Fedha hizi zililenga hasa katika kufidia wakulima tofauti ya bei kwa mazao ambayo bei zilishuka sana kama pamba, ili kuwapa uwezo wa kuendelea kuzalisha na kulinda ajira za Watanzania wakiwemo vijana. Vile vile Serikali ilifidia hasara waliyopata wanunuzi na ilidhamini makampuni na vyama vikuu vya ushirika vya pamba na kahawa ili viendelee kukopeshwa na mabenki kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulikuwa ni maalum na pekee kwa tukio maalum ambalo halipo katika mazingira ya sasa. Kutokana na hatua hii, biashara nyingi ziliweza kuimariswa na uchumi kuendelea kukua angalau kwa kiasi kidogo zaidi.

Baada ya hatua hii, Serikali inaendelea kuweka mkazo katika kusukuma maendeleo ya sekta ya kilimo ambacho ndiyo mkombozi wa Watanzania wengi.

Ili kuimariswa sekta ya kilimo, Serikali imeamua kutumia rasilimali nyingi kutekeleza mikakati endelevu ya kujenga mazingira yatakayowezesha sekta ya kilimo na maendeleo vijiji kuvutia vijana kuendelea kubaki kwenye maeneo ya kilimo na kujajiri. Aidha, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili sekta iweze kuzalisha ajira nyingi zaidi, katika uzalishaji, masoko na usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikakati itakayowezesha kilimo kuwa cha kisasa na hivyo kuvutia vijana kujajiri kwa wingi katika sekta hiyo ni pamoja na :-

- Kuendelea kuongeza ruzuku ya pembejeo,
- Kupima ardhi ya vijiji na kupanga matumizi ya ardhi,
- Kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa,
- Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji,
- Kuongeza matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo,
- Kuongeza wingi na ubora wa huduma za kilimo kama vile huduma za ugani, utafiti na mafunzo,
- Kutoa mikopo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uwezo mkubwa wa sekta ya kilimo katika kuzalisha ajira ambazo ni unganishi (*backward and forward linkages*), juhudi za Serikali za kuleta mapinduzi ya kilimo zitakuwa na mchango mkubwa katika kuongeza ajira za vijana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, wakati Serikali imeleta hoja ya kuwa na *stimulus package* yenye thamani ya trilioni moja na milioni mia saba aliekuwa Waziri Kivuli wa Fedha ndani ya Bunge hili aliiata Serikali imtakie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akague jinsi gani ambavyo matumizi ya fedha hizo yalifanywa. Je, Serikali tayari ina taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na fedha za *stimulus package*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Kabwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kawaida kwa fedha zozote za Serikali zinapotumika kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuzifutilia na kuzikagua na kwa vile Waziri Kivuli ndiye alietaka hivyo basi Serikali itakuwa imefanya na zaidi ya hivyo sisi wenyewe Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla inafutilia matumizi ya fedha hizo ili zilete manufaa yaliyokuwa yamekusudiwa na kwa vyovyote vile bila shaka wengi mtakuwa mmeona jinsi *stimulus package* ilivyosaidia wakulima waliokusudiwa wa pamba na wale amba walikuwa kwenye eneo la kahawa. Kwa hiyo, Serikali inajua hivyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa katika huo utaratibu kulikuwa pia na shilingi themanini kwa kila kilio moja kwa wakulima, lakini sasa ni msimu huu wa pili unakaribia inavyoonekana wengi wa wanunuzi ambao waliowalipa wakulima fedha yao ya themanini kama fidia hajjalipwa kwa wengi.

Sasa nashangaa kama Mheshimiwa Waziri akijua kwamba kuna suala kama hili, ameangalia ni watu wangapi ambao hajjalipwa na lini watalipwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cheyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba nia ya Serikali ilikuwa ni kunusuru uchumi ambao umetikisika kutokana na mtikisiko wa ujumla wa uchumi duniani na tulijielekeza zaidi kwenye kilimo na hasa kilimo cha pamba na Mheshimiwa Cheyo anauliza kwamba wanunuzi ambao hajjalipwa shilingi themanini kwa kilo wakulima wengine wa pamba, basi Serikali itafuutilia na kuona kwamba wale ambao hajjalipwa wanalipwa na kama kuna matatizo mengine ambayo yameambatana na juhud hizi za Serikali za kuwanusuru wakulima ambao wangeumia sana tutaona yote yale ambayo yalitakiwa kufanya yamefanya na kuendelea kusisitiza kilimo kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba ndiyo mkombozi wa Watanzania walio wengi ambao shughuli zao kwa asilimia themanini ni ya kilimo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kufutilia swali alilouliza Mheshimiwa Zitto, suala ambalo tulileta hapa Bungeni wakati huo tulitaka tupate *special audit report* ya matumizi ya fedha hizi. Serikali ikaahidi kwamba italeta *special audit report* sio ile taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Je, Serikali italeta lini hii *special audit report* juu ya matumizi ya fedha hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa jinsi maswali yalivyoulizwa inaelekea Wabunge na Bunge lako limekubali kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii. Sasa napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameomba *special audit* iletwe Bungeni na kama wameomba hivyo tutafanya hivyo kwa wakati muafaka.

Na. 2

**Hitaji la Hospitali ya Wilaya – Mkoa wa Rukwa**

**MHE. ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA** aliuliza:-

Mkoa wa Rukwa una Wilaya tatu, Nkasi, Sumbawanga na Wilaya Mpya ya Kalambo na Mkoa hauna Hospitali ya Wilaya badala yake unategemea Hospitali ya *Namanyere Designated District Hospital (NDDH)* iliyoko Nkasi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya hasa Wilayani Kalambo?
- (b) Kwa Mkoa kuwa na Hospitali moja tu kama za rufaa. Je, Serikali haioni kwamba haiwezi kupunguza au kumaliza tatizo la vifo vinavyotokana na uzazi na vya watoto wachanga ambalo limekithiri Mkoani humo?
- (c) Je, Serikali kwa kutojenga hospitali ya Wilaya haioni inapingana na hoja ya Mheshimiwa Rais ya kufikisha huduma za afya karibu na wananchi kwenye hotuba yake ya kufungua Bunge jipya tarehe 18 Novemba, 2010?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya kujenga hospitali za Wilaya katika kila Wilaya, Serikali inao mpango wa kupandisha hadhi vituo vya afya vya Kalambo na Laela vilivypo katika Wilaya za Kalambo na Sumbawanga kuwa hospitali kamili za Wilaya. Hatua za awali ambazo zimekwishachukuliwa katika kupandisha hadhi ya Kituo cha Afya cha Kalambo kuwa Hospitali ya Wilaya ni ujenzi wa jengo la upasuaji, jengo la wazazi na maabara. Kwa upande wa Kituo cha Afya Laela hatua zilizochukuliwa ni ujenzi wa wodi ya wazazi, chumba cha upasuaji, nyumba 2 za watumishi na jengo la maabara. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wilaya imeweka katika mpango wake wa maendeleo kiasi cha shilingi 250,000,000/= kwa ajili ya kujenga jengo la utawala na nyumba 2 za watumishi katika hospitali tarajiwa za Laela.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkoa wa Rukwa una hospitali moja tu ya rufaa, yaani hospitali ya Mkoa. Hospitali hii inasaidiwa na hospitali mbili za Wilaya ambazo ni hospitali teule ya Wilaya Nkasi (*Namanyere DDH*) na Hospitali Teule ya Dr. Atman iliyopo katika Manispaa ya Sumbawanga. Ili kupunguza tatizo la vifo vinavyotokana na uzazi na vya watoto wachanga, Serikali kuitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kuanzia 2007-2017 imeendelea na mkakati wa kujenga Vituo vya Afya 42 na Zahanati 121 ili kutekeleza Sera ya Afya inayotaka kuwa na zahati kila kijiji na Kituo cha Afya kila Kata. Lengo ni kupunguza vifo vya wagonjwa kutokana na magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifo vya uzazi na watoto wachanga.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu sehemu A na B hapo juu ni dhahiri kuwa Serikali inatekeleza kwa dhati hoja ya Mheshimiwa Rais ya

kufikisha huduma za Afya karibu na wananchi kwa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila Kata na Hospitali za Wilaya katika kila Wilaya nchini kote.

**MHE. ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa.

Kawaida mgonjwa anapokuwa ametibiwa zahanati ikashindikana anapewa rufaa kwenda kituo cha afya na inaposhindikana kwa sababu hakuna wataalamu na vifaa vyakutosha basi mgonjwa huyo hupelekwa hospitali ya Wilaya, inaposhindikana mgojwa huyo hupelekwa hospitali ya Mko na ndiyo hii *referral system* tunayozungumzia.

Sasa Mheshimiwa Waziri anaposema wanaboresha vituo vya afya kuwa hospitali ya Wilaya na amesema katika mpango wa MAM azma ni kwamba kila Kata iwe na kituo cha afya.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba tayari atakuwa amevunja vile vituo vya afya na kwamba wananchi wataendelea kuomba kituo cha afya?

Lakini sasa hivi wananchi wanatoka maeneo ya mbali ambayo pengine ni kilomita mia moja ili kufuata huduma hospitali ya Mko kwa sababu hakuna hospitali ya Wilaya, zile za pale Mjini ni tofauti, ni wananchi na wagonjwa wa pale Mjini, wananchi wanaotoka Vijijini wana shida.

Waziri haoni kwamba ni muhimu wakajenga hospitali ya Wilaya kwa sababu hospitali ya Wilaya ni hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya ni Kituo cha Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosweeter kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni-*declare interest* hapa hiki ninachojibu hapa ndiko anakotoka Mheshimiwa Waziri Mkoo na nataka nieleze hali halisi iliyoko pale. Hizi Wilaya zilizoanzishwa ziko nyingi kuna Kalambo kuna Mlele halafu kuna *District Counsel* mpya ambazo zimeanzishwa hapa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anachouliiza hapa anauliza swali la msingi kwa sababu ni sasa hivi hii hali imejitokeza. Kalambo ndiyo tunasema sasa kwamba imekuwa Wilaya unafanyaje, unagoja ujenge hospitali *fully fledge* kama anavyosema au unasema ebu *improve*, tumia kituo cha afya hapa peleka nguvu yako yote ya Serikali pale ili katika kipindi cha mpito sasa wapate huduma, halafu wewe uwasaidie sasa kupata hospitali ya Wilaya, ndiyo maana tukasema hivi tulivyosema.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aone kwamba hizi ni jitihada za hali ya juu sana za Serikali kuona kwamba sasa unaanzisha kituo cha afya pale, unakipandisha cheo unasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini hili la pili mnalozungumzia kwamba wananchi wa Mjini pale, pale Mjini Sumbawanga pale kuna *designated hospital* ya Dokta Atman na pale katika *District Counsel* kuna *designated hospital*, kuna eneo linaitwa Laela ambalo tunalizungumzia hapa.

Hapo Mjini huu utaratibu huu ni utaraibu amabo tumeukubali sisi wote na hapa wote tumeupitisha, hospitali teule ni hospitali ambayo inapata huduma zote zinazotakiwa pale, unapeleka kila kitu pale unawasaidia na wananchi wanakwenda na huduma zile zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Mbunge aone kwamba hizi pia nazo ni jitihada za Serikali. Lakini mawazo kwamba tujenge hospitali ya Wilaya bado sisi tunayakubali tunaona ni ya msingi, wakati utakapofika tutafanya hivyo kama anavyoelekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri swali lake alilijibu vizuri na suala hilo hata Zanzibar tunalo tatizo hili ingawa suala hili ni la Serikali ya Muungano siyo la Serikali ya Zanzibar. Lakini pia ningelipenda na kwa Zanzibar masuala kama haya yakawa yanaangaliwa?

**SPIKA:** Kwa hiyo, swali halipo, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa basi ngoja aulize swali moja Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa tatizo hili la hospitali ya Wilaya lililotajwa katika swali la msingi linafanana na la Wilaya ya Namtumbo, ambayo haina hospitali ya Wilaya. Lakini Serikali katika Bajeti yake ya mwaka jana ilitenga shilingi milioni 400 kuanzisha ujenzi huo. Je, Serikali inaweza kuwashakikishia wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwamba itaendelea kutenga fedha zingine ili ziweze kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ya Wilaya? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Namtumbo anayoizungumzia Mheshimiwa Kawawa mimi nimefika na hali iliyoko pale naifahamu. Kwa hiyo, Mbunge hakosei kabisa kusema hilo. Lakini Serikali kwa kawaida ikishaanzisha mradi haifiki mahali halafu ikuuacha ule mradi ukabaki hivi hivi. Kwa hiyo, kuna milioni 400 kama anavyosema zimetengwa na nina hakika kwamba bado zitaendelea kuwa ni kipaumbele na kwamba Halmashauri nayo itaendelea kufanya hivyo hivyo kwa sababu Halmashauri ndiyo *the bottom line*. Ndiyo inayoanza kwanza habari hii na kusema kwamba sisi bado tunafikiri hiki ni kipaumbele. Kwa hiyo, hili hatuna tatizo nalo

Mheshimiwa na hela hizi zitakuwa zinaendelea kutengwa kufuatana na jinsi ambavyo Halmashauri itakuwa imependekeza.

Na. 3

### **Upungufu uliiopo Kwenye Shule za Sekondari za Kata**

#### **MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA aliuliza:-**

Serikali ya awamu ya nne iliamua kujenga shule za sekondari za Kata kufanikiwa nchi nzima lakini kuna upungufu unaozikabili shule hizo kama ukosefu wa madawati, maabara, upungufu wa walimu hali iliyochangia kutofanya vizuri katika mitihani iliyopita:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani mahsus wa kuondoa kasoro hizo?
- (b) Je, ujenzi wa nyumba za walimu katika shule hizo unaendeleaje?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali ya kujenga shule za Sekondari kila kata imekuwa na mafanikio makubwa katika Sekta ya Elimu pamoja na kasoro zinazojitokeza. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa shule za sekondari nchini kutoka shule za sekondari za wananchi 1,597 mwaka 2006 hadi kufikia shule 3,397 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya shilingi bilioni 109.5 fedha za maendeleo zilipelekwa katika Halmashauri zote nchini kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo upatikanaji wa madawati, maabara na miundombinu mingine kulingana na vipaumbele vya kila Halmashauri. Aidha, Serikali imeandaa Andiko la Utenevezaji wa Madiwati katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2010 hadi 2012 na kuliwasilisha kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya upatikanaji wa fedha. Ni matumaini ya Serikali kuwa fedha zitakazopatikana zitatumika kuondoa tatizo hili sugu.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali imefanikisha ujenzi wa nyumba za walimu 5,424 kati ya mwaka 2006 hadi 2010. Aidha, Serikali itahakikisha kwamba miundombinu ya shule ambayo haijakamilishwa inakamilishwa katika kipindi cha utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari ujulikanao kwa jina la (MMES II).

Katika utekelezaji wa MMES II, Serikali itakarabati na kukamilisha shule za Sekondari 1,800 kwa kuziwekea miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara na ujenzi wa nyumba za walimu mbili mbili katika kila shule.

Kati ya shule hizo, shule 500 zitagharamiwa na Benki ya Dunia ambayo imeridhia mkopo nafuu wa dola za Kimarekani milioni 150 na awamu ya kwanza zimetolewa jumla ya dola za Kimarekani milioni 43. Shule 1,300 zilizobaki katika mpango huu zitagharamiwa na Serikali.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri nimwulize swalii la nyongeza. Katika taarifa ya Waziri Mkuu iliyotolewa kwenye Bunge hili mwaka jana Serikali ilisema kwamba ilitenga shilingi bilioni 55 kwa ajili ya matumizi ya shule kwa mwaka 2009/2010 na taarifa hiyo hiyo inaonyesha kwamba shilingi bilioni 21 hazikutumika hadi mwaka wa fedha unakwisha mwaka jana mwezi Juni.

Sasa swalii la nyongeza kwa Waziri. Ni kwa nini shule hazina madawati wakati fedha zinazotolewa na Serikali hazitumiki zote? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa taarifa hiyo na fedha zote zilishapelekwa katika Halmashauri zetu kwa ajili ya utengenezaji wa madawati. Ziko Halmashauri zimefanya vizuri sana kwa utengenezaji wa madawati na madawati yapo kwenye shule zile.

Ziko Halmashauri ambazo hazikufanya vizuri katika utengenezaji wa madawati hayo na Halmashauri zote ambazo hazikufanya vizuri tumeweza kuzibaini kupitia ukaguzi uliofanywa na Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri zetu na kujua ni kwa kiwango gani fedha zile hazikuweza kutumika na hatua dhidi ya Wakurugenzi hao zinaendelea kuchukuliwa.

**MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa mara nyingi Serikali inaweka mikakati mizuri ya kufanikisha utekelezaji mzuri katika sekta hii ya elimu. Lakini utekelezaji wake wa maagizo hayo unakuwa ni mgumu kutekelezwa na matokeo yake huambulia wananchi ambao wanaishi katika mazingira magumu kuchangia maeneo hayo.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuweko ufuatiliaji madhubuti wa kuhakikisha kwamba fedha ambazo zinatengwa ndiyo ambazo zinatekelezwa katika viwango ambavyo vimepangwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, swali ambalo linataka kujua mzigo mkubwa ambao wananchi wanaupata kwa kuchangia maeneo ambayo tayari Serikali ilishapeleka fedha.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Serikali inapeleka fedha nyingi kwenye maeneo yale kwenye Halmashauri zetu ili zifanye kazi iliyokusudiwa. Suala la wananchi kuchangia nguvu zao ni hamasa ambayo inasaidia sana kuchangia maendeleo na kuweka mtiririko wa kila mwananchi kutambua maendeleo yake.

Lakini hatua madhubuti juu ya Halmashauri ambazo zinapokea fedha kwa kazi iliyokusudiwa na hazifanyiki zinaendelea kufanywa kwa kuimarisha ukaguzi wa ndani.

Lakini pia ukaguzi kutoka nje ili kubaini mapungufu yaliyoko kwenye Halmashauri hizo na hatua kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la pili kwamba zinaendelea kuchukulia dhidi ya Wakurugenzi ambao hawatekelezi vizuri kama ilivyokusudiwa. Ahsante sana. (*Makofî*)

Na. 4

### **Mikakati ya Kupambana na Rushwa**

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali kuititia mikakati yake ya kupunguza umasikini kama vile MKUKUTA, lakini umasikini ujinga na maradhi vinaonekana kuwa bado ni kikwazo kikubwa katika suala zima la kupambana na rushwa hapa nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba lengo la Taifa katika kupambana na rushwa linafikiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa lengo la Taifa katika kupambana na rushwa linafikiwa, Serikali imefanya mambo yafuatayo ambayo ni endelevu.

Kwanza kabisa kwa kuititia Bunge lako Tukufu, Serikali ilipitisha sheria mbalimbali ambazo sasa ndiyo msingi wa mapambano dhidi ya rushwa. Sheria Na. 11 ya mwaka 2007 iliongeza makosa ya rushwa kutoka 4 hadi 24 ambayo yanashughulikiwa na TAKUKURU. Sheria nyingine muhimu ni Sheria ya Manunuzi ya 2004 ambayo inalenga kudhibiti rushwa na ubadhirifu katika manunuzi ya umma na Sheria ya Gharama

za Uchaguzi ya mwaka 2010 ambayo inalenga kudhibiti matumizi mabaya ya fedha na rushwa katika chaguzi zote nchini.

Pili, kupitia Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (*NACSAP*) na utaratibu wa *PETS* – *Public Expenditure Tracking System*, Serikali imeanzisha mafunzo dhidi ya rushwa na Miundombinu ya Maadili kwa watumishi wa Serikali na Taasisi zisizo za kiserikali, ili kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanazingatia maadili katika kutoa huduma kwa wananchi. Kamati za Uadilifu zimeanzishwa katika Idara, Taasisi, Mashirika na Halmashauri zetu na zina jukumu la kufuatilia mienendo ya watumishi katika utoaji huduma na kuwaadabisha wale ambao wanaokiuka maadili. Aidha, chini ya *PETS*, wananchi wanashirikishwa kwa kufuatilia fedha za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba zinatumika kama zilivyopangwa.

Mwisho, Serikali imeimarisha TAKUKURU kwa kufungua Ofisi katika kila mkoa na Wilaya ili kuwafikia wananchi na kuwashirikisha kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa vile watoaji na wapokeaji wa rushwa ni sisi wananchi wenyewe, vita hii ni yetu sote na ninawaomba Viongozi wote wa Serikali wa Siasa wa Dini na wa Jamii kwa ujumla, kukemea rushwa kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo, kwani rushwa ni adui wa haki.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa nina swali moja la nyongeza kama lifuatavyo:-

Kwa kuwa kusimamia utawala wa sheria na TAKUKURU kufanya kazi yake ipasavyo, ni sehemu ya msingi muhimu wa kupambana na rushwa na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa kauli hapa Bungeni kuhusiana na uchunguzi unaohusu kampuni ya Kagoda katika kashfa ya malipo ya madeni ya nje na kwa kuwa Serikali ilisema kwamba uchunguzi wa jambo hili unaendelea ukihusisha vyombo vyta kimataifa, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhusiana na tuhuma hizi za rushwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inasema bado tunaendelea na uchunguzi na pindi utakapokamilika hatua sahihi zitachukuliwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Wakati tulipokuwa kwenye semina ya Ubungo Plaza, Mkurugenzi wa TAKUKURU alisema kwamba amefanya uchunguzi wa kesi nyingi lakini kikwazo kikubwa kiko kwa *DPP*. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutuletea taarifa hapa Bungeni kuonyesha ni kesi ngapi zimechunguzwa na TAKUKURU zimefikishwa kwa *DDP* na ngapi zimekwama kwa *DDP* ambazo angalau zina viwango visivyopungua milioni 20 na kuendelea. Serikali itakuwa tayari kuleta taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Serikali italeta taarifa hiyo kabla ya kumalizika kwa Bunge hili.

**SPIKA:** Hivyo ndivyo wanavyojibu maswali Westminister

**MHE. JOHN LUGOLA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ya msingi amesema kwamba Sheria ya Manunuzi ni Sheria mojawapo ambayo ilitungwa na imesaidia sana katika mapambano dhidi ya rushwa. Na kwa kuwa Sheria hii ya Manunuzi imeletwa Bungeni hapa si kufanyiwa marekebisho ila kufutwa kabisa. Waziri haoni kwamba kitendo hiki kinaonyesha kwamba Sheria hii ya Manunuzi hakuna ilichofanya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatunga Sheria kulingana na mazingira yaliyopo kwa wakati husika. Tulipotunga Sheria ile tulikuwa na mazingira yale na sasa tunaleta kubadilisha na tunatunga nyingine kulingana na mazingira ya sasa. Sheria ile imefanya kazi vizuri na tunachobadilisha kwa kweli hakutakuwa na mabadiliko makubwa sana.

Na. 5

**Mapinduzi ya kilimo na kuwaandaa wakulima  
kuweza kukopa**

**MHE. LUHANGA J. MPINA (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM)** aliuliza:-

Serikali ya awamu ya nne inayo dhamira ya dhati ya kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kutoa ruzuku za kilimo na mikopo kwa wakulima na tayari zaidi ya shilingi 162 zimewekwa kwenye Benki ya Rasilimali *T.I.B.* jimbo la Solwa na sehemu nyingine nchini na wakulima wanasubiri kwa shauku kubwa kunufaika na mikopo hiyo:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaandaa wakulima ili wawe na sifa za kukopesheka?
- (b) Je, Serikali kupitia Benki ya Rasilimali *T.I.B.* itatumia mbinu gani kutoa elimu ya masharti ya mikopo hiyo kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

(a) Upatikanaji wa mikopo kwa wakulima ni mojawapo ya changamoto kubwa katika sekta ya kilimo. Takwimu zinaonesha kuwa mikopo inayotolewa kwa wakulima ni asilimia 12 ya mikopo yote inayotolewa na Benki nchini kwa mwaka.

Katika kuhakikisha wakulima nchini wana sifa za kukopesheka, Serikali kupitia Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenizesheni ya Ushirika inatekeleza mpango wa

kufufua, kuimarisha na kuendeleza vyama vya ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernization Programme (CRMP)*).

Mheshimiwa Spika, kuitia mpango huo vyama vya ushirika vinahimizwa kuweka uongozi makini kuitia uchaguzi katika wakati uliopangwa na kuwapatia mafunzo viongozi na wanachama. Lengo ni kuwa na vyama ambavyo vina sifa za kuwa hai kiuchumi, vyenye wanachama wengi na ambao wanachangia. Hivyo chama kuwa na mtaji unaokidhi mahitaji ya wanachama ili chama kiwe na sifa za kuwa na uwezo wa kuhudumia wanachama wake.

Sifa hizo zinachangia kukifanya chama kikopesheke na hivyo kukiongezea mtaji wa kuhudumia wanachama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri inaendelea na uhamasishaji wa uundwaji wa vikundi imara vya wakulima ili wakulima wasio na sifa za kukopesheka wapate fursa ya kupata mikopo kuitia vikundi au vyama vyao au vyama vya ushirika.

Kwa mfano, kuitia utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani katika msimu wa 2010/2011, vyama vya Ushirika vya msingi 345 katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani viliwezeshwa na kupata mikopo kwa ajili ya ununuvi wa zao la korosho.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeiagiza *TIB* kutenga asilimia 5 ya fedha za Mfuko wa Dirisha la Kilimo kwa ajili ya kugharamia mafunzo na elimu kwa wadau wa dirisha hilo. Fedha hizo hutumika kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima ili waboreshe utendaji na uandaaji na kuwa na sifa za kukopesheka.

Aidha, Serikali inahakikisha kwamba *TIB* inazifundisha taasisi za fedha hususan Benki Jamii, *SACCOS*, vikundi na Vyama vya Ushirika, kuwapatia wakulima mafunzo juu ya uandaaji wa mipango ya biashara (*Business Plans*) na umuhimu wa mikopo na usimamizi wake.

*TIB* kuitia vyombo vya habari, itaendelea kutoa elimu ya mikopo na usimamizi wake kuitia mikutano, makongamano na maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Saba Saba na Nane Nane na kadhalika.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kama alivyomaliza kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la fedha hizi ambazo zinatengwa asilimia 5 kwa ajili ya mafunzo ya wakulma wanafundisha wapi kwa sababu kule Solwa na kule Kisese nadhani hata na sehemu zingine za Waheshimiwa Wabunge hakuna mafunzo haya, hatujawahi kuyaona. Sasa yanatolewa wapi?

Swali lingine la pili ni kwamba Serikali ilijiandaa ikaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba hati za kimila zinatumika kama zamani.

Lakini mpaka sasa hivi mashamba mengi hayajapimwa. Kule Kisera hakuna shamba la mkulima hata mmoja lililopimwa na kupatiwa hati miliki. Tunataka hawa wakulima wawe na sifa. (*Makofi*)

Sasa Serikali inatoa tamko gani la kuhakikisha kwamba mashamba ya wakulima wetu yanapimwa na wanapata hati za kimila na kuwa na sifa za kukopesheka benki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TIB* ilizinduliwa muda si mrefu, mwaka jana, hili dirisha analolizungumzia ni mwaka jana tu Mheshimiwa Rais amelizindua pale Dar es Salaam, kwa hiyo, shughuli ndiyo zimeanza. Tayari baadhi ya wakulima wanakwenda kwenye Ofisi za *TIB* pale Mlimani City na wanaendelea kupata mafunzo. Sasa suala la kuendelea kufundisha siyo suala ambalo linaweza kufanyika tu mara moja unazindua dirisha, saa hiyo hiyo nchi nzima ipate mafunzo. Kwa hiyo, kama nilivyosema, Serikali kupitia *TIB*, itaendelea kusambaza mafunzo haya kwa wakulima taratibu mpaka tutakapohakikisha kwamba, wakulima wote wamefikiwa. Kwa hiyo, ni shughuli ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupimwa mashamba ni kweli ninakubaliana na yeze suala la kupima mashamba ili wakulima wapate Haki Miliki na hasa zile Haki Miliki za Kimila ni suala la msingi. Nakumbuka kuna sehemu moja ambayo tayari kabisa wakulima wameweza kufanikiwa na wameweza kukopa hata matrekta, lakini gharama ya upimaji ndiyo kubwa na hata hivyo tunaendelea kujitahidi kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kwamba, mashamba haya yanapimwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa nashauri siku zote kwamba, mashamba hasa ya kilimo cha umwagiliaji ambayo hayawezi kuendelezwa bila kupimwa, ndiyo hasa ambayo tunatakiwa tuanje nayo. Maana ukishayapima haya kwa ajili ya kilimo, unawenza pia ukaingiza humo humo upimaji kwa ajili ya kupatia Haki za Kimila.

**MHE. SALIM HASSAN TURKY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa lengo mojawapo la mikopo kwa wakulima ni kuwasaidia wakulima kupata mikopo kwa njia nafuu; lakini cha kushangaza sana ni kwamba wakulima wanapokwenda kutafuta mikopo wanakumbana na urasimu ule ule; je, kuna tofauti gani kati ya mikopo hii ya wakulima na mikopo ile ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sijui kama kweli kuna tofauti kubwa katika mikopo, lakini jambo la msingi hapa ni kuwa na dhamana, ndiyo jambo tunalolizungumza. Tunaposema wakulima hawakopesheki, mabenki yanapokuwa mara nyingi yanakataa kuwakopesha ni

yale masharti ambayo yamo mle kwamba, unapotaka kukopa ni lazima uwe na dhamana, uwe na *collateral*. Sasa wakulima mara nyingi *collateral* zao ni kama hazipo, maana wanatakiwa wawe na mashamba hayo ambayo yamepimwa. Mikopo mingine unakuta wanataka labda wapewe kwa ajili ya *collateral* zile ambazo ni nyumba au mali nyingine ambazo hazihamishiki.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba, tunachokifanya sasa ni kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata zile *collateral* ambazo ni sifa ambazo si rahisi wao kuzipata, sawa na wale watu wengine ambao wapo sehemu za mijini. Kwa hiyo, sasa tunataka waweze kutumia mashamba yao yapimwe. Ukienda kwa *TIB* siyo mashamba tu, tunawaruhusu hata kwa kupitia kwenye *SACCOS* zao waweze kudhaminiwa ili angalau kulainisha hayo masharti.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kifupi tu, sijui kama nimekidhi swal la Mheshimiwa Salim?

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na mkopo ambao utakidhi uboreshaji wa kilimo katika sehemu ya mkakati ni lazima tuangalie kwamba, *TIB* iliyo na Makao Makuu Dar es Salaam, bila kuwa na tawi au bila kuwa na *Window of Lending* kila Mkoa, itashindwa kutekeleza kazi zake. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba sasa ni wakati tuzungumze ni namna gani tutapanua huduma hii ya *TIB* au dirisha hili lienezwe katika benki zilizopo kwa mkakati maalum ili wakulima wanufaikie na mkopo huu badala ya kuwa Dar es Salaam peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kwamba; ni kweli na mimi naona ni wakati muafaka. Kama nilivyosema, *TIB* sasa dirisha hili ndio linaanza, ipo haja ya kufanya mazungumzo na kutazama namna ya kupanua huduma hii katika nchi nzima.

Na. 6

### **Bei ya Uhakika kwa Zao la Tumbaku**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Tumbaku ni Zao la Biashara kwa Wakulima wa Mkoa wa Tabora lakini Wakulima wameshindwa kujikwamua kiuchumi kwa kukosa bei ya uhakika kutokana na kampuni zinazonunua tumbaku hiyo kujipangia bei wanazotaka wao bila kujali gharama za uzalishaji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahakikishia wakulima soko na bei ya kufaa ili kuinua pato lao na la Taifa kwa ujumla?

(b) Kampuni ya TLTC na AOTTL mwaka 2010 walinunua tumbaku kwa wakulima kwa wastani wa Dola za Kimarekani 2.12 sawa na shilingi 3,180 na mwaka wa

huu 2011 wanataka kununua tumbaku chini ya kiwango hicho, yaani TLTC kununua kwa dola 1.64 na AOTTL kwa dola 1.59; je, katika hali ya namna hiyo Serikali inawasaidiaje Wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilito, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bei za tumbaku kwa mkulima hujadiliwa na kuamuliwa na Halmashauri ya Tumbaku Tanzania, kwa mujibu wa Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya Mwaka 2001. Hivi sasa kuna makampuni matatu yanayonunua tumbaku nchini. Makampuni hayo ni *Tanzania Leaf Company (TLTC), Alliance One Tobacco Tanzania Ltd. (AOTTL)* na *Premium Active Tanzania Ltd. (PATL)*.

(b) Bodi ya Tumbaku Tanzania na Idara ya Maendeleo ya Ushirika, hushiriki katika Halmashauri kushauriana na wadau kwa ajili ya kupata muafaka wa bei inayolinda maslahi ya pande zote mbili. Masuala yanayozingatiwa katika majadiliano hayo ni gharama za uzalishaji, mwenendo wa mahitaji na ugavi wa tumbaku na bei katika Soko la Dunia. Wakulima kuititia ushirika wao, wanapata fursa ya kujadiliana masuala ya masoko na bei ya zao lao. Katika msimu wa 2009/2010, bei ya wastani iliyofikiwa kwenye mauzo ya tumbaku nchini ilikuwa Dola za Kimarekani 2.34, sawa na shilingi 3,510 kwa kilo moja.

(c) Mheshimiwa Spika, msimu wa kilimo wa mwaka 2011, Kampuni ya TLTC inapendekeza inunue tumbaku kwa Dola za Kimarekani 1.64, sawa na shilingi 2,460 na AOTTL inapendekeza inunue kwa Dola 1.59, sawa na shilingi 2,385 kwa kilo moja, kwa madai kuwa biashara ya tumbaku duniani inayumba. Aidha, inakisiwa kuwa, kuna albaki ya takriban tani 450,000 za tumbaku ya msimu wa 2009/2010 ambazo hazijauzwa na makampuni yanayonunua tumbaku ya wakulima hadi sasa kutokana na kushuka kwa mahitaji ya tumbaku kwenye viwanda vinavyotengeneza bidhaa za tumbaku kama vile sigara.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ya bei ya TLTC na AOTTL bado hayajakubaliwa. Majadiliano yanaendelea kufanywa na wanunuvi hao ili kusiwepo na anguko kubwa la bei chini ya kiasi kilichopendekezwa na makampuni haya. Majadiliano zaidi yataendelea kufanywa na Serikali ili kuhakikisha kwamba, maslahi ya mkulima yanalindwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa ukiritimba kwenye suala zima la ununuvi wa tumbaku linatokana na makampuni ya tumbaku kupewa uhuru kupita kiasi; kiasi kwamba wanafanya lolote wanilotaka kwa muda wanaotaka; na kwa kuwa Serikali inatambua

mchango wa Zao la Tumbaku kwenye uchumi wa Taifa; sasa Serikali iko tayari kusimamia soko la tumbaku kama ilivyofanya kwa soko la korosho wakulima wakainuka ikiwa ni pamoja na kuandaa adhabu kwa makampuni yanayonunua tumbaku pale yanapokiuka makubaliano?

(ii) Kwa kuwa kikao cha wadau wa tumbaku kilichopita cha mwaka juzi (2009), makampuni yalishauri wakulima waongeze uzalishaji wa tumbaku zaidi ya mara mbili; na kwa kuwa wakulima walikubaliana na pendekeso hilo na hivyo wakajiandaa kuzalisha zaidi na walijiandaa kuzalisha kutoka *kilogram* milioni 50 mpaka milioni 108; na kwa kuwa mwaka jana makampuni ya tumbaku yalisema yatanunua *kilogram* milioni 50 tu; je, Serikali inaandaa utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba tumbaku inayobaki inanunuliwa kutoka kwa wakulima ikiwa ni kufidia hasara ili wakulima wale wasiendelee kuanguka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, sehemu ya mwisho nimesema, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wanunuzi na lengo letu ni kuhakikisha kwamba, wakulima hawalaliwi na makampuni hayo; na ndiyo maana tumesema kwamba, bado hatujakubali bei zao. Kwa sababu hiyo, Serikali itaendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba, bei zinazopangwa siyo zile ambazo zinamwumiza mkulima.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili ni kwamba, mpaka hivi tunavyozungumza, Serikali imechukua hatua. Nimesema kuna albaki ya karibu tani 450,000 za tumbaku ambayo bado haijanunuliwa. Kwa hiyo, sasa Serikali imeamua kuanza kutafuta soko katika masoko yale ambayo siyo *traditional, non-traditional buyers* wa tumbaku kama China na Iran. Hivi ninavyozungumza ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, anaondoka kwenda Iran kutafuta masoko ya tumbaku ili tumbaku yetu ambayo haijanunuliwa iweze kununuliwa. Tunaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba, tumbaku iliyopo inanunuliwa yote bila kumwumiza mkulima.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda nifahamu, kwa vile Serengeti ilikubalika na Serikali waanzishe kilimo cha tumbaku kwa majaribio; ningependa nipate tarehe *exactly* ni lini majaribio hayo yanakwisha? Pamoja na hayo; huyu mnunuzi pekee aliyepo, *Kenya Alliance One Ltd.*, ni ukiritimba na ni kwa nini kusiwe na mbia mwingine ili kupunguza ubanaji wa bei na pia kunyanyasa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu kwa kifupi swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda nikiri tu kwamba, sijafuatilia kama majadiliano yamekamilika, maana tulikuwa tumetenga kwamba mpaka kufikia mwisho wa mwezi Machi tuwe tumpata majibu. Hadi sasa mimi binafsi nilikuwa sijapata, lakini ninaamini kwamba, hayo majadiliano yamefanyika. Naomba labda baadaye kidogo niweze kukupa taarifa kwamba, hayo majadiliano yamefanyika maana ametaka kujua tarehe ya kukamilika kwa majadiliano hayo.

Na. 7

**Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd* Kujenga Mgodi wa  
Dhahabu Singida Mashariki**

**MHE. TUNDU A. LISSU** aliuliza:-

Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd* imepewa leseni ya kutafiti madini ya dhahabu katika Jimbo la Singida Mashariki katika Kata za Mang'onyi, Issuna na Mhintiri na Kampuni imeshatangaza kujenga mgodi wa kisasa kwenye maeneo ya leseni yake na tangu mwaka 2006 Kampuni ilishatwaa ardhi zinazomilikiwa na wananchi kwenye maeneo ya Kinyamberu, Taru na Sambaru:-

(a) Je, ni Wananchi wangapi bado wanaishi kwenye maeneo yaliyoathiriwa na yatakayoathiriwa na mgodi na ni wangapi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa kuombwa kwa maandishi na Kampuni hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Madani, Sura ya 116?

(b) Je, ni Wananchi wangapi ambao maeneo yao yameshafanyiwa tathmini kwa kulipwa fidia na ni Wananchi wangapi kati ya hao wameshalipwa fidia?

(c) Kama hakuna Mwananchi aliyelipwa fidia kwa mujibu wa Sheria husika; je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ukiukwaji huo wa Sheria?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** aliibju:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd* ilipewa Leseni ya Utafutaji Madini, Namba PL 2792 ya terehe 30 Oktoba, 2004 kwa eneo la ukubwa wa kilometra za mraba 17.9 katika eneo la Sambaru, Wilaya ya Singida, Jimbo la Uchaguzi la Singida Mashariki. Leseni hiyo inatarajiwa kumalizika muda wake tarehe 29 Oktoba, 2011.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Kampuni hiyo umeonesha kuwepo kwa mashapo ya madini ya dhahabu yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Kutokana na

matokeo hayo, Kampuni imeanza kufanya upembuzi yakinifu. Imejiri Kampuni ya *MTLGO Engineering Consultant* kufanya tathmini ya athari ya mazingira katika eneo husika na imewasilisha Wizarani maombi mawili ya leseni za uchimbaji wa dhahabu zitakazojumuisha eneo lote la utafutaji ambalo wanalo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kutohana na sharti la kisheria linalozuwia kutolewa kwa leseni ya uchimbaji madini, yaani *mining license* ya dhahabu kwa eneo linalozidi kilometra kumi za mraba, Kampuni hiyo imelazimika kuomba leseni mbili.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd* inafanya upembuzi yakinifu, ambao taarifa yake itawasaidia katika kufanya uamuzi wa kuwekeza na itaonesha ni Wananchi wangapi wataathirika kwa kiwango gani na mradi huo. Aidha, taarifa ya tathmini ya athari ya mazingira itabainisha orodha ya watakaotakiwa kulipwa fidia na ama kuhamishwa na kujengewa makazi mapya. Serikali pia itapata na kuchambua taarifa ya athari za kijamii na kimazingira na mpango wa kushughulikia athari hizo kutoka kwa Kampuni husika kama sehemu ya masharti yanayotakiwa kutimizwa kabla ya kukamilisha kushughulikia maombi yao ya leseni ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawasihi Wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki, chini ya Mheshimiwa Tundu Antiphasi Lissu, wanaoishi katika maeneo ayatakayotumika kwa shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu, kutoa ushirikiano na kutoa taarifa sahihi kwa Kampuni ya *Shanta Mining* ama Wakala wao wanaopita katika maeneo yao kufanya tathmini ya athari za mazingira ikiwa ni pamoja na kupata orodha ya watakaolazimika kuhama kupisha shughuli hizo za uchimbaji wa madini ili wakati utakapowadia, waweze kuhamishwa na kufidiwa na ama kujengewa makazi mapya.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba, Kampuni ya *Shanta Mining* imepewa leseni katika Kijiji cha Sambaru tu. Je, ni kwa nini hii Kampuni imechukua maeneo ya Wananchi kwa nguvu katika Kitongoji cha Kinyamberu, Kijiji cha Mwau, katika Kitongoji cha Taru, Kijiji cha Mang'onyi; na ni kwa nini imejenga uwanja wa ndege katika mashamba ya Wananchi bila kuwapa fidia? Kwa nini Serikali isichukue hatua za kuwashtaki kijinai kwa *criminal trespass?* (*Makofî*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tundu Antiphase Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nifafanue kupitia Bunge hili Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba, kwa mujibu wa maelekezo ya Bunge Tukufu na hasa kwa kupitia Kanuni zetu, majawabu yetu yanatakiwa yaye mafupi, yakiwa yanmejielekeza kwenye swali liloulizwa. Kwa maeleo haya, ni sisi Wizara yetu kutoa *reference*, kutoa rejea ya maeneo ambayo Kampuni ya *Shanta Mining* imepewa katika maeneo ya Sambaru ni urahisishaji wa maeneo ambayo wamemilikishwa na wamepewa leseni kisheria. Haina maana kwamba, eneo hilo ndiyo liwe Sambaru, Kitongoji cha

Sambaru peke yake. Kwa hiyo, tulichokuwa tunamaanisha hapa ni rejea kwa urahisi wa kuelewa *Shanta Mining* wanafanya wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini pili ni kwamba, kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizonazo, haiwezekani na siyo kwamba Kampuni ya *Shanta Mining* imechukua hili eneo la kwenye kile kiwanja chao walichonacho, ile *air strip* ndogo waliyonayo, pamoja na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema kwa nguvu; si kweli. Maeneo yote ambayo wanayafanya kazi na mimi nimefika pale mwaka 2007, eneo lile ninalifahamu na wamepewa kisheria na sheria siku zote imekuwa ikituongoza na Serikali tunasimamia kuhakikisha kwamba, hawatoki nje ya eneo hilo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, eneo hilo liko ndani ya mamlaka ya kisheria. Ahsante sana. (*Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 63 (1), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 64 (1) (a), kutokusema uwongo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Madini na Nishati amesema uwongo Bungeni na ninaomba chini ... (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa, kwa sababu ya kutumia muda, tunao utaratibu mwingine. Naomba ieleweke hata ukishasema hivyo, hutegemei Kiti hiki kujua kwamba sasa huu ni uwongo au sivyo. Ndiyo maana tunatoa nafasi ukajiandae vizuri kusudi uwongo huu tuufahamu.

Sasa ukisema hapa mimi sitajua wewe unasema uwongo ama yeze anasema uwongo. Kwa hiyo, sasa ili tuokoe kipindi cha maswali, tumalize kazi hii, wewe una nafasi ya kueleza kabisa uwongo aliousema Mheshimiwa na tutakwambia lini ulete.

Naomba tuendelee. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kilichotokea katika Jimbo la Mheshimiwa Tundu Lissu kinafanana sana na kile kinachotokea Tunduru, Jimbo la Tunduru Kusini, Kata ya Mbesa; sasa hivi kuna machimbo pale yamegundulika ya shaba na Wananchi wengi wameanza kujihusisha katika uchimbaji huo. Vilevile cha kushangaza kuna wawekezaji amba Serikali hatuna uhakika kama inawatambua. Sasa nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri je, anaweza akatuma timu ya wataalam katika Jimbo la Tunduru Kusini, Kata ya Mbesa ili kwenda kutathmini na kujua hali halisi ilivyo katika eneo hilo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu kwa niaba ya Serikali, tuko tayari kutuma timu kwenda kufanya uchunguzi katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ametuomba. Ahsante sana.

Na. 8

**Tatizo la Maji - Handeni**

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Tatizo la maji kwa Mji wa Chanika - Handeni ni changamoto kubwa kwa Mji huo ambao hivi karibuni utakuwa Halmashauri ya Mji wa Handeni:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuupatia Mji huo maji ya kutosha kutokea Mzeri, Itake kupitia Misima, Kwenjugo hadi Chanika ili kumaliza kabisa tatizo la maji?

(b) Ili utekelezaji wa Mradi huo uweze kuanza; je, Serikali ipo tayari kuanza upembusi wa awali ili kujua gharama zake ili Mradi uanze kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Kitaifa wa Handeni, *Trunk Main (HTM)*, pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Handeni, ndiyo wenye jukumu la kutoa huduma ya majisafi kwa Wakazi wa Handeni pamoja na vijiji vilivyopo kwenye eneo la Mradi. Miundombinu ya Mradi huo imechakaa na haikidhi mahitaji ya maji ya sasa.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kijerumanzi (GTZ), inafanya upembusi wa awali wa upanuzi na ukarabati wa Mradi wa HTM (*Feasibility Study for Rehabilitation and Extension*). Mhandisi Mshauri (*Hydroplan* kutoka Ujerumanzi), akishirikiana na Kampuni ya ITECO ya hapa nchini, ameanza kazi mwezi Agosti, 2010. Matokeo ya upembusi wa awali yatakamilika mwezi Juni, 2011. Taarifa ya Mhandisi Mshauri itabainisha maeneo kwa ajili ya vitekeo vya maji vitakavyokidhi mahitaji kwa Mji ya Kwenjugo, Chanika na Misima.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la (a), upembusi wa awali umekwishaanza. Hivyo, tatizo la maji maeneo ya Mkata, Handeni Mjini, Komkonga, Kabuku, Michungwani/Segera na Kwamkono, litamalizika baada ya kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa Mradi huu.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(i) Kwa kuwa Wilaya ya Handeni ni karibu asilimia zaidi ya 30 ya Mkoa wa Tanga; na kwa kuwa *intake* ya sasa ya HTM mpaka Makao Makuu ya Wilaya ni karibu kilomita 65 mpaka 70; na kwa kuwa *intake* ya Mzeri ni kama kilomita 25; je, Serikali haioni kwamba utaratibu wa kuchukua maji kutoka *intake* ya Mzeri itaongeza jitihada ya kupunguza tatizo la maji hata kama HTM itakuwa inahudumia maeneo mengine kwa Jimbo kubwa kama hili?

(ii) Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja Handeni tumwonyeshe *intake* ya Mzeri iko wapi ili aelewé ni kwa ukaribu gani Mji wa Handeni unaweza kupata maji hivi sasa kuliko tunavyopata maji kutoka *intake* ya Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kama tungeweza kuchukua maji Itake, Mzeri ni kweli kwa sasa ndiyo tunachukua katika Mradi huu wa Handeni na ndiyo maana kwa sababu ya umbali imeonekana kuna upotevu mwangi sana wa maji. Sasa kwa sababu tumemwajiri Mhandisi Mshauri, ye ye ndiyo atakayesema ni wapi tutapata maji yanayokidhi mahitaji ya sasa. Kwa hiyo, tingoje Ripoti ya Mhandisi Mshauri ili tuweze kupima pamoja na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge na hayo atakayopendekeza ye ye ndiyo tutakapokuwa maji kwa ajili ya mahitaji ya sasa ya Mji wa Handeni.

Katika swali la (b), nashukuru kwa kukaribishwa kufika Handeni, nitafika na watalam wangu tuweze kuiona hiyo Itake na kuweza kushauriana namna gani ya kuweza kuumaliza Mradi huu. Ahsante.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa lipo tatizo kubwa la maji eneo lote la Jimbo la Bumbuli na hasa kwenye Kata ya Bumbuli, Vijiji vya Bumbuli Kaya, Bumbuli Mission na Bokoyi; na kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji wa Mradi wa Benki ya Dunia kutokana na taratibu za Mhandisi Mshauri; na kwa kuwa kwenye Halmashauri pale tunao wahandisi ambao wanajulia vizuri eneo wamepitia michoro: Je, Serikali iko tayari sasa kuruhusu Wahandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto watekeleze Mradi huu?

**SPIKA:** Swali la nyongeza haliwezi kuwa refu; ni moja tu.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Makamba, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji unatekelezwa kwa usimamizi wa Halmashauri za Wilaya na katika Bunge lililopita tulitoa taarifa ya hali halisi ya kila Halmashauri ya Wilaya. Sasa wahandisi waliopo kule hawajazuiliwa kutekeleza Mradi huu; ni kwamba, ni lazima twende kwa awamu; Benki ya Dunia inataka ukimaliza *stage* ya kwanza upate kitu kinachoitwa *no objection* ndiyo unakwenda awamu ya pili. Kwa hiyo; ni lazima tufuate utaratibu huo. Tulishakubaliana na hawa washirika wa maendeleo kwamba, lazima tufuate utaratibu huo ili tuweze kufikia matokeo ambayo ni mazuri.

Na. 9

### **Madai ya Katiba Mpya**

#### **MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR** aliuliza:-

Wakati kuna madai makubwa ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuwaelimisha Wananchi wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani hasa wale walio vijijini juu ya Katiba iliyopo ili watoto michango sahihi ya kupata Katiba mpya?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, iko haja ya kutoa elimu kwa kutumia njia mbalimbali hata kwa kufanya semina mijini na vijijini ili Wananchi waweze kutoa mchango wa mawazo mazuri ya kutufikisha mahali pa kupata Katiba mpya na nzuri?

#### **WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja na kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa utungaji wa Katiba mpya, Serikali imeona kuwa, ipo haja ya kutoa elimu kwa Wananchi wote kuhusu Katiba inayotumika hivi sasa. Serikali inaanini kuwa, ikiwa Wananchi wataelimishwa kuhusu Katiba inayotumika hivi sasa, watakuwa katika nafasi nzuri ya kuchangia maoni yatayotuwezesha kupata Katiba nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume itakayoundwa kuratibu zoezi zima la utungaji wa Katiba mpya, inakusudia kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu Katiba inayotumika hivi sasa. Aidha, Serikali itashirikiana kikamilifu na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Katiba inayotumika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Muswada unaopendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (*The Constitutional Review Act, 2011*), ambao pamoja na mambo mengine, utaanzisha Tume itakayoratibu zoezi la utungwaji wa Katiba mpya umekamilika na utawasilishwa katika Mkutano huu kwa hatua zenu muhimu. Muswada huo sanjari na kuainisha majukumu mengine ya Tume, utaainisha jukumu la Tume hiyo la kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu Katiba inayotumika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu tutakaowasilisha katika Bunge lako hili Tukufu kama ulivyobainisha wenyewe katika sehemu ya jina refu, unatarajiwa kutungwa kwa Sheria itakayoanzisha Tume ya Kuratibu Maoni ya Mchakato wa Katiba mpya. Utaratibu utakaotumiwa na Tume kuratibu maoni ya wadau na mambo mengine yanayohusiana nao siyo Muswada wa Katiba mpya.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Wananchi wote wa Tanzania wanaizungumzia Katiba hii mpya; na kwa kuwa Serikali kwa ujumla nayo imetoa uhuru kuchangiwa Katiba hii; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa na mbinu gani ya ziada kuwafanya Watanzania kuwa na uhuru mkubwa wa kuweza kuichangia Katiba hii?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia, kama ifuatavyo:-

Mimi ningeomba Wabunge wasubiri tuwasilishe huo Muswada watachangia kwa kirefu. Vilevile ninaomba tuwaeleweshe Wananchi kwamba, huu siyo Muswada wa Katiba; ni Muswada ambao tunaunda Tume ya kufikia huko kwenye Katiba mpya. Kwa hiyo, Wananchi waelewe hivyo na watapata muda wa kujadili hiyo Katiba mpya; sasa hivi tunajadili mchakato tu wa Tume, Katiba mpya itakapojadiliwa Wananchi watapata muda mrefu sana wa kujadili Katiba hiyo. (*Makofî*)

Na. 10

### **Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. MARGARETH AGNES MKANGA** aliuliza:-

Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ilikwishatungwa na kuitishwa na Rais:-

- (a) Je, ni lini kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo zitakamilishwa ili Sheria iweze kutekelezwa?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuwaelimisha walengwa na jamii kwa ujumla kuhusiana na Sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
**(K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ningependa kujibu swalii la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu tayari ilikwishatungwa na Bunge lako Tukufu na baadaye kuridhiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Mei, 2010. Taratibu za kuandaa Kanuni za Sheria za Watu Wenye Ulemavu zinaendelea kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wadau mbalimbali. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2011. Mara baada ya Kanuni kukamilika, zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu inatarajiwa kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2011. Aidha, tangazo la kuanza kutumika kwa Sheria hii tayari limekwishawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mpango madhubuti wa kuwaelimisha watu wenyewe ulemavu na jamii kwa ujumla, kuhusiana na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu. Mpango huu unaainisha masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili, kuandaa vipeperushi ya ufanuzi wa Sheria, kutoa elimu ya sheria kwa umma kwa njia ya televisheni, redio, vikundi vya sanaa na mafunzo ya ana kwa ana kwa vikundi vya watu wenyewe ulemavu na wadau mbalimbali hususan mashirika yanayojihusisha na utekelezaji wa Haki za Binadamu.

**MHE. MARGARETH AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa jibu lenye matarajio mazuri, lakini naomba kuuliza tu swalii dogo la nyongeza. Huu mpango madhubuti wa uelimishaji utaanza lini kwa sababu sioni kama itakuwa busara kuanza kutumika Julai Mosi mwaka huu na bado haijatafsiriwa hiyo Sheria kwa Kiswahili; je, wadau watajuaje? Lini mpango huu madhubuti unaanza hasa (*time-frame*)?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
**(K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi na Jamii, ningependa kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Margareth Mkanga, kama ifuatavyo:-

Kweli sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2011 lakini kwa mujibu wa taratibu za kisheria, Sheria itaanza kufanya kazi baada ya kuwa tayari tuna kanuni ambazo ziko kwenye hatua za mwisho za kukamilika. Kwa hiyo, tunategemea wakati kanuni zinaanza kufanya kazi, hapo hapo tutazindua mpango wa kuielimisha jamii kuhusu haki za watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme haki za watu wenyewe ulemavu hazitekelezeki kwa kutumia Sheria hii peke yake, ukisoma Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inazungumzia haki ya watu wenyewe ulemavu. Kwa hiyo, tayari tunaendelea kuielimisha jamii, kwa kutumia Sheria mbalimbali na kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ili jamii iweze kufahamu haki za watu wenyewe ulemavu. Ukitazama TV na vipeperushi mbalimbali, tayari tumeshaanza utekelezaji wa mkakati huo.

Na. 11

### **Utekelezaji wa *Mtwara Development Corridor***

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Mwaka 1979 katika Mkutano wa SADC pamoja na mambo mengine, uliibua suala zima la *Mtwara Corridor* unaohusisha Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Mbeya, Morgoro na Mkoa wa Pwani:-

- (a) Je, Mkataba wa Utekelezaji huo umeshaletwa Bungeni ili kuridhiwa na Bunge na hatimaye utekelezaji wake uanze?
- (b) Je, mpaka sasa Serikali imeteketeza Miradi hiyo kwa kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkataba kati ya Nchi za Malawi, Msumbiji, Tanzania na Zambia, uliotiwa saini tarehe 25 Desemba, 2004 ni Mkataba wa Ushirikiano katika nyanja za kiuchumi, kibiashara na kijamii. Mkataba huo unalenga uanzishwaji wa miundombinu ya uhakika baina ya nchi husika ili kufungua uwekezaji na biashara. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Mkataba wa Ushirikiano ni wa kiutendaji zaidi, Mkataba huo haujawahi kuletwa Bungeni ili kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Kamati za Ufutiliaji ndizo zinazoshauri juu ya maendeleo ya Kanda.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama zilizotumika kwa ajili ya msaada wa kiufundi, yaani *technical assistance*, kufanya utafiti wa Miradi ya Mchuchuma na Liganga na kujenga Daraja la Umoja (*Unity Bridge I*) na la Mitomoni (*Unity Bridge II*) kati ya Tanzanian na Msumbiji na Mradi wa Umeme wa Umoja ujulikanao kama Umoja Light ni Dola za Kimarekani milioni 1,138.4. Fedha hizo zilitolewa na Serikali ya Tanzania, Afrika ya Kusini na Msumbiji. Aidha, Miradi ambayo inaendelea kutekelezwa ni ujenzi wa Barabara ya Masasi hadi Mangaka (56 km) itakayogharimu Dola za Kimarekani milioni 5.5 na itagharimiwa na Serikali ya Japani; na Miradi ya Makaa ya

Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, itakayogharimu jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 3.0. Fedha hizo zitalipwa na wawekezaji kutoka China. Vilevile Barabara za Namtumbo hadi Songea (67 km), Peramiho hadi Mbinga (78 km) na Tunduma hadi Sumbawanga (224 km) zinafadhiliwa na Shirika la *Millenium Challenge Corporation (MCC)*.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ambayo nimepewa lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwanza, nilitaka huu mradi ufikishwe Bungeni ili upate kibali cha Bunge ili Bunge liweze kuufuatalia; vinginevyo, Bunge haliwezi kuufuatalia kama Mradi haujaletwa Bungeni ili upate ridhaa ya Bunge.

(ii) Tangu Mradi huu uanze kuibuka ni takriban miaka 32 sasa na Miradi iliyotajwa kutekelezwa kwa kweli ni michache sana, ukiacha Mikoa ya Rukwa, Iringa, Lindi, Mtwara, Mbeya, Ruvuma, Morogoro na Pwani, baadhi ya mikoa haijaguswa kabisa na Miradi ya Mtwara Corridor. Ninaomba sana suala hili lizingatiwe na Miradi hii itekelezwe. Tunataka kufahamu ni lini itawekwa mikakati madhubuti ili mikoa mingine iweze kuguswa vilevile ambayo haijaguswa katika miradi ambayo imetajwa hapa? Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swalii la msingi, Miradi hii ni ya kiutendaji zaidi na Serikali inawakilishwa na Kamati ya Wataalamu wa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Serikali imewakilishwa vilevile na Kamati Maalum ya Wataalamu inayojulikana kama Kamati ya Makatibu Wakuu, ambayo imekuwa chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu au Ujenzi kwa hivi sasa na Kamati ya RCs wa maeneo yanayohusika na Mikoa ambayo Mradi huu unapitia.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niseme kwamba, katika utekelezaji wa *Mtwara Corridor*, Serikali imefanya mambo mawili; kwanza, imeainisha kwa kushirikiana na Serikali ya Afrika Kusini katika msaada ambao ultolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Afrika Kusini kwa kushirikiana na NDC, tukaainisha Miradi 100. Miradi hii ina jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 12 na inategemewa itakapokamilika italeta mapato ya bilioni 1.8 kila mwaka na itatengeneza kazi za watu 300,007 itakapokuwa imekamilika. Aidha, Miradi kumi ndiyo ambayo imepewa kipaumbele ili iweze kutekelezwa na Mheshimiwa Mbunge atakapotaka nitampatia orodha ya Miradi hiyo ambayo inaunganisha na Mradi wa Makaa ya Mawe na Mchuchuma, Ngaka, Reli ya Mchuchuma, yaani itakayotoka Mchuchuma mpaka Mtwara, Bandari ya Mtwara na Miradi mingine katika hii Miradi kumi niliyoisema.

Azma ya Serikali ni kufungua eneo la *Mtwara Corridor*. Pia ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, maendeleo ya eneo hili yatagusa siyo tu Mikoa ambayo tumeitaja Mkoaa wa Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya na Mikoa ya Morogoro na Pwani, sehemu za Kusini mwa Mto Rufiji lakini italeta maendeleo kuunganisha na nchi ambazo zinatuzunguka.

### **Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Songwe umechukua muda mrefu kukamilika na mara kwa mara Serikali imekuwa ikitoa majibu yasiyo na uhakika:-

- (a) Je, ni lini sasa uwanja huo utakamilika?
- (b) Je, Serikali imejiandaaje kuhakikisha kunakuwepo na vivutio vya kutosha vya kuvutia uwekezaji ili kuinua uchumi katika Nyanda za Juu Kusini ?
- (c) Kulingana na ukubwa wa uwanja huo ni ndege zenyе uwezo na ukubwa kiasi gani zitabeba abiria wangapi na mizigo yenye uzito wa tani ngapi zitawezza kutumia uwanja huo ?

### **NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe utakamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa 2011.
- (b) Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanya mikutano na wadau mbalimbali Mkoani Mbeya kuhusu fursa za maendeleo na vivutio vya uwekezaji katika Mikoa wa Mbeya na Mikoa ya jirani ya Iringa, Ruvuma, Rukwa na Katavi na jinsi Kiwanja cha Ndege cha Songwe kitakavyoweza kuchochea maendeleo ya Mikoa hiyo. Kwa sasa Wizara kupitia mamkala ya Viwanja vya Ndege imepokea maombi kuhusu uwekezaji katika maeoneo ya hoteli, huduma za mafuta ya ndege, maduka na benki katika eneo la kiwanja.
- (c) Ndege za abiria zitakazohudumiwa na kiwanja ni ndege kubwa zenyе uwezo wa kubeba abiria 150 kama vile ndege za aina ya *Boeing 737-800* au *Airbus A320*. Ndege za mizigo ni zile zenyе uzito wa juu wakati wa kuruka, yaani *maximum takeoff weight* wa wastani wa tani 100 za mizigo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na pia Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya jirani ya Iringa, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Katavi, kuwashamasisha Wananchi katika Mikoa yao ili watumie fursa ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kuanzisha kilimo cha mbogamboga, matunda na maua ili bidhaa hizo ziweze kusafirishwa na kuuzwa nje kupitia kiwanja hicho na hivyo kuingiza kipato katika Mikoa hiyo pamoja na taifa kwa ujumla.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa uwanja huu wa Songwe umekaribia kukamilika. Mimi niliutembelea Uwanja huu wa Songwe mwezi wa Februari nikakuta kuna *control tower, terminal building* pamoja na *fire station*; ni majengo ambayo ni magofu ya muda mrefu ambayo yamekuwa yakisusua. Kwa kuwa mkataba wa mkandarasi pamoja na Wizara husika *components* hizi hazipo; je, Serikali ina mkakati gani katika kulikamilisha hilo?

(b) Wenyeji wa Kusini mwa Uwanja huo hawana *access* ya barabara, huwa wanakatiza pamoja na mifugo yao katika Uwanja huu wa Ndege. Ssa hiyo inapelekea kwamba, Uwanja huu utakapokamilika watakuwa hawana *access* ya kwenda kupata huduma za jamii. Je, Serikali ina mkakati gani katika kukamilisha hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Uwanja huu ulichukua muda mrefu kidogo kwa matengenezo kwa sababu ratiba ilibadilika, mwanzoni ilikuwa ichukue ndege zenye ukubwa wa Foka 28 na ATRs, lakini sasa tumeongeza barabara ya kurukia ndege na hivyo haya majengo mengine yatakarabatiwa katika kiwango kinachohitajika.

Kuhusu utaratibu wa Wananchi pamoja na mifugo kukatiza kwenye uwanja wa ndege; viwanja vya ndege vina uzio na uzio utajengwa na taratibu nyingine zitapatikana ili kusaidia Wananchi kuweza kupata mahitaji yao lakini pia kulinda usalama wao.

Na. 13

**Kubadilisha Miundombinu ya Reli ya TRL na Kuunganisha  
Njia za Reli Nchini**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Kabla Serikali haijaingia ubia na Kampuni ya RITES ya India, Kampuni ya TRL ilikuwa na injini 79 na mabehewa 1,357 na ilikuwa ikipata mapato ya Dola za Kimarekeni milioni 64 kwa mwaka; lakini baada ya kuingia Mkataba na RITES ufanisi umeporomoka na kufikia injini 40 na mabehewa 693 na mapato kushuka hadi kufikia Dola za Kimarekani 45 kwa mwaka na kwamba kiasi cha shilingi trilioni 3.7 zinahitajika ili kuirejesha TRL kwenye utoaji wa huduma za kawaida:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika badala ya kukarabati reli hiyo ibadilishwe kabisa njia ya reli hii na kuweka mataruma mapya ili gharama za uzalishaji zipungue?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha njia ya reli ya TRL na TAZARA ili kuwa na mtandao wa reli nchini?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chritowaja G. Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuitia Mradi wa Reli Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Gitega hadi Musongati unaozishirikisha Nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania, Serikali itaboresha njia ya Reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati. Sehemu hii ya njia ya reli itaboreshwaa na kuongeza upana wake kutoka mita 1.0 hadi mita 1.435 kwa kutandika mataruma na reli mpya. Lengo ni kuhuisha reli hii kuwa na viwango vinavyolingana na vile vilivypendekezwa kujengwa katika reli mpya kutoka Isaka, Tanzania kwenda Kigali, Rwanda na kutoka Keza kwenda Msongati, Burundi. Haya pia ni maamuzi yaliyofikiwa na Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, uboreshaji huu unalenga kuifanya njia hii ya reli kuhimili treni zenye kubeba mzigo mzito na kusafiri kwa mwendokasi wa km 80 mpaka km 120 kwa saa. Hivyo, kuboresha ufanisi na kupunguza ghamama za uchukuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kuziunganisha reli hizi mbili za TRL na TAZARA kwa sababu Shirika la TAZARA linamiliwa kwa pamoja kati ya Serikali mbili za Tanzania na Zambia ambapo km 970 ziko upande wa Tanzania na km 890 ziko upande wa Zambia. Upana wa reli hii ni sawa na upana wa reli nyingine zilizoko Kusini mwa Afrika. Aidha, kwa kuwa uamuzi umekwishapitishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba reli zijengwe kwa kiwango cha upana wa mita 1.435, yaani *Standard Gauge* itakuwa vigumu kwa Serikali kuunganisha njia hizi mbili katika upana mmoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza:-

Je, Serikali inawaambia Watanzania kwamba ni lini sasa utekelezaji wa zoezi hilo la kuboresha njia za reli hususan katika kusafirisha mizigo na zile za kwenda kwa mwendokasi utaanza tena? Je, ni lini Reli ya Kati na ile ya Dodoma itaanza kuboreshwa ambapo Reli ya Dodoma mpaka Singida ilikuwa ni mhimili mkubwa sana katika kusafirisha mazao ya mifugo pamoja na mazao ya chakula na biashara ambayo yanapatikana kwa wingi katika Mikoa ya Singida na Mikoa ile ya karibu kama Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tena kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, uboreshaji wa ujenzi wa Reli ya Kati utaanza mara Waheshimiwa Wabunge watakapopitisha bajeti ya mwaka unaoanza 2011/2012. Tumeomba shilingi bilioni 150 ambazo zitaboresha usafiri katika Reli ya Kati kuelekea mpaka Isaka. Utaratibu huo pia unafanyika katika hizi Serikali tatu, sisi tunahitaji dola bilioni moja, kwa hiyo, inakuja kama shilingi trilion 1.5.

Kuhusu suala la Reli ya Dodoma mpaka Singida hilo pia liko katika mpango wetu wa kuboresha na si mifugo tu, lakini tumekuwa na mazungumzo na wawekezaji kwenye suala la dhahabu na madini mengine ambao wanahitaji hii reli haraka sana na wao wako tayari kushirikiana nasi katika kuboresha usafiri wa Reli hii ya Kati na pia reli inayotoka Dodoma mpaka Singida.

Na. 14

### **Shughuli za Maendeleo Muyowosi na Malagarasi**

#### **MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-**

Wananchi wanaozunguka eneo la Msitu wa Muyowosi na Bonde la Mto Malagarasi wamekuwa wakitegemea maeneo hayo kwa shughuli za kuwapatia kipato kama urinaji asali, kilimo na uwindaji lakini sasa wamezuiliwa na mamlaka husika kuendelea na shughuli zao kwenye maeneo hayo:-

- (a) Je, Serikali inafanya juhudu gani za haraka kuwawezesha Wananchi kuendelea na shughuli zao katika maeneo hayo?
- (b) Je, ni lini Serikali itaweka mipaka katika maeneo hayo ili kuondokana na mgogoro baina ya wakulima na wamiliki wa vitalu?

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhammadi, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Pori la Muyowosi lilipandishwa hadhi kutoka Pori Tengefu na kuwa Pori la Akiba mwaka 1981, ambapo shughuli za kilimo na uwindaji uliokuwa ukifanyika hapo awali kabla ya kupandishwa hadhi pori hilo zilisitishwa, isipokuwa shughuli ya urinaji asali ambayo bado inaendelea kufanyika hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuwasaidia Wananchi kuendelea na shughuli zao hususan urinaji asali, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kuwaruhusu Wananchi kwa kuwapatia vibali maalum ili wapate fursa ya kuingia ndani ya hifadhi kwa ajili ya kurina asali, ikiwa ni pamoja na kupewa ulinzi na askari wa wanyamapori dhidi ya wanyama wakali wakati wa kurina asali. Vibali hivyo pamoja na ulinzi wa askari hutolewa kwa Wananchi ambao wameunda vikundi.

Mheshimiwa Spika, mipaka katika maeneo hayo ipo na inatambulika kisheria. Tatizo lililopo ni Wananchi kuvamia maeneo ya Hifadhi ya Msitu wa Makere, ambao unasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na ndani ya msitu huo kuna vitalu viwili vya uwindaji. Wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiingia ndani ya hifadhi hiyo ya msitu na kufanya shughuli za kilimo.

Katika mazingira hayo, hapo ndipo mgogoro unapojitokeza kati ya wakulima na wamiliki wa vitalu vya uwindaji. Wizara yangu imeanza zoezi la kuweka wazi mipaka ya hifadhi zake na tayari tumeshawaandikia Halmashauri ya Wilaya ya Kasuli ili iweke alama za mipaka kwenye Msitu wa Makere wanaousimamia. Lengo ni kuwa na mipaka iliyio wazi kabla ya mikataba mipy ya uwindaji wa kitalii inayotegemea kuanza mwaka 2013.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, kabla ya kuuliza swali ni kwamba, kwenye majibu yako umesema Wilaya ya Kasulu na swali langu lilikuwa ni Wilaya ya Kibondo.

(i) Serikali ina juhud gani za kupima upya maeneo ya hifadhi na kuwaruhusu Watanzania kuanza kuwinda kwenye maeneo hayo kwani kuruhusu wageni peke yao ni suala la ukoloni mamboleo?

(ii) Tumekuwa tunapoteza mabilioni ya shilingi kutokana na Serikali kushindwa kutoza kodi hoteli za kitalii zilizoko kwenye mbuga hizi. Sasa Serikali ina mpango gani wa kufuata ushauri wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili tuweze kunufaika na pesa hizi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkosamali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Namba 5 ya Mwaka 2009, inayosimamia Sekta ya Wanyamapori. Katika Sheria hiyo, tulianzisha utaratibu wa kuwepo kwa *Wildlife Management Areas* kwenye maeneo ambayo yako nje ya *core protected areas*, yaani nje ya *Game Reserve* na *National Parks*.

Kwa maeneo kama haya ya Makere ambayo yako nje ya *core protected area*, kwa maana ya *Muyowosi Game Reserve*, Wananchi wa maeneo hayo wanashauriwa kuanzisha *Wildlife Management Areas* ili waweze kuyasimamia wenye na kwa kufanya hivyo inakuwa ni rahisi kwao kupata *user right* na kuweza kupata mapato. Aidha, niseme tu kwamba, katika zoezi ambalo tumekamilisha hivi sasa na tumekwisha kutangaza, la vitalu vya uwindaji wa kitalii, kuna maeneo ambayo tumetenga kwa ajili ya wawindaji wenyeji. Katika jumla ya vitalu 172 ni vitalu 156 tu ambavyo vimetangazwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii, vitalu vitano ni kwa ajili ya utafiti pamoja na mafunzo na vitalu vingine vinavyobaki ni kwa ajili ya wawindaji wenyeji pamoja na utalii wa picha. Kwa maana hiyo, kuna maeneo maalum kabisa ambayo yametengwa kwa ajili ya wawindaji wenyeji.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Naomba tumalize maswali tafadhali. Mheshimiwa Kapt. John Komba, naomba uulize swali linalofuata.

Na. 15

### **Mipaka ya Hifadhi ya Liparamba na Eneo la Wananchi**

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Mabadiliko ya mipaka ya Hifadhi ya Liparamba yaliyofanywa na Wahifadhi bila ridhaa ya Wananchi waliopakana nao yamesababisha kutolewana kati yao:-

(a) Je, kwa nini Serikali inawaonea wanakijiji hao kwa kubadili mipaka bila kujali maslahi yao?

(b) Je, Serikali iko tayari kurejea mipaka ya awali ambayo iliridhiwa na Wanavijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga?

### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa; ni kweli kumekuwepo hali ya kutolewana baina ya Serikali na Wananchi hususan kuhusu suala la mipaka ya hifadhi na eneo ambalo hutumiwa na Wananchi kwa shughuli za kilimo. Hali hiyo ya kutolewana ilijitokeza baada ya Wizara kukabidhiwa jukumu la kusimamia Pori la Akiba la Liparamba na kuweka mpaka kwa kufuata vipimo vyta kisasa vyta GPS Coordinates kama zilivyoainishwa katika Tangazo la Serikali Na. 289 la Mwaka 2000.

Hivi sasa Serikali imesimamisha zoezi la kuainisha mipaka hiyo na Uongozi wa Wilaya ya Mbinga umeteua Kamati Maalum ili kutafuta ufumbuzi wa chanzo cha mgogoro ambapo taarifa ya Kamati hiyo itawasilishwa na kujadiliwa kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani na mapendekezo ya Baraza hilo yatawasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko tayari kupokea mapendekezo hayo ya Baraza la Madiwani na kuyafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009. Wakati suala hili linashughulikiwa kwa utaratibu huo, napenda

kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge, kusaidia katika kuwashauri na kuwaelimisha Wananchi ili waendelee kuheshimu mipaka iliyowekwa kisheria kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 289 la Mwaka 2000.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa Serikali imenitaka mimi Mbunge nisaide kuwashauri Wananchi kuheshimu mipaka iliyowekwa kisheria kwa kadiri ya Tangazo la Serikali. Je, Serikali itakuwa tayari kuheshimu maamuzi ya Baraza la Madiwani kwa maoni na mapendekezo ya Wananchi wanaoishi katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kusema kweli ni kupata suluhisho ambalo ni *acceptable* kwa pande zote mbili. Kwa hakika tunakusudia kuzingatia mapendekezo ya madiwani. Hata hivyo, nitoe tu angalizo moja kwamba, katika kuititia upya maeneo ya mipaka, kuna maeneo ambayo yanaonekana ni ya muhimu kwa upande wa hifadhi kwa maana ya vyanzo vya maji au mambo ya namna hiyo, lakini vilevile kuna maeneo ambayo yanakuwa muhimu sana kwa upande wa Wananchi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, tukikaa pamoja tukaainisha maeneo kwa utaratibu huo, tutaweza kufikia mwafaka, lakini hakika tutazingatia mapendekezo yao.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha tena tumekopa muda usiokuwa wetu, tulikuwa tumalize na dakika 35 lakini tumezidisha. Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mwongozo wa Spika.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kupata Mwongozo wako, endapo Mbunge anauliza swali la Wilaya au Jimbo lake na Waziri anajibu swali hilo kutoka Jimbo au Wilaya nyingine; naomba nipate mwongozo wako endapo Serikali haipo makini kiasi hiki.

**SPIKA:** Ukweli ni kwamba, Waziri alipokuwa anajibu alitakiwa aeleze alikosea Wilaya ile ama ilikuwa ni kitu kingine, alitakiwa afanye hivyo. Sasa nitamwagiza Mheshimiwa Waziri akaangalie yale majibu ni ya hiyo Wilaya yako au ni ya hii Wilaya aliyoisoma; kama ni Wilaya nyingine basi itabidi atueleze hapa. Ila kufuatana na hiyo nilikuwa nimemwambia Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba; ni kipindi cha maswali nitampa muda unaostahili.

Waheshimiwa Wabunge, kama Waziri amejibu maswali yako na wewe hujaridhika, kuna njia tatu; moja ni kutumia kifungu cha 50(1) ambapo hapo utatakiwa wewe uandike maelezo umpe Spika kwa muda halafu utapata muda wa kuweza kujieleza.

Pia unaweza kutumia kifungu cha 28(8); utaniarifu mimi ninapoahirisha kikao jioni ninaacha muda ili wewe ujieleze. Unaweza kujieleza kwa sababu hiyo au jambo lingine lolote kwamba, labda Waziri alipojibu pale mimi sikuridhika na masuala kama hayo.

Kwa nafasi ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ameisema sasa, ye ye amesema Waziri kasema uongo, kwa hiyo, ninamwomba atumie kifungu cha 63(6) ambapo ataeleza maelezo yake hayo kuthibitisha uongo ulikuwa wa nini. Sasa mimi ninampa muda kwa sababu tupo hapa hapa kama akiwa tayari, Ijumaa anaweza kutuletea maelezo tuweze kuangalia.

Waheshimiwa Wabunge, naomba hili niliangalize kwa mara ya pili kwa sababu mara ya mwisho tulipokuwa kwenye Bunge la mwisho niliagiza hivyo hivyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 63, Mbunge anasema mwezie kasema uongo, Spika hawezi akakaa hapa akasema nani kasema uongo. Kwa mujibu wa Kanuni unampa nafasi anaandika vizuri anawasilisha na huyo mwingine anapewa na mimi nina vyombo vyangu ambavyo vinanisaidia kuona kwamba nani kati ya hawa alisema isivyo sahihi. Kwa hiyo, nitakaporudi hapa ndiyo tutatoa maelezo hayo. Kwa hiyo, hata suala la Mheshimiwa Godbless Lema, nitalitolea maelezo katika kipindi hiki. Huo ni utaratibu ambao uko kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Ninaomba Wananchi waelewe hivyo, maana yake walifika mahali wakasema hiyo siyo haki, hapa hatuwezi kuanza kutupiana maneno, hakuna Bunge la namna hiyo, hili ndiyo Bunge tunalofuata. Kama mtu mwingine yeyote hakuelewa vizuri ni kwamba, hatuwezi kutumia ule muda wa saa moja wa maswali tuenze kubishana hapa; haiwezekani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kifungu cha 50(1) unaweza kukitumia; kifungu cha 28 unaweza kukitumia; kwa mfano, Mheshimiwa Tundu Lissu alivyosema, ye ye ameeleza hapa kwamba, hajaridhika na maneno hayo kwa sababu kuna mtu amesema uongo. Kwa hiyo, mwenye nafasi ya kujibu ili kuthibitisha uongo ni ye ye mwenyewe kwa mujibu wa kifungu cha 63(6). Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Tundu Lissu, uweze kuthibitisha hilo na tutaweza kuliangalia wakati ukileta.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusu Kanuni ya 63(3) inayosema: “Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka “kuhusu utaratibu” na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliye kuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uwongo kuhusu jambo au suala alililokuwa analisema Bungeni.”

Na fasili ya (4) inasema: “Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa ana wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.”

Mheshimiwa Spika, ninaoomba mwongozo ...

**SPIKA:** Endeleo kusoma mpaka ile ya mwisho.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Fasili ya (5) inasema: “Bila kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yejote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.”

Fasili ya (6): “Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyyoyatoa Bungeni, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, papo hapo au katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo.”

Mheshimiwa Spika, sasa hii fasili ya (6) inahusu huyo aliyetuhumiwa kuwa amesema uongo. Huyo anayetuhumu kuwa uongo umesemwa, anatakiwa atoe maelezo chini ya fasili ya (4) na maelezo yanatolewa Bungeni na huyo anayedai kwamba Mbunge amesema uongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaoomba mwongozo wako kama sikutakiwa kuthibitisha uongo wa kauli ya Waziri humu humu Bungeni.

**SPIKA:** Nakushukuru umesoma yote kama inavyostahili. Waheshimiwa Wabunge, hizi Kanuni zimeundwa kwa ajili ya mwenendo mzuri wa kuendesha Bunge hili. Kifungu cha 63(3) kinasema, mtu anaweza kusimama pale akasema aliyesema hajasema kweli. Kifungu cha (4) kinasema, Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge. Kwa hiyo, wewe kama ulivyosema unatumia kifungu cha (4).

Kifungu cha (5), Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ningemruhusu angesimama akasema ninaoomba uthibitisho, yeye ndiye angesema ninaoomba uthibitisho kutoka kwako. Sasa unaona hapa tuko katika kipindi cha maswali, muda ni mfupi sana wewe umesema na wewe unaambiwa ni lazima uthibitishe bila kubabaika. Yule aliyedaiwa naye anakwamba thibitisha, unaona hiyo. Sasa tukifikia hapo, itakuwa ni malumbano, ndiyo maana kifungu cha (6) kinasema, unaweza kuthibitisha papo hapo ama Spika atakupa muda utamwandikia Spika, yeye atatumia utaratibu wake wa namna ya kuwaunganisha ninyi wawili kusudi ukweli ujulikane. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa mvisome vizuri hivi vifungu, vililetwa kwa makusudi maana anayesema mtu mwingine mwongo ni lazima yule anayeambiwa mwongo amwambie thibitisha. Sasa tukifanya hivyo wakati wa kipindi cha maswali, kweli tutafika? Ndiyo utaratibu wa kifungu cha (6) unakutaka ufanye hivyo na mimi nimekwambia Siku ya Ijumaa ukiwa tayari tutaweza kujua. Utanipa na mimi nitatumia vyombo vyangu na ninyi wote mnaweza kukutanishwa katika Kamati nyingine ya Maadili kueleza ni nani kasema uwongo na mimi ndiye nitatoa maamuzi hapa. Huo ndiyo utaratibu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo; kwanza, nina tangazo la Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi. Yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao leo hii saa saba mchana katika Ukumbi Na. 227.

Mheshimiwa Pindi Chana, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na mkutano leo hii. Wao ni saa tano katika Ukumbi Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa LAAC kwamba, leo kutakuwa na kikao saa tano katika Ukumbi wa Msekwa B, kwa ajili ya kuridhia taarifa za Kamati.

Halafu nimepewa tangazo lingine kwa maandishi, matangazo haya inabidi muyachapishe kwa sababu ni *documents* za siri zetu. Huyu ni Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, yeye anaomba niwatangazie Wabunge wa CCM wa Wilaya ya Magharibi Zanzibar, wakutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa mtagongana tena, mtapanga huko huko.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo tunaendelea na shughuli zinazofuata.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

### **Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Mabadiliko ya Katiba ya Nchi wa Mwaka 2011 (*The Constitutional Review Bill, 2011*)**

(*Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni  
kwa Mara ya Kwanza*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada umeletwa chini ya Hati ya Dharura na kwa hiyo basi, tunaupeleka sasa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. Wao itabidi wafanye *public hearing*, yaani kuwaalika Wadau mbalimbali waweze kuusikiliza Muswada huu kwa siku kama tatu kuanzia tarehe 7 mpaka tarehe 9. Tumeona kwamba,

Muswada huu unapendwa na watu wengi, tukisema tufanyie *public hearing* hapa Dodoma peke yake, wale wengine walioko Dar es Salaam ambako pia kuna ofisi yetu, watakosa uwezo au usafiri au gharama za kuja huku. Kwa hiyo basi, tunafungua vituo viwili; kimoja kitakuwa hapa Dodoma katika Ukumbi wa Msekwa na kingine kitakuwa Karimjee, Dar es Salaam.

Madhumuni ya Muswada huu siyo kujadili mabadiliko ya Katiba. Ninaomba Wananchi waelewe, kwa sababu naona watu wameupotosha kwamba ni kujadili Maudhui ya Kitaba; sivyo. Muswada huu unataka kuangalia ni namna gani tutaingia katika zoezi hilo. Naona Wananchi wanadhani kwamba, tunajadili Muswada, siyo hivyo bali ni namna gani tutaingia katika zoezi hilo. Kwa hiyo, tumetoa muda mrefu sana ili Wananchi waweze kutoa maoni yao na waende kwenye madhumuni ya Muswada na siyo kitu kingine.

Kwa hiyo, Wananchi wanakaribishwa Dar es Salaam tarehe 7 na Dodoma kwa wale wanaozunguka Dodoma tarehe 7 hiyo hiyo. Nimesikia mazungumzo asubuhi kwamba, kwa nini tusiende na mikoa mingine? Sisi hiso ndiyo *centres* za kufanya kazi. Kwa hiyo, tunapenda Wananchi waseme na watoe maoni yao kwa uwazi kabisa, bila hofu yoyote, halafu Wabunge watakuja hapa kufikiria yale maoni waliyotoa Wananchi. Ule Muswada ni mapendekezo ya Serikali, siyo Sheria; kwa hiyo, unaweza ukaandikwa upya na mimi nimekaa katika Bunge najua mahali ambapo Muswada uliandikwa upya. Ninaomba watu wawe huru, kikubwa watu tuaminiane, kama unaona kuna kitu unakitaka kieleze mle ndani, sisi hatuna tatizo; wewe ieleze Kamati itasikiliza chochote mtakachokisema. Kwa hiyo, wadau wanakaribishwa Dar es Salaam na hapa Dodoma.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, kuhusu maneno yangu?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo kuhusu maneno yako ambayo yametufurahisha sana, lakini kuna tatizo dogo tu kwamba, umeagiza hii Kamati ya Katiba na Sheria kusikiliza wadau hapa Dodoma na Dar es Salaam; lakini kwa kweli hili suala ni la nchi nzima na Muungano, Zanzibar tuna Ofisi ya Bunge ambayo haijafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Kamati hii ya Katiba na Sheria, kikundi kimoja kisiende Ofisi ya Bunge Zanzibar wakasikiliza maoni ya wadau nako ili kukamilisha Jamhuri nzima ya Muungano mbali ya Mikoa? (*Makofî*)

**SPIKA:** Hilo limefikiriwa na Kamati imeshawaandikia Zanzibar watafika kwenye Kituo cha Dar es Salaam.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na kwamba, umetoa hivyo vituo viwili nya kujadili huu Muswada, lakini Muswada huu asilimia kubwa ya Watanzania hawajui Kiingereza na unasema unataka utoe fursa kwa Wananchi wengi kuujadili. Huoni kwamba tunawanyima haki Watanzania wengi kuujadili Muswada huu ambao umeandikwa kwa Lughya ya Kiingereza ambacho Watanzania wengi hawakifahamu? (*Makofî*)

**SPIKA:** Serikali mnataka kujibu; AG?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa kutumia lugha ambayo Wananchi wa Tanzania wanaifahamu, wanaizungumza na wanailewa. Tunafahamu na kwa ajili hiyo, ndiyo maana Katiba yetu imeandikwa kwa Kiswahili na Katiba yoyote utakayoiona imeandikwa katika lugha nyine, ujue kwamba, inayotambulika ni ile ambayo ni ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili umefafanua vizuri kwamba, tunachotegemea hapa ni mchakato wa kwanza kabisa wa kufikia mabadiliko ya Katiba ambayo itaandikwa kwa Kiswahili na hatukufanya tafsiri ya Muswada huu kwa Lughya ya Kiswahili. Tunafahamu kwamba, huo ni upungufu lakini kwa sababu tunakwenda kwa Wananchi na kutakuwa na watu wanaotoa tafsiri kama mlivyoona kwenye Kongamano la *University of Dar es Salaam (UDASA)* kwamba, wale wanazungumza Kiingereza lakini walikuwa wanauchambua Muswada kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo yatafanyika kwenye hizi Kamati na sidhani kwa nadharia ni kikwazo lakini sidhani kama litakwamisha Watanzania kufahamu tunachokusudia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kufuata maelezo ya awali ambayo umeyatoa kwamba, Muswada umesomwa kwa mara ya kwanza na tutausoma kwa hatua zake tatu ndani ya Bunge hili; ni kweli kabisa kwamba, Muswada huu unaweka mchakato kwa ajili ya kuja kufikia kuandika Katiba. Vilevile ni ukweli ulio dhahiri kwamba, mchakato usipokuwa unajenga Mwafaka wa Kitaifa, kwa vyovyote vile Katiba haitakuwa inajenga Mwafaka wa Kitaifa.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo kwanza wamepata Muswada na unataka tuupitishe kwenye Mkutano huu. Wabunge hatujakwenda majimboni kwetu kupata *opinion* ya wapiga kura wetu, namna gani ambavyo Muswada huu utajadiliwa.

Mheshimiwa Spika, huoni kwamba ni busara kuishauri Serikali *to extend debate* ya Muswada huu na Mheshimiwa Rais aombwe aiondoe Hati ya Dharura ili Wabunge tupate fursa ya kwenda Majimboni kushauriana na Wananchi wetu ili baadae tuje kuandika Muswada ambao una *consensus* ya Kitaifa?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwongozo wangu ni kwamba, Mheshimiwa Zitto ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi. Kama kuna mtu aliyeanzisha kwamb, huu Muswada uje kwa *Certificate of Urgency* ni Mheshimiwa Zitto. Sababu zilizotolewa ilikuwa kwamba, tusipoanza mchakato huu tukifika bajeti fedha hazijaandalila kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kubajeti hapa, tutashindwa kuendesha mazungumzo haya anayoyasema Mheshimiwa Zitto kwamba, kwa ada ya Muswada huu ndiyo mtakwenda Wabunge mpaka vijijini na mtakaa na watu wenu na mtazungumza. Hii ni hatua ya kufunga mlango. (*Makof*)

Sasa naona *contradiction*, basi tunaendelea na Hoja za Serikali. Mwongozo wa Spika, sasa unatosha. Mheshimiwa Msigwa, huwezi kupewa nafasi kwa sababu umeshapewa nafasi ya kutoa mwongozo na huwezi kuzungumzia miongozo kumi kwa wakati mmoja. Eeh Mheshimiwa.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi natoa msisitizo mmoja kuhusu kauli ya Mheshimiwa Mnyaa kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imejengeka kwa nchi mbili; Zanzibar na Tanzania Bara. Huu ni mchakato wa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kauli yako ya mwanzo uliyoitoa hapa kwamba, imekuwa ni vigumu kufanya Dodoma peke yake, ufanyiwe na Dar es Salaam kwa sababu ya kuogopa gharama na watu kujikimu watakapokuwa hapa Dodoma. Baadae ukatoa kauli kwamba, Zanzibar wamearifiwa waje Dar es Salaam. Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano na hii ni *public hearing* kule hawatatumwa Wajumbe wa Serikali peke yake, kuna Wananchi wanataka kusikia na kuchangia. Kama utaona gharama kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma ni kubwa, zinakuwa ni mara mbili kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam na nani atazisimamia gharama hizo ili tuwatayarische hao watu katika Majimbo yetu waje wasikilize?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimetangaza hapa kwamba, Kamati ya Katiba na Sheria, itakaa baada ya kikao hiki na hizi Kamati zetu Wabunge mnaweza kuhudhuria. Sasa kuna mwingine alifika pale akaanza kuchukua *documents* nyeti za wenzao akaondoka nazo, hurusiwi wewe unakwenda kusikiliza wenye Kamati ndiyo wana

madaraka ya kuwa na nyaraka zao. Kwa hili suala tuliloliangalia sisi tulifikiria kwamba, tuweke centre Dar es Salaam *in the Eastern Zone* hapa tuweze kushughulikia maeneo haya huku. Ninaposema kule Zanzibar kufuatana na Mwenyekiti wa Kamati amewaalika watu wanakuja kutoka Zanzibar, Waheshimiwa Wabunge, tusiendelee kujadili hapa kama nilivyosema, huu Ukumbi ni mkubwa sana, hatuwezi kuendelea kujadiliana hapa mpaka tukafika. Sasa napenda tuendelee na mengine yanayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### M A A Z I M I O

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa UNESCO wa Kulindwa  
kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika wa 2003**  
*(Convention for the Safeguarding of the Intangible  
Cultural Heritage, 2003)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) wa Kulindwa kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika wa 2003 (*Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage, 2003*).

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie fursa hii, kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika, Naibu Spika Job Ndugai na Wenyeviti wa Kamati. Kipekee, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa kwao katika Uchaguzi Mkuu wa Novemba 2010, ambao ulikuwa mgumu, huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa maelekezo na michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili wakati wa vikao vilivyofanyika baina ya Kamati na Wizara yangu, kati ya tarehe 22 na 28 Machi 2011. Napenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba, michango yao tunaithamini na pia tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu mapendekezo ya kuridhia Mkataba uliokusudiwa, ambao ninaliomba Bunge lako liweze kuridhia.

Mheshimiwa Spika, usuli wa Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 2003 wa Kulindwa kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika (*Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage, 2003*) ni Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 1972 wa Kuhifadhi Urithi wa Kiutamaduni wa Asili wa Ulimwengu (*Convention for the Protection of the World Cultural and Natural Heritage*).

Mkataba huo ambao Tanzania imeshauridhia na hivyo kuwa mshirika wake, unahuksika na urithi wa kiutamaduni unaoonekana kwa macho na kushikika kama vile

majengo na makazi ya zamani na pia urithi wa asili kama vile mabonde, milima na mbuga za uoto na wanyama. Tanzania inayo maeneo saba yanayotambuliwa Kimataifa na kulindwa chini ya Mkataba huu, yaani:-

1. Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.
2. Mji Mkongwe wa Zanzibar.
3. Michoro ya Mapango ya Kondoa (*Kondoa Rock Art Sites*).
4. Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.
5. Hifadhi ya Serengeti.
6. Hifadhi ya Kilimanjaro; na
7. Hifadhi ya Selous.

Mheshimiwa Spika, japo Mkataba huu wa Mwaka 1972 ulihuisha maeneo muhimu sana ya urithi wa kiutamaduni, ilibainika kuwa, haukugusa kabisa urithi wa kiutamaduni usioshikika, ambao Tanzania inao kwa wingi. Urithi usioshikika ni ule unaorithishwa kwa mapokeo ya kusimuliana kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hujumuisha utambaji wa hadithi; vitendawili; sanaa za maonesho kama vile michezo ya kuigiza, ngonjera, uimbaji wa mashairi na tenzi, majigambo na kadhalika; lugha; matambiko; ujuzi; na ufundi wa jadi kama vile uganga wa jadi.

Mkataba huu wa Mwaka 2003 umedhamiriwa kuutambua urithi wa kiutamaduni usioshikika na kuweka taratibu za kuulinda kwa kuwa ni sehemu muhimu ya utamaduni wa ulimwengu. Mkataba huu una jumla ya ibara (*Articles*) 40. Napenda kuchukua fursa hii, kuelezea vipengele vichache muhimu zaidi vya Mkataba huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ibara ya kwanza ya Mkataba huu inaelezea madhumuni yake ambayo ni pamoja na:-

- (i) Kulinda urithi wa kiutamaduni usioshikika.
- (ii) Kuhakikisha urithi huo unaheshimiwa.
- (iii) Kuinua utambuzi wa urithi huo mionganoni mwa jamii husika, kitaifa na kimataifa.
- (iv) Kutoa fursa ya kushirikiana na kusaidiana kimataifa katika kulinda urithi wa kiutamaduni usioshikika.

Kila nchi mshirika wa Mkataba huu, haina budi kuweka taratibu na kanuni za kulinda na kuendeleza urithi wa kiutamaduni usioshikika, ikiwa ni pamoja na kutengeneza orodha ya urithi wa kiutamaduni usioshikika uliomo ndani ya mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, ibara ya pili inahusu fasili au ufanuzi wa Urithi wa Utamaduni Usioshikika. Urithi wa Utamaduni Usioshikika ni mapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Urithi huo siku zote huundwa na jamii, makundi na wakati mwingine, mtu mmoja mmoja kwa mujibu wa mazingira na historia inayotoa hamasa ya kuwa na utambulisho na kuwa endelevu. Jamii hazina budi kuhamasishwa juu ya umuhimu wa urithi wa kiutamaduni usioshikika kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ibara za nne na tano za Mkataba huu zinahusu vyombo vya maamuzi. Mkataba huu una vyombo viwili vikuu vya maamuzi, yaani:-

- (i) Mkutano Mkuu wa Wanachama wote, ambacho ndicho chombo cha juu zaidi.
- (ii) Kamati ya Utendaji yenye Wajumbe 18 ambao watachaguliwa kutoka mionganini mwa Wawakilishi wa Nchi Wanachama. Wajumbe wa Kamati wataongezeka kufikia 24 pindi nchi Wanachama wa Mkataba zitakapofikia 50.

Taratibu za uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji pamoja na majukumu ya Kamati hiyo zimefafanuliwa katika ibara ya (6) na (7).

Mheshimiwa Spika, ibara za 19 – 24 zinahusu ushirikiano wa Kimataifa. Mkataba huu unahimiza Nchi Wanachama kushirikiana, kusaidiana na kujalizana uzoefu katika harakati zote za kulinda na kuhifadhi urithi wa kiutamaduni usioshikika. Mashirikiano yanaweza yakahusu: Ubadilishanaji wa mbinu za kutunza urithi huo; upatikanaji wa wataalam; utoaji wa mafunzo kwa watumishi; ujengaji wa miundombinu; utoaji wa vitendea kazi na ujuzi wa kuvitumia; na utoaji wa aina nyingine ya misaada ya kifedha na kiufundi.

Mheshimiwa Spika, ibara za 25 - 28 zinahusu Mfuko Maalum. Mkataba huu unaunda Mfuko wa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika (*Intangible Cultural Heritage Fund*), kwa ajili ya kusaidia umuhimu wa majukumu yaliyoainishwa katika Mkataba wenyewe. Nchi washiriki wa Mkataba huu, zinaweza kuomba msaada kutoka katika Mfuko utakaoundwa. Taratibu zimewekwa bayana katika Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu pia umezungumzia masuala mengine ya msingi yatakayoweza kufanikisha utekelezaji wake. Masuala hayo yanahusu Haki za Binadamu, uhusiano na Mikataba mingine, umuhimu wa kuijunga na Mkataba, Matokeo ya kuijunga na Mkataba, utaratibu wa kuijunga na Mkataba, gharama za kuijunga na Mkataba, Mawasiliano na Wadau na Maoni yao kuhusu Mkataba na namna ya utekelezaji wa Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Haki za Binadamu, Mkataba huu unasisitiza haki ya kila jamii kufurahia utamaduni wake pasipo kubaguliwa au kuzuiliwa. Mradi kwa kufanya hivyo, jamii haikiuki Haki za Binadamu. Kwa mfano, mila zinazonyanyasa watu wa jinsia fulani au kutesa watu wa umri fulani, haziwezi kutetewa eti kwa kuwa ni sehemu ya utamaduni wa jamii maana mila hizo zinakiuka Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhusiano na Mikataba mingine, Mkataba huu hauathiri uhalali wala umuhimu wa Mkataba wa Kuhifadhi Urithi wa Kiutamaduni na wa Asili wa Ulimwengu wa Mwaka 1972. Tanzania tayari ni mshirika wa Mkataba huo na haina budi kuendelea kuutekeleza kwa kuwa malengo yake yanajitegemea.

Mheshimiwa Spika, maelezo juu ya umuhimu wa kujiunga pia yametolewa. Kwa mujibu wa Ibara ya 32 ya Mkataba huu, kila Nchi Mwanachama wa UNESCO anahitajika kuridhia Mkataba huu. Tanzania ni Mwanachama wa UNESCO na ilishiriki katika mikutano kadhaa iliyoandaa na kupitisha Mkataba huu; kwa hiyo, haina budi kuridhia kama ilivyokuwa wajibu wa wanachama wote. Mkataba huu ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa unalenga kuzisaidia Nchi Wanachama kulinda tamaduni zake na kunufaika na tamaduni hizo pasipo kukiuka Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya kujiunga na Mkataba huu ni kwamba, kutaiwezesha Tanzania kutumia fursa zifuatazo:-

- Kushirikiana na nchi nyininge duniani kulinda utamaduni wake na wa nchi nyininge kwa uwazi pasipo shinikizo la kisiasa au kiuchumi. Kwa mfano, Tanzania inaweza kutumia vipengele vya Mkataba huu kuamua ni asilimia ngapi za matangazo yote ya redio na televisheni yawe ni ya Kitanzania (muziki, filamu, lugha na kadhalika) ili kulinda utambulisho wake. Hatua za namna hii ni muhimu katika kuendeleza utamaduni wa taifa pasipo kufunga kabisa milango kwa tamaduni za nchi nyininge.
- Kupata fursa ya kuchagua na kuchaguliwa kuongoza vyombo vya Kimataifa vinavyoundwa na Mkataba huu, hususan Kamati ya Utendaji na Mfuko wa Fedha uliopo.
- Sheria za nchi kama vile Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki zitapata msukumo wa Kimataifa kuitabu na mwaka 2003.
- Kunufaika na utaalamu na fedha zinazopatikana chini ya Mkataba huu, hasa Mfuko wa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika (*Intangible Cultural Heritage Fund*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kujiunga na Mkataba, Ibara ya 32 ya Mkataba huu, inazitaka nchi zinazotaka kujiunga zifanye hivyo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Katiba yenyewe. Kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndilo lenye madaraka ya kujadili na kuridhia Mikataba ya Kimataifa kama huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na gharama za kujiunga na Mkataba huu; ziko za aina tatu. Kwanza, ni ile michango ya kila mwaka ambayo ni kiasi kisichozidi asilimia moja ya mchango wa kila mwaka kwa UNESCO. Kiasi hiki ni sawa na Dola za Marekani mia moja na themanini na tatu. Pili, ni gharama za utekelezaji wa Mkataba ambazo zitakuwa ni sehemu ya bajeti za Idara na Mashirika ya Serikali yatakayokuwa yameainishwa kutekeleza Mkataba huu. Aina ya tatu ya gharama ni michango ya hiari ambayo inaweza kulipwa na Tanzania kwa Mfuko ulioanzishwa na Mkataba endapo uwezo utaruhusu. Utekelezaji unaweza kuanza kwa kutumia Bajeti ya sasa ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano na Wadau na maoni yao juu ya Mkataba huu, Wizara yangu ikiwa katika mchakato wa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekero la kuridhia Mkataba huu, iliwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni na ushauri wao. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano

wa Kimataifa, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Maliasili na Utalii (Idara za Mambo ya Kale na Makumbusho ya Taifa), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Kanda ya UNESCO – Dar es Salaam.

Wadau wengine ni Tume ya Taifa ya UNESCO, Vyuo vikuu, Asasi za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), pamoja na wasanii binafsi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maoni ya wadau hawa, Mkataba huu ni muhimu sana kwa Tanzania, kutokana na utajiri mwingi wa urithi usioshikika ilionao na ambao unahitaji kutambuliwa rasmi Kitaifa na Kimataifa na pia kulindwa ipasavyo.

Ninaomba nielezee kipengele cha mwisho kinachohusu utekelezaji wa Mkataba wenyewe. Mkataba huu ulianza kutumika tarehe 20 Aprili, 2006 na kufikia tarehe 15 Machi, 2011 jumla ya nchi 134 zilikwishajiunga, zikiwemo 35 za Bara la Afrika. Mionganini mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi sasa (2011) ni Rwanda na Tanzania tu ndizo hazijaridhia Mkataba huu. Tanzania itakuwa mshirika wa Mkataba huu miezi mitatu baada ya kuwasilisha Hati za Kuridhiwa kwa Mkataba kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hata hivyo, utekelezaji Kitaifa utaanza mara tu baada ya Mkataba kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, marekebisho ya Mikataba ya Kimataifa ya aina hii yanapaswa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Uamaduni (UNESCO);

NA KWA KUWA Mwaka 2003 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba unaohusu Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni Usioshikika. Utamaduni usioshikika hujumuisha simulizi na mapokeo yake, sanaa za maonesho, lugha, matambiko na sherehe, ujuzi na ufundi wa jadi, ambavyo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine;

NA KWA KUWA lengo na madhumuni ya Mkataba huu ni kuutambua urithi huu kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuweka taratibu za kuulinda kwa kuwa ni sehemu muhimu ya utamaduni ulimwenguni;

NA KWA KUWA Mkataba huu unazingatia kila Nchi Mwanachama kuweka utaratibu na kanuni za kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni usioshikika, ikiwa ni pamoja na kutayarisha orodha ya urithi wa utamaduni husika uliomo ndani ya mipaka yake;

NA KWA KUWA Mkataba huu unaunda Mfuko wa Fedha kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa na Mkataba wenyewe. Kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itafaidika kama ifuatavyo:-

- (a) Kuomba msaada kutoka katika Mfuko ulioanzishwa na Mkataba huu;
- (b) Kushirikiana na nchi nyingine duniani kulinda utamaduni wake na wa nchi nyingine kwa uwazi pasipo shinikizo la kisiasa wala uchumi;
- (c) Kupata fursa ya kuchagua na kuchaguliwa kuongoza vyombo vyaa Kimataifa vinavyoundwa na Mkataba huu;
- (d) Sheria za Nchi kama vile Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki zitapata msukumo wa Kimataifa; na
- (e) Kunufaika na utamaduni, utaalamu na fedha zinazopatikana chini ya Mkataba huu hasa Mfuko wa Urithi wa Utamaduni Usioshikika (*Intangible Cultural Heritage Fund*).

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutohata na kuwepo kwa Mkataba huu, Bunge hili katika mkuhato wake wa tatu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia Kuridhia Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuhusu Kuhifadhi Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa Mwaka, 2003, yaani *The Convention for Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa, sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 114(15), naomba sasa niwasilishe mbele yako, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuhusu Uhifadhi, Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa Mwaka 2003 (*The Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage, 2003*).

Awali ya yote, Kamati yangu inapenda kutoa salamu za pole kwa Wananchi walioathirika na kupoteza ndugu zao katika majanga mbalimbali yaliyotokea mwanzoni mwa mwaka huu. Majanga hayo ni pamoja na milipuko ya mabomu Gongo la Mboto,

ajali ya basi iliyohusisha Wasanii wa Bendi ya *Five Stars* na ajali zingine mbalimbali zilizopoteza maisha ya Watanzania. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. (*Amina*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilipata maelekezo kutoka katika Ofisi yako ya kushughulikia Azimio hilo. Kwa wakati huo Kamati yangu ilipata maelezo fasaha kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) Kuhusu kuhifadhi Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa Mwaka 2003 (*Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage*), uliowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, tarehe 25 Machi, 2011 na 28 Machi, 2011 katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1972, nchi yetu iliridhia Mkataba wa UNESCO wa Kuhifadhi Urithi wa Kiutamaduni na Asili wa Ulimwengu (*Convention for the Protection of the World Cultural and Natural Heritage*). Mkataba huu unajumuisha utamaduni unaonekana kwa macho na kushikika kama vile majengo, makazi ya zamani, milima, mabonde, mbuga za uoto na wanyama na mambo mengine ya kiasilia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, Mkataba huu wa Mwaka 1972 ulihusisha maeneo muhimu ya urithi wa kiutamaduni, ilibainika kuwa, haukugusa kabisa urithi wa kiutamaduni usioshikika kama hadithi, vitendawili, sanaa za maonesho, uimbaji wa mashairi, tenzi, majigambo, michezo na matambiko, lugha, ujuzi na ufundi wa jadi.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2003, UNESCO ilikutanisha Nchi Wanachama na kuridhia Mkataba huu mpya wa utamaduni usioshikika. Katika kuridhia Mkataba huo, nchi nyingi tayari zimesharidhia Mikataba hiyo ndani ya nchi zao na kujiunga na kufanya utekelezaji wa Mkataba huo. Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Nchi za Tanzania na Rwanda ndizo ambazo mpaka leo tunaporidhia Mkataba huu ndani ya Bunge, zilikuwa hazijafanya hivyo. Kila Nchi Wananchama wa UNESCO ikiwemo Tanzania, inahitajika kuridhia Mkataba huu ili kulinda tamaduni zetu na hasa tamaduni hizo ambazo hazishikiki kwa kuzinufaisha na kuziweka zikifanya kazi bila kukiuka haki za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Azimio hili yalivyoletwa mbele ya Kamati yangu ilikuwa kama ifuatavyo: Kulinda urithi wa kiutamaduni usioshikia ndani ya nchi yetu; kuhakikisha urithi huo unaheshimiwa; kuinua utambuzi wa urithi huo mionganoni mwa Jamii husika Kitaifa na Kimataifa; na kutoa fursa ya kushirikiana na kufaidiana kimataifa katika kulinda urithi wa kiutamaduni usioshikika.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kuweza kuwasilisha Azimio hili lenye lengo la kuboresha, kulinda na kuhakikisha kuwa, tunakuwa na ushirikiano na nchi nyingine duniani katika kulinda utamaduni wetu na Wananchi wetu hasa kwa kushirikiana na nchi nyingine kwa uwazi, pasipo shinikizo la kisiasa iwe ni ndani ya nchi ama ni nje ya nchi, iwe kiutamaduni au hata kiuchumi.

Mheshimwa Spika, Azimio hili la Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa UNESCO wa Kulindwa kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika wa Mwaka 2003, ni la muhimu kwa Nchi yetu ya Tanzania kwani litasaidia kuwepo utambulisho halisi wa Mtanzania, kwani utahimiza mambo ambayo ni Utamaduni wetu na mambo mengi ambayo ni mazuri tangu zamani na yanapaswa kuendelezwa; mfano, ziko hadithi, tenzi, ngnjera majigambo na lugha zilizokuwa zikitumika kuhamasisha shughuli mbalimbali za kimaendeleo hapo awali na kuwa yamesahaulika sana kwa sasa. Kwa kuridhia Mkataba huu, nchi yetu itapata nafasi ya kuyakumbuka na kuyahifadhi na kuyatumia mambo hayo kwa faida na manufaa ya nchi yetu kwa ujumla. Haya yote yatatakiwa yahifadhiwe siku hadi siku katika Idara na Taasisi mbalimbali; mfano, Makumbusho ya Taifa na Maktaba mbalimbali, lakini kwa muda mrefu tumekosa nafasi za kushiriki katika uhifadhi huu iwe ni ndani ya nchi ama kimataifa. Vilevile tumekosa nafasi ya kupata usoefu wa nchi nyingine zinavyohifadhi tamaduni zao hasa hizo zisizoshikika katika kuzienzi na kuzipa umaarufu zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kufikiria Azimio la Kuridhia Itifaki hii, Kamati imebaini kuwa, kwa muda mrefu wasanii mbalimbali nchini wamekuwa wakilalamikia suala la upatikanaji wa Haki Miliki ambapo zitawafanya wasiweze kuibiwa kazi zao. Kuridhiwa kwa Azimio hili kutasaidia pia Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi na kuhakikisha Sheria hiyo inapewa msukumo iwe ndani ya nchi na hata nje ya nchi, kwa manufaa ya wasanii wetu, lakini vilevile kwa manufaa ya Watanzania wote na kwa kufanya hivyo, tunaamini kabisa kipitia Mkataba huu, basi suala la kupambana na umaskini kwa kutumia dhana ya usanii ndani ya nchi yetu, litakuwa limefikia katika kiwango cha kuridhisha na kuwasaidia Wananchi wetu na Wasanii wetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa Azimio hili itakuwa hatua muhimu kwa Tanzania, kwani nchi yetu ina utajiri mwangi wa urithi usioshikika, ambao unahitaji kutambuliwa rasmi Kitaifa na Kimataifa na kulindwa ipasavyo. Mambo mengi yamekuwa yakijidhihirisha na tumekuwa tukiyaona lakini yamekuwa yakisahaulika. Ziko dalili za nyakati; wakati wa mvua, wakati wa mavuno na kadha wa kadha, hayo yote yanatakiwa kuhifadhiwa kwa ufasha.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Mkataba huu unatekelezwa, Kamati inashauri Serikali kuangalia sheria mbalimbali tulizonazo kwa sasa kama zinaweza kukidhi mawanda ya Mkataba huu na kama zitakuwa zinakinzana, basi Serikali ifanye haraka sana kufanya marekebisho ya Sheria hizo ili Mkataba huu uweze kutekelezeka kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, bado Kamati imegundua ziko changamoto na inashauri kwa Serikali baada ya kuridhia Azimio hili ni vema mambo kadhaa yafanyike. La kwanza, mara baada ya Bunge kuridhia Azimio hili ni vema Serikali kufanya yafuatayo:-

- Kuweka taratibu na Kanuni za kulinda na kuendeleza urithi wa kiutamaduni usioshikika; na

- Kutengeneza orodha ya urithi wa kiutamaduni huo usioshikika uliomo ndani ya nchi yetu ili kuulinda usiweze kuibiwa nje ya mipaka yetu na katika kufanya hivyo, Lugha yetu ya Kiswahili imeona ni utamaduni usioshikika ambao ni wa msingi kabisa na kama Serikali yetu haitakuwa makini, basi lugha hii inaweza ikaibiwa na nchi yoyote ambayo ingeweza kuona umuhimu wa lugha hiyo kama utamaduni katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri kutumia mwanya huu kuhakikisha kwamba, katika suala la kupambana na tatizo la ajira nchini, Kamati zitakazoundwa kusimamia utekelezaji wa Mkataba huu, ofisi zitakazofunguliwa kushughulikia utekelezaji wa Mkataba huu, basi nchi yetu ijipange vizuri ili Watanzania wengi ambao wamekwishakuelimika katika Vyuo Vikuu mbalimbali na wana elimu ya kutosha na wamekosa ajira, basi iwe ni mwanya na nafasi nyingine mojawapo ya kuwasaidia kupata kazi na ajira na maeneo ndani ya nchi na hata nje ya mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu vilevile imeona kwamba, upo utaratibu wa kutambua tamaduni hizi zisizoshikika na kuziweka kama mifano mizuri ya kufuatwa na Nchi Wanachama katika Jumuiya nzima. Tunaiomba sana Serikali yetu itakapopeleka na kutambulisha tamaduni zetu katika nchi hizo, nchi yetu itengeneze utaratibu ambao utafanya tamaduni hizo zibakie kuwa ni mali yetu na zisije zikaibiwa na nchi nyingine katika kigezo hicho cha kuzitambua na kuzipeleka zikatambulika na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia kwa kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kabla Azimio hili halijaridhiwa leo hapa ndani ya Bunge lako Tukufu. Wajumbe hao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Mch. Getrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumper Nshunju Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe, Mheshimiwa Dkt. Seif Selement Rashidi, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Abdallah Haji Ally, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah, kwa kuiwezesha Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake, pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John, kwa kuihudumia Kamati wakati wote tulipokuwa tunapitia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba niwashukuru Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, wakishirikiana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Sethi Kamuhanda na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa Azimio hili, kuliwasilisha mbele ya Kamati na hivyo Kamati kupata muda wa kulijadili na kutoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, vilevile shukrani za pekee ziwaendee wadau mbalimbali walioshiriki kuboresha Azimio hili. Wadau hao ni pamoja na Chuo Kikuu Cha Mzumbe, Makumbusho ya Taifa, *Lawyers Environmental Action Team* na wote walioshiriki kutoa michango yao kwa namna mbalimbali toka mchakato wa ushughulikiaji wa Azimio hili ulipoanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio. (*Makofit*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa UNESCO wa Kulindwa kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika wa Mwaka 2003 (*Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage, 2003*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuongea nikiwa kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara, naomba kuchukua fursa hii, kwanza, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani, kwa imani yake kwangu na kunitfea ili niisimamie Wizara hii. Ahsante sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, aidha, shukrani kwako, kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi hapa Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba nitoe shukrani kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), pamoja na Wanachama wote na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa ujumla, kwa kuniyamini na kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika mchakato mzima wa mimi kuwa hapa Bungeni. Nashukuru kwa kuniwezesha kutengeneza historia ya mimi kuwa msanii wa kwanza wa Bongo Flava kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge hili Tukufu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mimi na wewe tumeingia katika historia kuitia Bunge hili la Kumi kwa mimi kuwa msanii wa kwanza wa Bongo Flava Kuingia Bungeni na wewe kuwa Spika wa kwanza Mwanamke hapa Tanzania; hongera sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kuangalia baadhi ya ibara ambazo Kambi ya Upinzani inaona zinaweza kuwa na upungufu kwa Tanzania. Ibara ya kwanza inayohusu madhumuni ya Mkataba huu; madhumuni yake ni mazuri na

yako wazi tatizo ni kwamba, kwa kuwa Tanzania kama nchi ambayo ina zaidi ya makabila 120 na kila kabile lina utamaduni wake (lughya, mila, majigambo, maigizo, nyimbo na ngomba, matambiko na jadi zake); je ni urithi na utamaduni usioshikika wa kabile lipi utatakiwa kuhifadhiwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashukuru kwa jitihada alizozifanya Mwasisi wa Taifa letu, kukifanya Kiswahili kuwa Lugha ya Taifa ambayo iliwaunganisha Watanzania wote ambao wanatoka katika makabila hayo takriban 120. Ingawa katika kutuunganisha, alizinyima nguvu mila na tamaduni za makabila hayo na hivyo kuifanya Tanzania kutokuwa na Utamaduni wa Taifa, badala yake tuna tamaduni za makabila mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, sasa ni muda mwafaka kwa Serikali kuzitunza na kuzitambua lugha zetu za asili, kwani lugha zetu za asili ndizo zinatufanya sisi kuwa Wahaya, Wasukuma, Wanyakyusa, Wangoni, Wachagga, Waruguru, Wahehe, Wabena, Wagogo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utu wetu ni lugha zetu za asili na ndicho kitambulisho kikubwa cha sisi ni akina nani katika dunia hii. Kambi ya Upinzani inasikitika kwamba, Serikali kwa makusudi kabisa imezuia vyombo vya habari vinavyohamasisha kukua kwa lugha zetu za asili kurusha matangazo kutumia lugha hizo. Hili ni kosa kubwa sana, ambalo kwa sasa tunashukuru Azimio hili litasaidia kuwabadilisha Watendaji wa Serikali kuona umuhimu wa lugha zetu za asili.

Mheshimiwa Spika, wahusika wakuu wa UNESCO ni Ufaransa na Marekani, tunashukuru kwa kufikiria kuwa na haja ya kulinda urithi wetu usioshikika; lakini nchi yetu ni tofauti sana na nchi hizo kwani wao utamaduni wao ni wa nchi nzima kama vile lugha, hawana lugha tofauti zaidi ya Kifaransa na Kiingereza, tofauti ya lugha hizo huko kwao ni jinsi gani wanavyotamka baadhi ya maneno lakini lugha ni ile ile.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inapata tatizo kubwa kuhusiana na urithi huo wa kiutamaduni usioshikika kurithishwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo, kwani wahusika wakuu katika makabila ambao wanahitajika kurithisha utamaduni huo, wamepoteza mwelekeo kutokana na ukweli kuwa, mambo hayo kwa sasa yamepoteza ufuasi ndani ya jamii zetu; mfano, jando na unyago.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kabisa kuwa, kuna baadhi ya watu watapingana na hoja ya unyago kwa madai kwamba, katika baadhi ya makabila watoto wa kike wanafundishwa mambo ya kikubwa na kushawishika kuanza mahusiano kabla ya kufikisha umri unaoruhusiwa kisheria. Kwa sasa ni ukweli ulio wazi kuwa, masuala ya unyago ndiyo mambo yanayoendelea katika sherehe za *kitchen party* ambazo dhana yake ni ya utamaduni wa nje. Kimsingi, Kambi ya Upinzani inasema kuwa, suala la jando na unyago ni zuri ila kitu cha msingi ni kusisitiza kwa makabila yetu kuhusiana na tamaduni hizo na suala liwe ni umri gani hasa unatakiwa kwa mtu kufanyiwa tamaduni hizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisisitiza kuwa, Azimio hili ni zuri na linatakiwa kuungwa mkono kwani linaturudishia hadhi ya utu wetu kwa makabila tunayotoka. Ili kwenda sambamba na Azimio hili, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuruhusu redio na television kutangaza kwa lugha za makabila yetu, jambo la msingi ni kuangalia matangazo hayo yanatolewa vipi na lengo lake ni nini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilipomaliza kutangaza baadhi ya matangazo, wengine walichelewa kuyaleta. Ninaomba tuwe tunawahi ili tusirudi nyuma, kwa sababu kuna kipindi cha kutangaza na kipindi cha shughuli nyingine. Sasa hapa nina tangazo la Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, yeye ni *Captain* wa Timu zetu hapa, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Timu ya Bunge kwa Wanaume na Wanawake zitaanza mazoezi rasmi kesho asubuhi ili kujiandaa na mechii kabambe ambazo maelezo zaidi yatatolewa baadae. Kwa hiyo, mazoezi ya Timu zetu za Wanawake na za Wanaume yanaanza.

Mheshimiwa John Mnyika, yeye ni Katibu wa Wabunge wa Chama cha CHADEMA anasema, niwaarifu Wabunge wa CHADEMA kuhudhuria Kikao cha Kamati yao saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 231; naona kama mmegongana pale, tafuteni namna ya kuwasiliana.

Katika mjadala huu nina wachangiaji mpaka sasa wanne. Tunaanza na Mheshimiwa Kabwe Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Assumper Mshama na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kidogo tu juu ya Azimio hii la *Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage* kama jinsi ambavyo limewasilishwa. Napenda kuunga mkono maelezo ambayo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni ameyazungumza na nadhani Serikali itayazingatia katika utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo nilikuwa napenda kulichangia na kutaka lipewe uzito unaostahili ni la utunzaji wa Lugha za Asili. Lugha zetu za Asili zinapotea, kuna Lugha ambazo zinapotea kabisa kabisa; na katika juhudii tunazofanya kuhakikisha kwamba, tunakuwa ni nchi moja kwa kuimarishe Kiswahili, kwa sababu nacho kinapaswa kuimarishe, tumesahau kabisa ya kwamba, tuna Lugha zaidi ya 130 Vijijini ambazo zinapaswa kutunzwa, kuwekewa maandishi yake, kuwekewa historia yake na kuhakikisha kwamba Lugha hizi hazipotei. Sasa hili Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amelizungumza na nadhani kuna haja ya kuhakikisha kwamba, katika taratibu

zetu zote za kibajeti, tunaweka fungu maalum kwa ajili ya kuwezesha watu wanaofanya tafiti waweze kufanya tafiti zaidi za Lugha za Asili na kuzitunza.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo nilikuwa nadhani labda tuliangalie upya kama Taifa; mwaka 1962, tulifuta Machifu nchi nzima. Ilikuwa ni hatua nzuri katika juhudzi za Taifa dogo limetoka kwenye Ukoloni wa Kiingereza ambalo halikuwa ni Taifa bado, haikuwa ni Dola, katika juhudzi za kujenga ili kuondoa ukabila, kuondoa udini na kadhalika, ilikuwa ni hatua nzuri sana kuwaondoa Machifu. Ninadhani kuna haja ya kuja na Muswada wa Sheria ambaa utaweza kutambua, kwa sababu kuna Makabila tayari Machifu wamerudi. Tumeona jinsi ambavyo Machifu wamekuwa wakisimikwa kwa Wanyamwezi akina Fundikira, tumeona kwa Wahehe baada ya Chifu Adam Sapi Mkwawa kufariki na Chifu wa Wahehe alisimikwa.

Tumeona kule Mbozi kuna Chifu pia na bado Wananchi wanawaheshimu. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna haja ya kuangalia uwezekano katika utekelezaji wa jambo hili, tutunge sheria ili tuwarejeshe hawa *Cultural Leaders* kwa ajili ya kutunza tamaduni zetu kule chini, kwa sababu Serikali peke yake haitaweza kuhakikisha kwamb, Wananchi wa Kabilia fulani au wa jamii fulani wanazingatia tamaduni zile na kuweza kuzitunza. Kuna aina za vyakula, kuna aina za nyimbo, kuna majigambo na kadhalika ambayo yanapaswa kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani kama Taifa, tufikirie kwamba, kwa hatua ambayo tumefikia sasa ya kwamba, tayari tuna Taifa, tayari tuna Dola ambayo mimi naamini ni Dola imara kabisa, sasa tuangalie ni namna gani ambavyo tutakwenda kutunza hizi tamaduni zetu kule chini. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria pamoja na maoni mazuri ambayo yametolewa, hoja ya Serikali, hoja ya Kamati ya Bunge kupitia Mwenyekiti wao na hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni; lakini pia tuone namna gani ambavyo tutaweka *Cultural Institutions* kule chini kwenye jamii zetu. Si lazima ziwe zile zile ambazo tulikuwa nazo, lakini kama kuna maeneo ambayo tayari Machifu wale wameanza kutokea ku-*define roles* zao, waweze kuwa na kazi ya kutunza tamaduni. Kwa sababu vinginevyo, Asili ya Taifa hili itapotea. Tunaweza tukafurahi kwamba, tuna Kiswahili kinatuunganisha, lakini tukapoteza mambo ya msingi kabisa ambayo ndiyo yametufanya tuwe Tanzania leo, kwa sababu Tanzania ya leo ni mchanganyiko wa haya makabila yote, ni mchanganyiko wa hizi tamaduni zote, ni mchanganyiko wa vyakula vya aina mbalimbali ambavyo vimekuwa vikifanyika katika maeneo haya. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, katika bajeti inayokuja, tujaribu kuangalia namna gani ambavyo tutaweka fedha za kutosha kwa ajili ya tafiti za kutunza lugha zetu na mambo yetu mbalimbali ya kitamaduni.

Tuanze pia kufikiria kuja na sheria ambayo itaweza kuwarejesha *Cultural and Traditional Leaders* kwa ajili ya kutunza tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Pindi Chana; sijamwona, kwa hiyo Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii, kutoa salamu za rambirambi kwa misiba miwili mikubwa ambayo ilitukumba katika Jimbo la Ubungo, kwa kupotelewa na watu ambao walikuwa na mchango mkubwa kwa Taifa; Dkt. Justine Katunzi, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam pamoja na Mwanahabari Adam Lusekelo. Natumia fursa hii vile vile kutoa salamu za rambirambi kwa kifo kilichotokea jana cha Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli (TRAWU), Bwana Rwegasira. Tuko pamoja na wafiwa katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, naunga mkono moja kwa moja maoni ya Kamati na maoni yaliyotolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio lililo mbele yetu; lakini kuna mambo machache ambayo naomba kuongezea kwa ajili ya kuzingatiwa na Serikali kama sehemu ya utekelezaji wa Azimio hili na Maazimio mengine yatakayokuja.

La kwanza, Hoja ya Serikali inaonesha kwamba, Serikali ilitia saini Azimio hili mwaka 2003 na Azimio hili limeanza kufanya kazi mwaka 2006. Katika kuhitimisha hoja hii, ni muhimu Serikali ikalieleza Bunge lako Tukufu sababu za kuchelewa kuletwa kwenye Bunge hili Azimio hili ambalo Serikali ilitia saini miaka takriban minane iliyopita na limeanza kufanya kazi takriban miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kuchelewa kuridhiwa kwa Azimio hili, kumesababisha hasara ya kifedha kwa Taifa kwa fursa ambazo tungezipata kutoka kwenye huu Mfuko katika kipindi cha miaka yote na faida zote zilizoainishwa hapa katika kipindi chote. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikalieleza Bunge lako Tukufu sababu za kuchelewa kuletwa Bungeni kwa Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, kuna Azimio lingine ambalo ni muhimu sana kama sehemu ya kufanikisha suala hili. Utamaduni huu unahu na unagusa vizazi vilivyopita, vizazi vya sasa, lakini pia vizazi vijavyo. Nchi yetu kuititia kwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, iliweka saini Mkataba mwagine wa Afrika, ambao unagusa vijana (*African Youth Charter Banjul, 2006*), lakini mpaka leo Mkataba ule nao haujaja Bungeni. Mkataba ule una vifungu vinavyohusu masuala ya kiutamaduni na dhima ya vijana kulinda utamaduni katika masuala kama haya. Nitoe wito kwa Serikali kuweza kuharakisha kuletwa kwa Mkataba huu na kuweka utaratibu ambapo viongozi wetu wanaposaini Mikataba kama hii, basi kabla hata ya Mikataba kuletwa kuridhiwa, Bunge liwe linapewa taarifa ili kuweza kufuatalia kwa karibu Mikataba hii kuletwa Bungeni kwa wakati kwa sababu ni kazi ya Bunge kuridhia Mikataba hii kwa mujibu wa Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ni muhimu pamoja na yote yaliyozungumzwa na Kamati kuhusu marekebisho ya Sheria na mazingatio ya kisheria ukaenda sambamba na kuitathmini upya Sera yetu ya Utamaduni kama imizingatia maudhui ya msingi

yaliyoko kwenye Mkataba huu. Jambo hili ni jipya sana kwa Sera yetu kwa ukamilifu wake. Kwa hiyo, ni vizuri kukafanyika mapitio ya Sera ama kuwa na Waraka Maalum utakaotoa mwongozo wa kisera wa utekelezaji wa huu Mkataba ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwenye Azimio lenyewe; ninaunga mkono hoja ya kupitisha Azimio hili. Ningependekeza marekebisho madogo ama nyongeza ndogo kwenye utangulizi wa Azimio, kwenye sehemu inayozungumza Tanzania itafaidika ifuatavyo na Mkataba huu ambao leo tunauridhia; hoja zilizoainishwa kwenye kipengele (a) mpaka (e) zote zina sura ya faida ambazo tutazipata kutoka msukumo wa nje. Vizazi vijavyo vikisoma Azimio hili la Bunge vinaweza kudhani kwamba, Wabunge waliopitisha Azimio hili walikuwa wanatazama zaidi tija za fedha kutoka nje na mambo mengine yanayotokana na Azimio hili kama yalivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwa Bunge lako Tukufu kuwa, kiongezwe kipengele (f) ambacho kitagusa zaidi dhima yetu kama Watanzania katika hoja hii iliyo mbele yetu, kisomeke kwamba; moja ya faida za kupitisha Azimio hili ni kuongeza jitihada za kulinda urithi na utamaduni usioshikika ili ielevweke wazi kwamba, tunalipitisha hili Azimio kama sehemu ya kunufaika kama Taifa kwa *commitment* ya Kimataifa ya kuwezesha haya yaweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami siko mbali na wenzangu waliotangulia. Kwanza, napenda niwape pole wote ambao wamepoteza ndugu zao na tunaamini kabisa Mungu atawatia nguvu waweze kulishinda hilo jaribu. Pia napenda niishukuru Kambi ya Upinzani kwa namna ya pekee, kwa walivyotutia nguvu na kuunga hoja yetu.

Mheshimiwa Spika, labda niongelee jambo moja katika Azimio hili; hapo chini utaona tunesema kuna changamoto; changamoto mojawapo itakayokuja ni kuorodhesha ni nini kiingie katika Azimio hilo. Kwa hiyo, ni sisi wenyewe tutakaochagua kwamba vitu gani viingie. Kwa hiyo, kila kitu ambacho tutataka kiingie katika hilo Azimio ni sisi wenyewe.

Suala lingine lililoongelewa ni la unyago, sana sana tunesema tungependa yaingie mambo mazuri, siyo yale yote ya zamani yaliyo mazuri. Kwa mfano, suala la unyago lilikuwa linafanya watoto wetu waanze mambo yasiyofaa mapema mno. Kwa hiyo, suala hili tunapolipeleka kwenye *Kitchen Party*, ni pale ambapo mtu amebakiza wiki moja kuingia labda katika jambo hilo. Kwa hiyo, inampa nafasi ya kuelewa nini afanye na nini asifanye kabla ya wakati wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ambalo kweli tunaliona na Kamati yetu ililiona vizuri ni kwamba; si kwamba hizi tamaduni zetu zilikuwa hazijahifadhiwa, lakini sasa tunakwenda Kimataifa, yaani tunaongeza nguvu Kimataifa zaidi. Kwa hiyo mimi...

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nimefuatilia mazungumzo ya Mheshimiwa Mbunge, ambaye ametoka kuzungumza ni kana kwamba, anajibu hoja za Wabunge wengine na nafasi ya kujibu hoja ni ya Waziri mwenye Azimio, maana hili Azimio limetoka Serikalini. Sasa nilikuwa naomba nielewe kidogo, anajibu hoja kwa mamlaka gani, maana ni vizuri Mbunge aeleze hoja yake na Waziri atajibu hoja zao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako katika hilo.

**SPIKA:** Huu Ukumbi unapaswa kuwa na *dialogue* inayoongozwa na Spika. Mimi sikuelewa kama anajibu hoja. Kwa hiyo, anaendelea kujadili.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Basi niendelee tu kwa kusema, utamaduni wetu ulikuwa unahifadhiwa, lakini sasa tunakwenda kwa ngazi kubwa zaidi kwamba, utakwenda mbele na kuna namna ya pekee ambayo tulikuwa hatuwezi kutunza Haki Miliki vizuri, lakini kwa kuingia katika Mkataba huu, kwa kukubaliana na UNESCO na nchi zingine, tutaimarisha zaidi namna gani ya kutunza Haki Miliki za kazi za Wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, pia jambo lingine, kuna vipindi ambavyo tunaona kwamba, vilikuwa havifai katika *television*; kwa mfano, Kipindi cha *My Diary*, nadhani kwa ajili ya kutunza utamaduni wetu, tungeomba hicho Kipindi kisiendelee. Kama ushauri wangu tu, kinafundisha mambo ambayo kwa kweli yanatuletea aibu; kama umekaa mezani unasikiliza, msichana wa miaka kumi akiwa *form two* alianza kuwa na *boyfriend* na anachekelea alivyokatishwa tamaa; kwa kweli ningeshauri Wizara husika itusaidie hicho kipindi kisiendelee, kinatuondolea utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ningependa kukushukuru. Kwa namna ya pekee, ninaunga mkono hoja na kuchelewa si tatizo, lakini ni vema kuanza. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati, kwa mchango wao mkubwa wa kuboresha na kutoa maoni kwenye Kamati kuhusu hoja hii ambayo mimi mwenyewe nimewasilisha hapa mbele. Kwa namna ya pekee, nimpongeze sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kitendo chake cha kuelewa na kuunga mkono hoja hii kwa umuhimu wa hoja yenye kwa maslahi ya Watanzania wote. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbilinyi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru sana wachangiaji wengine waliofuata. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa kweli ametambua na amesema maneno ya msingi kabisa katika hoja hii, ambayo Serikali inatakiwa kuyasikiliza. Kwa kushirikiana sisi Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili na Watanzania wote, haya tunayoyasema leo yatakuwa ni mchango mzuri sana kwa Serikali yetu katika kuboresha hoja hii kwa upana wake. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi tulivyona hoja hii. Mimi naungana nao kama walivyosema na walivyota hoja zao. Niseme hoja hii ni ya msingi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina historia ya utamaduni na nchi yoyote ili iweze kutambulika ni lazima ijitahidi sana kuhakikisha inahifadhi utamaduni wake. Utatambulika kwa namna ya utamaduni wako ulivyo. Sisi kama Watanzania, tutatambulika kwa utamaduni wetu. Kwa hiyo, kuachia utamaduni wetu unakufa na kupotea, tunapoteza utambulisho wa Taifa letu. Nimefurahi sana, Mheshimiwa Mnyika ametoa hoja ya msingi, kuridhia Mkataba huu kutatufanya sasa tukimbie twende na wakati.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili linaonesha litakuwa na Mfuko Maalum na wakati tunachambua Azimio hili kwenye Kamati, Imeelezwa kabisa lengo la Mkataba huu ni kuhakikisha masuala ya umaskini yanapungua. Huu utamaduni tulionao tunaweza kuugeuza kuwa biashara, ikawa biashara kubwa ya Kimataifa. Yapo mambo mengi, Waheshimiwa Wabunge hawa wanasafiri kila siku, unafika kwenye Viwanja vya Ndege vya Kimataifa unakuta ni namna gani wenzetu wanahifadhi tamaduni zao; tamaduni zinazoshikika na zisizoshikika. Hata sisi kwenye Uwanja wetu wa Ndege wa Mwalimu Nyerere pale tunaweza kuweka muziki wa nyimbo za asili zinazoonesha makabila ya Watanzania ambao utapigwa kwa saa 24, abiria wanaposhuka pale wakutane na Ngoma ya Gobogobo na Lizombe kule Jimbo la Peramiho, wakutane na Saida Karoli anavyoghani mashairi ya Kihaya, akutane na nyimbo za Pwani kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hapo utaona kabisa kila mtu anajisikia kwamba, kweli ameingia katika Nchi ya Tanzania, anakutana na utamaduni wa Mtanzania na anaporudi hakika hatasahau alikotoka. Kwa kufanya hivyo, wapo watu wangevutiwa kuja kutafuta haya mashairi, nyenzo na kuna watu wangevutiwa kuja kuvitafuta vitu hivi viko wapi na hapo tungekuza utalii wa nchi yetu na kuongeza Pato la Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naipongeza Serikali, pamoja na kwamba, Kamati ilishangaa toka mwaka 2003 kwa nini hatukuridhia Mkatabaa huu kwa manufaa haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hapa, mimi naendelea kuutazama umaskini wa Watanzania na hiki ni kitu kingine cha kuwasaidia. Ninamshukuru sana Waziri alilieleza vizuri sana, tunaona kutakuwa na Mfuko, imeandikwa Mfuko huo utatoa mkopo wenge riba nafuu na utatoa misaada ya namna moja ama nyingine ya uhifadhi na *ku-promote* masuala yetu haya ya utamaduni. Wapo wasanii wetu wengi wanahangaika, hawajui wapate wapi pesa za kuwasaidia, hawajui waboresheje vipi kazi zao walizonazo

na si kwa manufaa yao tu, ni kwa manufaa ya nchi yetu pia. Sasa kumbe kupitia Azimio hili, Mfuko wetu wa Utamaduni wa Taifa ulioanzishwa kwa Sheria ya Bunge uko hoi; hauna pesa za kutosha, lakini Wananchi wachache wa Tanzania waliobahatika kuwezeshwaa na Mfuko huo wamefanya kazi za utamaduni nzuri na zenyeheshima sana ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumbe kupitia Azimio hili, leo tunaweza kuutumia mfumo wetu wa utamaduni ikawa ni kigezo na chombo cha kufanya tafiti za utamaduni wetu, namna ya kuhifadhi na namna ya kuzigeuza kutoka katika hali iliyopo sasa zikawa ni tamaduni zenyekuweza kutukuka na kupata heshima ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuliridhie Azimio hili, tulikubali, si tu kwa masuala ya kiutamaduni, lakini litasaidia sana kupambana na umaskini katika Nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea na taratibu za uanachama, itaundwa Kamati Maalumu ya Kiutendaji, itaanzzishwa Ofisi Maalum na Nchi Wanachama tutaruhusiwa kujiunga ama kwa *block* labda Afrika Mashariki tukaingia kwa pamoja au kila nchi itaingia kivyake. Sasa utaona hapa tunalo tatizo kubwa la ajira, ninaomba nirudie; ni tatizo kubwa ndani ya nchi yetu, lakini kwa kutumia Vyombo hivi vya Kimataifa, kama tutajipanga vizuri, vijana wetu watapata ajira katika hivyo vyombo na tutakuwa tumepunguza tatizo hili la ajira hata kama ni kwa theluthi moja.

Mheshimiwa Spika, nawaomba tuliridhie Azimio hili leo ili vijana wetu ambaowana elimu ya kutosha, wamesoma vizuri katika Vyuo vyetu Vikuu, wapate nafasi za ajira katika Vyombo hivi vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kujiunga na Mfuko huo kutoka katika Nchi Wanachama ni Dola 180 tu. Sasa kile tunachoweka na tutakachokipata ni kikubwa. Kwa hiyo, natoa wito kwa Serikali, Mikataba mizuri ya namna hii tusiwe tunailazia usingizi; ni Mikataba muhimu sana kwa maendeleo yetu. Dola 180 ndiyo ada ya kujiunga, sasa dola 180 kwa kweli iko ndani ya uwezo wetu, lakini tutakachokwenda kukipata ni mara mia tano elfu ya hii dola 180. Kwa hiyo ni kitu chema.

Mheshimiwa Spika, tumeona makabila mbalimbali yalivyoweza kushiriki katika shughuli za kuleta maendeleo; kule Kagera wanapokwenda kulima pamoja, wana neno lao wanalitumia, wakipiga ngoma asubuhi zamani watu walikuwa wanaondoka kwenda kulima. Unaona kabisa sasa hivi zipo namna nyingine za utamaduni wetu, utaambiwaa Kakakuona leo ameonekana Dodoma, akipewa mahindi ama maharage, maharage yatavunwa sana, akipewa maji mvua itanyesha, lakini hakuna anyeshughulika. Tukihifadhi vitu vya namna hiyo, wapo Wamarekani, Waingereza watasema ngoja tukaone huyo Kakakuona anavyofanya hicho kitu inakuwaje. Hivi ndiyo vitu vya kuhifadhi utamaduni usioshikika ndani ya jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi sana kwenye huu Mkataba. Mimi leo nafurahi na kuipongeza Serikali kwa kuleta Mkataba huu leo tuuridhie. Miaka yote hiyo

tulibaki Tanzania na Rwanda tu, basi leo na sisi tunajiondoa katika wale ambao walikuwa hawajaridhia tunaridhia na baada ya miezi mitatu tu, Mkataba unasema matunda hayo tunaanza kuyafaidi. Kwa hiyo, tunaanza kuhesabu kuanzia mwezi wa nne, wa tano na wa sita, mwezi wa saba tungependa Serikali iwe imeshajipanga *ku-domesticate* ili tuweze kufaidika na mambo haya yote.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana Wabunge wenzangu kwa michango yao na mimi ninawaunga mkono. Ninaunga mkono hoja ya Waziri na ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoletwa mbele yako leo asubuhi ya kuridhia Mkataba wa Kutambua Utamaduni wetu Usioshikika ndani ya Tanzania, kwa manufaa ya nchi yetu na kwa manufaa yetu sisi wenyewe Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako. Nami ingawa ni kwa mara ya kwanza kupata nafasi hii kusema katika Bunge hili, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu na niwapongeze Wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni, pamoja na Chama changu cha *Civic United Front (CUF)*.

Mheshimiwa Spika, mimi katika hili, nisiwe kama mwazima jamvi, napenda niunge mkono na niwashawishi Wabunge wenzangu tuuridhie huu Mkataba. Katika yale mambo ambayo yanazungumzwa kama changamoto, kuna mambo mengine pengine Kamati imeyataja kwa juu juu, naomba kidogo niseme nionavyo.

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto kubwa ambayo maisha ya Mtanzania yalikuwa kwa kiasi kikubwa yanadhibitiwa mno na siasa na hili labda pengine ndiyo moja ya sababu zilizotuchelewesha; kwa mfano, kule Zanzibar, Wananchi wana makabila yao kama ilivyo huku Tanaganyika au Tanzania Bara. Huku kuna watu wanawenza wakafurahia kuitwa Wazanaki, Wanyakyusa na wengineo, basi na kule Zanzibar kuna Watumbatu, Wapemba na Wamakunduchi na wana lugha zao, lakini ilifika mahali mtu akaambiwa usijiite wewe Mtumbatu au Mmakunduchi, sema wewe ni Mwafrika; ikashangaza sana kwa watu wenyewe akili, kwani huyu Mmasai aliyepo sehemu nyingine siyo Mwafrika?

Kwa hiyo, ninasema moja ya changamoto ni kwamba, utamaduni wetu huu usioshikika, umedumazwa sana; labda kwa kuridhia Mkataba huu, tutajikosoa baadhi ya makosa yetu na sasa tutaruhusu tamaduni za watu hawa zichangie ipasavyo katika suala zima hili la kuimarisha utamaduni wetu wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango. Nami pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili, naomba niwashukuru Wapiga Kura wa Jimbo la Iringa Mjini, kwa kuniyamini na kunifanya niwe Mbunge wao kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, ningeomba na mimi niunge mkono hoja hii kwa ipite, lakini nilikuwa na ushauri ambao kwa namna moja au nyingine, niliwahi kuutoa kwenye Kamati lakini ni vizuri nikausema hapa pia.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa, Taifa linakua na kwa sababu Taifa linakua ni lazima lipitie hatua mbalimbali. Hoja yangu ya msingi ni jinsi gani ambavyo Taifa tunapoupitisha Muswada huu hizi mila na desturi hazitatufanya tusiendelee mbele katika ulimwengu wa kisasa? Kwa sababu kama Taifa au kama kizazi ni lazima tupitie hatua tatu; tunapokea mambo ya nyuma, tunayapima kama yanatufaa kwa sasa, halafu tunayajadili, tunayaandaa kwa ajili ya kizazi kijacho. *We conceive, we criticize, we create.*

Mheshimiwa Spika, sasa kama Taifa ambalo linakua ni lazima tukae tuangalie ni mambo gani ambayo yalifaa katika kizazi kilichopita. *We are the product of previous generation but not prisoners of previous generation;* kwa hiyo, hoja yangu ya msingi ni jinsi gani tunapoupitisha huu Muswada, hatuwezi kuwa *prisoners* wa mambo ya zamani. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali kwamba, haya mambo tunapoyapitisha ni lazima tuangalie yanatufaa vipi katika kizazi cha sasa, inawezekana yalitufaa katika kizazi kilichopita yasitufae sasa na wakati huo huo tuna-*preserve*.

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine mzuri ni namna gani ambavyo tunahangaika sasa hivi, tunajitahidi kutafuta utamaduni wetu wa Kitaifa, lakini bado tuna lugha ya kichotara. Ukiangalia kwa sababu utamaduni tunaosema unahusiana na lugha, Kiswahili chenyewe hatuongei kwa ufasaha, ukimwona Mkenya anaongea Kiswahili fasaha kuliko Mtanzania. Kiingereza chenyewe hatuongei vizuri, kwa hiyo, tunajikuta tuna lugha chotara ambayo tayari ni changamoto kwa Taifa letu na sijaona mkazo ukitiliwa.

Nilipokuwa sijarika Bungeni, nilikuwa nasikia Wabunge mliokuwepo mnajadili kwamba, lugha itakayotumika Bungeni itakuwa ni Lugha ya Kiswahili, lakini sijaona msisitizo mkubwa; tumekuwa tukichanganya lugha hata sisi wageni tunajikuta tunachanganya lugha, kwa sababu hakuna msisitizo mkubwa ambao unatumika kama tunataka tuenzi utamaduni wetu tutatumia lugha gani, kwa sababu mila na desturi zinakwenda pamoja na lugha.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ambao hata nimejaribu kuuliza hapa ni Miswada inayoletwa kwa Wananchi, tunataka tuenzi lugha yetu lakini bado inaletwa kwa lugha ya kigeni; ni kuwatesa Wananchi hata Wabunge humu ndani tunateseka kwa lugha ambayo hatujui bila sababu ya msingi. Kwa hiyo; ni vizuri kama tunataka tuenzi mila na desturi zetu, tuanze na Lugha ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linanitatiza kidogo katika Muswada huu ni lile neno Matambiko, mambo mengine sina tatizo nayo, lakini neno tambiko linapoingia hapa linahusiana na imani; sasa unapokwenda kwa ujumla wengine hawaamini kama Taifa ambalo halina lugha, sipingani na imani hizo, lakini wengine hawaamini.

**SPIKA:** *Declare interest* kwamba, mimi ni Mchungaji, hayo mambo siyajui. (*Kicheko*)

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna watu wengine hawaamini mambo ya matambiko yanaendana na imani; sasa tukiliingiza moja kwa moja, mambo mengine sina tatizo nayo, lakini hili suala la tambiko kwa sababu lina-*involve faith*, nilikuwa nadhani Serikali ingeliangalia vizuri, haya mambo mengine yabaki lakini suala la matambiko lina-*involve* imani ambapo tukilichanganya kwa pamoja linaweza likaleta kikwazo kwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri haya mambo tuyajadili kwa mapana, tuangalie yanayotufaa yasije yakaharibu mwendelezo kwa sababu wenzetu pamoja na kwamba, wanalinda tamaduni zao, wana-*embrace* teknolojia ya kisasa ambayo tamaduni na mila haziwezi kuzuia maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhagama ameongea vizuri kwamba; ni kweli kabisa ukienda nchi zingine, kwa mfano, ukifika viwanja vyta ndege kama South Africa, utakuta nyimbo zao za kiasili zinapigwa, lakini ukija Tanzania utakuta saa zingine tunapiga nyimbo za South Africa *as if* Tanzania hatuna utamaduni wetu!

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi naunga mkono hoja, lakini ningeomba ushauri huu Waziri auzingatie. Ahsante sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mchungaji anashangaa matambiko ndiyo nini tena. Sasa nimwite Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Profesa Kahigi pia atapata nafasi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu. Kwa kuwa ni mara yangu ya pili, naomba nikiri tu kwamba, hakuna ziada mbaya. Nawashukuru Wananchi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi, ambao wamenipigia kura na kunileta katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nianze kumshukuru Waziri ambaye ameleta Muswada huu, lakini nimpongeze pia Waziri Kivuli wa Wizara hiyo husika, kwa maelezo aliyotoa na ninapenda nimpe taarifa kwamba, katika Nchi ya Ufaransa, lugha inayotumika siyo Kifaransa peke yake, wanatumia Ki-dutch na Kifaransa. Marekani wanatumia Spanish, English na French. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wanatumia lugha moja tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nikiri kwamba, naridhia Mkataba kwa maana kwamba, mpaka sasa hakuna athari yoyote ambayo tumeona kwamba, tutaipata kama tutaridhia Mkataba huu. Angalizo ambalo mimi ningependa tuliangalie ni kwamba, baada ya kuwa tumeridhia Mkataba huu, tusitumie vibaya hizi fursa, tuainishe

maeneo yote ambayo tunaona kwamba yanafaa kuwa urithi wa vizazi vyetu vya sasa na vijavyo. Kwa maana kwamba, pamoja na mambo mengine, tumekuwa tunaona Vyombo vya Habari vinatumika vibaya kupotosha Umma kutokana na historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa pili, nilisoma gazeti moja siwezi kulitaja, liliandika taarifa ambayo ilikuwa ni potofu kabisa; mimi naamini kwa kuandika taarifa hiyo, umma umepotoshwa.

Mheshimiwa Spika, katika chombo hicho waliandika taarifa kwamba, Mfalme wa Songea (Nduna Songea), alifanya biashara ya kuwachukua watumwa kutoka katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na kuwapeleka kwao; hii sijui yeye ameitoa wapi? Ninaamini kabisa, tutakaporidhia mkataba huu, historia yetu itaandikwa vizuri na itahifadhiwa vizuri na umma hautapotoshwa katika tamaduni na mila zetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hili ni hayo machache. Ninaomba tuisahau kuainisha maeneo yote; tunayo maeneo mengi sana hata katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, tunayo mapango ya asili katika maeneo ya Kipatimu, Chumo na Kibata; nawakaribisha sana tuandike na tuhifadhi urithi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia Mkataba huu. Kimsingi, mchango wangu ningependa kusema kwamba, hakuna Taifa linaloweza kuendelea bila ya kuwa na utamaduni sahihi au utamaduni ulio bora kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vilevile si kila utamaduni ni sahihi katika Taifa lolote, isipokuwa yapo mambo ambayo kimsingi yanaweza kuwa na faida kwa Taifa letu, ambayo ni sehemu ya utamaduni wetu; ni vizuri utamaduni ukajaribu kuzingatia falsafa ambayo inaliongoza Taifa letu kuhusiana na masuala mbalimbali ambayo yanahusiana na tamaduni tulizonazo.

Hoja iliyo mbele yetu kimsingi ni nzuri na mimi binafsi naomba ni-*declare* mapema kwamba naunga mkono japo kuna mambo ambayo tunapaswa kuyaangalia kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya ustawi wa Taifa letu na jamii ambayo inapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kimoja ambacho nikiangalia sehemu kubwa ya hoja iliyo mbele yetu imejikita sana kwenye kuangalia rasilimali fedha. Tukisema kwamba tujielekeze kwenye kuangalia tu kwamba rasilimali iwe ndio kitu cha msingi cha kutusukuma kwenye suala zima la kukubaliana na hoja iliyo mbele yetu, naamini kuna mahali tunaweza tukajikuta tunatenda vibaya.

Kwa mfano, kuna hoja ya matambiko, hii dhana ya matambiko nafikiri katika mazingira yetu inaweza ikatafsiriwa kwa mapana zaidi. Sasa tuangalie pengine kwamba

ipo haja ya Serikali kuweza kuangalia kwamba sasa ni matambiko ya aina gani? Isije ikatokea watu wanafanya matambiko ya kuweza kuhatarisha usalama wa watu kama ambavyo imepata kutokea hapa siku za nyuma kidogo watu wamekuwa wakiwadhuru jamii ya binadamu wenzetu aina ya *albino*. Sasa ni vizuri Serikali ikajaribu kuweza *justify* kwamba haya yatakuwa ni matambiko namna gani, pale ambapo inapokuja kuonekana kwamba kuna jamii fulani fulano ambazo zinaendesha matambiko haya ambayo hayaendani na misingi ya falsafa ya haki za binadamu basi waweze kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa ajili ya kulinda usalama wa watu pamoja na rasilimali zao.

Mheshimiwa Spika, isije kuwa tu kwamba tutanufaika kuweza kupata fedha nyingi kutoka kwa Mashirika na Jumuiya za Kimataifa ili hali kuna jamii ya watu ambao wanawenza wakapata matatizo baada ya Bunge kuwa limeridhia vigezo ambavyo vinaainishwa katika mkataba ambao umewasilisha leo hii ndani ya Bunge lako tukufu. (*Makofi*)

Lakini pia binafsi nafarijika juu ya suala zima la kuweza kuenzi utamaduni usioshikika na kuangalia jinsi gani ya kuweza *ku-promote* ndani ya nchi yetu hasa kwenye kipengele cha lugha, si kwamba lugha zote zinaweza zikapata fursa ya kuweza kutumika ndani ya nchi yetu isipokuwa katika makabila mbalimbali na katika maeneo ambayo makabila hayo huweza kupatikana.

Sasa ningependa kutoa pendekezo moja kama kweli Watanzania tuko *serious* kwenye suala zima la kutaka kuenzi tamaduni na kuweza kuziimarisha tamaduni zetu ni vizuri tukajaribu kuangalia lugha yetu ya Taifa ambayo ni lugha ya Kiswahili tunaijengea mazingira gani ya kuweza kutambulika kwamba ni lugha ambayo tunaithamini kama Watanzania na hapa moja kwa moja tu ningependa kuishauri na kuiomba Serikali ni kwa nini kama kweli sisi tunainenzi lugha ya Kiswahili kama sehemu ya tamaduni ambazo hazishikiki tusitumie katika kufundisha katika nyanja mbalimbali za kielimu, kama vile Vyuo Vikuu kwa sababu watu wengi unajikuta kwamba katika taasisi mbalimbali wamekuwa wakisoma kwa kukariri lugha za kigeni kwa sababu *competence* inaonekana kama vile ni hafifu mionganoni mwa Watanzania walio wengi hasa kwenye suala zima la kutumia lugha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, unazidi kujengeka utamaduni fulani mionganoni mwetu Watanzania kwamba mtu unapozungumza lugha za kigeni unaonekana kwamba wewe ndio msomi tu kwa sababu unazungumza lugha ya Kiingereza au unazungumza lugha ya Kifaransa. Hii naona binafsi kama ni dhana potofu sasa kama kweli sisi tuko *serious* na suala hili ni vizuri tukaanza kuitumia lugha yetu ya Kiswahili kama moja ya ishara na utambulisho wetu mkubwa kama Watanzania kwa sababu lugha ni kipengele muhimu sana katika suala zima la utamaduni wa watu. Kama hatuwezi tukaitumia lugha yetu ambayo *almost* inafahamika katika maeneo mengi sana hapa nchini kwenye kufundishia huko katika taasisi hasa ya elimu ya juu pamoja na sekondari na vyuo mbalimbali bado itabakia tu kwamba tunaenzi lugha hii kwa nadharia lakini kwa vitendo bado hatujawenza kuipatia nafasi kubwa sana. (*Makofi*)

Hoja ambazo zimekuwa zikitolewa za kusema kwamba Kiswahili hakina msamiati wa kutosha siyo sahihi. Tuna wana taaluma wengi sana wa lugha ya Kiswahili akina Profesa Kahigi nafikiri anaweza akachangia sijui kwamba pengine atachangia nini lakini tutamsikiliza. Kwa hiyo, ni vizuri tukajaribu kuangalia kwamba lugha ya Kiswahili sasa tuitumie katika maeneo mbalimbali na hii itaweza kudhihirisha kwamba kama Watanzania tunraithamini na kuiheshimu lugha yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Asante sana.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kuhusu hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza natanguliza kauli kwamba naunga mkono hoja hii. Pia sitarudia kusema ambayo yameshasemwa na nakubaliana na yote ambayo yameshasemwa hasa yale ambayo yanasisitiza mabadiliko katika mwelekeo wa kiutekelezaji katika Wizara.(*Makofi*)

Mimi nasema kwamba tumechelewa, nchi nyingi sana zimeanza zamani sana. Ukiangalia katika nchi za Afrika Magharibi Wanigeria wametutangulia, wako mbele zaidi kuliko sisi kuhusu masuala haya ya utamaduni usioshikika na ule ambao unashikikika. Ningependa kusitisitiza kwamba Serikali ijpange vizuri sana kiutekelezaji.

Kwanza kama ilivyokwishapendekezwa ipitie vizuri Sera ya Utamaduni. Sera ya Utamaduni kama ilivyo na tunavyoifahamu ina mapungufu mengi. Katika kuipitia sera hiyo iwashirikishe wadau mbalimbali, watalaam na watu wengine.

Pili, Serikali ichangie kwenye Mfuko wa Utamaduni. Nafahamu kwamba huo Mfuko wa Utamaduni ulipoanzishwa ni nchi moja tu ya Sweden ambayo ilichangia. Serikali ya Tanzania ilipaswa kutoa mchango lakini haikutoa mpaka sasa na sidhani kama imeshatoa mchango kwenye huo Mfuko wa Utamaduni. Kwa hiyo, napenda kuomba Serikali ianze kuliangalia hilo.

Tatu, Serikali kwa makusudi kabisa itenge fungu linalotosha kwa ajili ya taasisi zinazofanya utafiti katika lugha na tamaduni za Taifa letu. Taasisi hizo ni kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vyuo Vikuu vingine. Pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna taasisi ya taaluma ya Kiswahili, kuna mradi wa lugha za Tanzania ambao uko katika Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu. Huko Zanzibar kuna taasisi moja ambayo inahusika pia na tamaduni kama hizo. Serikali lazima ijithabidi katika Bajeti yake iwasaidie hawa watafiti ili wawewe kufanya utafiti katika tamaduni hizi zisizoshikika pamoja na lugha ili lugha hizo zihifadhiwe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningekusitisitiza ni kwamba Tanzania tumekuwa tumelala kwa muda mrefu hasa kuhusiana na utamaduni. Msimamo wetu kuhusu utamaduni umekuwa haueleweki mara utamaduni unahamishwa kutoka kwenye Wizara hii unapelekwa huko kwingine, mara unatolewa kwenye elimu

unapelekwa sijui kwenye michezo. Toka tupate Uhuru tumekuwa na mtindo huo ni kama tulikuwa hatujui utamaduni tuuweke wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni fursa nzuri ya kusahihisha kosa hilo. Utamaduni lazima upate nafasi, upate uzito, nchi nyingine ambazo zimeendelea hata nchi za Magharibi kwa mfano Uingereza hata Marekani utamaduni unapewa nafasi kubwa sana, sidhani kwamba Uingereza inapoanzisha *British Council* katika nchi mbalimbali inafanya hivyo tu kwa mzaha, hapana inatambua umuhimu wa utamaduni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba Bunge hili liishauri Serikali ianze kutambua hilo kwamba utamaduni siyo kwamba tu ni utambulisho bali pia ni rasilimali. Kiingereza kinaingiza fedha nyingi sana kwenye uchumi wa Uingereza na hata Marekani. Hata sisi tunaweza kujoingezea kipato kikubwa sana kwa kutumia Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kama nilivyokwisha tangulia kusema naunga mkono hoja hii. Lakini nasisitiza kwamba Serikali kwa kweli lazima ijipange vizuri la sivo hatutawenza kutekeleza mkataba huu kikamilifu kwa sababu ni mkataba ambao umegusia karibu kila kitu. Asante sana. (*Makofi*)

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kwanza na mimi kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu kwa heshima kubwa naomba niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunichagua kwao kuweza kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza napenda niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ambayo imeshughulikia Azimio hilo pamoja na Mawaziri. Mimi niseme Wabunge wenzangu Serikali yetu haijachelewa na bado inafanyakazi kubwa. Leo kupitishwa kwa Mkataba huu siyo sababu ya kufanya tujione sisi tuko nyuma, lakini pia mimi nitakuwa mkosefu wa fadhili kama sijaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa inayofanya ya kuandaa watu ambao wanawenza wakafanyakazi hiyo. (*Makofi*)

Mimi nilipata msaada kupitia UNESCO kama mwanamke kufundishwa *Diploma* ya Urithi wa Utamaduni *tangible* na *intangible*. Kwa hiyo, mimi nasema hatujachelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi nashukuru kwa kuletwa hili jambo hapa kwa kweli hili suala litatusaidia hata walimu kutoka shule za msingi, sekondari na hata vyuo kwa sababu sasa hivi vitabu vyote vyta maarifa ya jamii darasa la tatu vinazungumzia juu ya tamaduni za Mtanzania, asilia ya Mtanzania au makazi ya watu katika eneo lao. Kila wanafunzi wanafundishwa kulingana na Mkoa wao, Wilaya yao, Kijiji chao na Mtaa wao. Kwa kukuza kwetu hizi tamaduni na kuwekwa katika utaratibu mzuri wa

kuhifadhiwa itatusaidia hata kwa wanafunzi wale wa shule za msingi. Hivyo itasaidia katika kizazi hiki kilichopo sasa hivi na kile kinachokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nishauri bado tunazo *cultural heritage site* katika Mkao wa Dar es Salaam ambazo ni Uwanja wa Taifa wa Zamani (Uhuru) Nyumba ya Mwalimu Nyerere - Magomeni, *Nkurumah Hall* pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Makao Makuu ya *TANU* pale Mtaa wa Lumumba. Hizi ni sehemu za asili kabisa ambazo zinahifadhi utamaduni wa Mtanzania kabla ya Uhuru na baada ya Uhuru. Kupitishwa kwa Mkataba huu mimi naona iwe changamoto ya kuhifadhi zile nyimbo, tamaduni za Mtanzania, taratibu na yale mashairi ambayo yalitumika katika Uhuru na katika mambo mengine mengi basi viwekwe hata kama ni katika *CD* zake, au kanda au picha huko ili vile vizazi vya sasa waweze kutambua mwanzo wa Taifa lao mpaka kufikia katika Uhuru na mpaka kufikia katika Mfumo wa Vyama vingi na kufikia katika wakati huu tulionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja mkataba huu upitishwe ili ute faida kwa kizazi kilichopo na kizazi kijacho. Asante sana. (*Makofi*)

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja hii juu ya Mkataba kuhusu masuala ya Utamaduni wetu. (*Makofi*)

Kwa kweli hii ni fursa adhimu kabisa niliyoipata ikiwa hii ni mara yangu ya kwanza katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo kuweza kusimama hapa mbele yenu na mimi kutoa mchango wangu. Hii si kwa sababu ya uzembe au kwa sababu ya kutoelewa lakini ni kuwa mara nyingi tunavyotakiwa sisi wanadamu tujifunze kutokana na wenzetu waliotutangulia. (*Makofi*)

Pili, natoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha hoja hii. Kwa kweli hii ni hoja adhimu kabisa kwa sababu Taifa lisilo na utamaduni ni sawa na ng'ombe aliyeachiwa na kuweza kuharibu kila kilichobakia katika maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kulielewesha Bunge lako Tukufu kwa kuiunga mkono hoja hii kabla kwa asilimia mia moja kwa sababu moja kubwa ya msingi ni kuwa sisi Watanzania yaani Watanzania wa huku Tanganyika pamoja na Zanzibar nahisi utamaduni wetu kwa kiasi kikubwa umepotea. Kwa fursa hiyo tulioipata adhimu ya kupitishwa hoja hii leo katika Bunge hili Tukufu nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu hoja hii tushikamane na tuifikirie vizuri sana kwa sababu kukosekana kwa utamaduni ni sawa sawa. Narudia tena ni sawa na ng'ombe aliyeachiliwa na kuharibu kila kitu kilichopo katika maeneo. (*Makofi*)

Tatu, kwa mfano naona kwa kiasi kikubwa siku hadi siku zinavyozidi kuendelea Watanzania tunapoteza hadhi yetu kutokana kuhadaliwa na watu binafsi wanaotumia fedha zao kwa kupotosha utamaduni wetu. Maadili ya watoto wetu wa Tanzania kila leo

mpaka kesho, kila tukienda mbele yanazidi kuporomoka. Nachukua nafasi hii kutoa mfano mdogo kama huu ufuatao;

Kwanza, kuna hiki kitu kinachotangazwa kinaitwa *Miss Tanzania*, jamani hili si kosa kuitumia nafasi hii kwa kujipatia maendeleo sisi Watanzania lakini watu wenye fedha zao wanachukua nafasi hii kuturudisha nyuma kabisa katika tamaduni ambazo zilikuwa ni asili zilizokuwa zinachunga malezi ya watoto wetu na sisi wenyewe kwa ujumla. Kwa kweli ni kitendo cha aibu na fedheha kuwachukua watu kwa kutumia fedha zao wakawa wanawatembeza utupu na aliyetakiwa atembee utupu nadhani katika maumbile yetu kwa Mwenyezi Mungu ni wanyama tu hata wao wamepewa sehemu zao za kuwashifadhi ili wasionekane tupu zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Watanzania tumefikia pahala kwa sababu ya umaskini wetu tunawakaribisha matajiri au watu wenye fedha zao na kuweza kutukashifu kiasi ambacho watu wanatembea hovyo katika maeneo yasiyo halali. (*Makofi*)

Jamani Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nakuombeni suala hili tuliangalieni vizuri, tukichukua nafasi ya sisi tunatafuta maendeleo kwa kupatiwa fedha na watu wenye fedha zao, tutafikia mahali hata watoto wetu watatukataa na hii imeshatokea. Watoto wanathubutu hata kutusonya ndani ya daladala, hiki kitendo kama hiki utoto wetu sisi wenye umri wa miaka 50 sasa hivi tunaona ni kitu cha ajabu sana, halafu lingine tuihangalia hata hivi vyombo vyetu vya habari tumeviachia nafasi kubwa sana ya kupotosha utamaduni wetu, utawakuta watu wanacheza utupu jambo ambalo watoto wetu wadogo nao wanarithi kwa kuviangalia vyombo vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nisizungumze sana, naona nichangie hapa padogo tu kwa sababu uzoefu wangu bado ni mdogo kabisa na ni mara yangu ya kwanza, lakini nawaomba hoja hii tuiunge mkono mia juu ya mia kwa sababu tunaelekeea pahali pabaya sana sisi Watanzania kwa watu wanaotumia fedha zao kwa kuanza kutuchuza hovyo hovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar sasa hivi tumefikia pahala watoto jambo ambalo kwa utamaduni wetu wa Wazanzibari ilikuwa ni kitendo haramu kabisa kumuona mtu anatembea utupu, leo watu wanakuja kwa sababu tu tunahitaji tupate fedha kuititia watalii. Sasa mimi naishauri Serikali, hao watalii au hata watu wengine wanaokuja hapa ni njia moja ambayo tunazalisha au tunapata maendeleo kutokana na watu wanaokuja, lakini Serikali iangalie kuhusiana na suala zima la utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nikae na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi leo angalau nikaanza kujifunza katika Bunge lako hili Tukufu, asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante, umesema kama vile ulikuwa siku nyingi humu ndani. Haya Mheshimiwa Modestus Kilufi. (*Makofi*)

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Mimi pengine nianze kwa kusema wanaosema shukurani hazina mwisho, niwashukuru sana ndugu zangu wa Mbarali kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na naahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu wote kabisa.

Ndugu zangu, suala la utamaduni ni muhimu sana lakini mimi pengine niwe tofauti kidogo nisiseme kwamba tumechelewa, inawezekana kabisa ilifanyika hivyo kwa makusudi kwamba inaonekana ilikuwa turidhie toka mwaka 2003 lakini tukawa tumechelewa, inawezekana mazingira yetu kwa viongozi ambao walikuwepo wakati huo waliona ilikuwa sio muda muafaka lakini niseme labda sasa wakati umefika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu waasisi wetu tukichukulia Baba wa Taifa, kazi kubwa aliyokuwa nayo kwanza ni kuwaunganisha Watanzania na njia pekee ilikuwa ni kuwafanya wote waelewane kwa lugha moja na hiyo ilisaidia sana hata wanapojifunza shuleni ili wawe na lugha moja ambayo wanaelewana. Kwa hiyo, kwa sasa nadhani imefika wakati sasa Watanzania wanaweza wakazungumza Kiswahili, lakini vilevile wasisahahu lugha zao za asili. Lugha za asili zina faida kubwa, zina mafundisho, zinafundisha nidhamu, busara, hekima na mambo mbalimbali kuititia hadithi, vitendawili ambavyo vinapatikana kwenye lugha zetu za asili.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni mazoea zamani wazee wanakaa na watoto na wajukuu zao wanawaambia mambo mema ya hekima kuititia lugha zao, lakini mambo hayo sasa hivi yamepotea, tukiulizana humu majumbani kwetu inawezekana tunaojua lugha za nyumbani ni sisi wazee yaani baba na mama, lakini watoto wetu hawajui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kumbe zipo lugha za asili ambazo zingeweza kumueleza motto, zikamuonya akaelewa pengine kuliko Kiswahili, inawezekana sasa hivi tunasema nidhamu kwa vijana au kwa watoto wetu imepungua, inawezekana lugha hii ya Kiswahili haina makali ya kutosha ya kuwaonya; kwa mfano hivi mtu anatembea nusu uchi, yaani nguo fupi kabisa kabisa sasa tumewaeleza kwa Kiswahili imeonekana bado hawajaelewa, nadhani hizi lugha za asili tukizirejesha inawezekana utakapo waambia wakatuelewa kwa sababu ilikuwa haiwezekani kabisa binti akapita mbele ya watu wazima, watu wakubwa akiwa na nguo nusu uchi, ilikuwa haiwezekani, ilikuwa ni kitu ambacho hakiwezekani. Angeweza akaelezwa kwa lugha za asili na jamii yake wakamueleza asiendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile lugha za asili zilisaidia kwenye makuzi na malezi ya watoto kwa sababu ilionekana kila mtu anaweza akamuonya mtoto hata kama sio wa kwake, lakini leo hii imekuwa ni tofauti kidogo. Mtoto ambaye hakuhusu ukimuonya na pengine akakutukana, lakini kwa asili yetu sisi ilikuwa sio rahisi kwa mtu ambaye amekuzidi umri alikuwa anaweza akakuonya ukasikia, lakini leo imekuwa tofauti kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kabisa kwa kudumisha lugha zetu za asili, pengine inaweza ikatusaidia tukarudisha utamaduni wetu wa kila mtu, kila mzazi akawajibika kumuonya mtoto yeote hata kama sio wa kwake na pengine akamsikia. Imefikia hatua mbaya kwa sasa hivi kwamba watoto wetu hata sisi wenyewe tumeanza kuiga utamaduni ambaio sio wa kwetu, kwa mfano ni kweli nakubaliana kwamba yatima ni wengi sana kwa sasa hivi, kutokana hasa na maradhi yametukumba, lakini kweli ndugu hawapo kabisa?

Kwa lugha zetu za asili kulikuwa na maneno ambayo yalikuwa yanakufanya ndugu umjali sana uone kwamba ndugu yako ni sehemu ya utajiri, kuwa wengi ilikuwa ni sehemu ya utajiri wa kujivuna, lakini leo hii, mjomba mtu hawezi kumchukua mtoto wa dada yake eti tu kwa sababu yeye sasa hivi tunabana matumizi, huwezi kumtunza kwa sababu hali ya maisha ni ngumu. Kwa hiyo, unakuta watoto wengine ni yatima wako mitaani, lakini ukifuatilia wanandugu kabisa, wapo wajomba, akina shangazi, wapo watu ambaio kwa mila na desturi yetu sisi usingeweza kuwaacha, lakini leo sasa tunaacha tu kwamba huyo ni yatima hana baba, hana mama, lakini ukifuatilia ana mjomba na ana shangazi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hizi lugha zetu za asili ziliweza kutufanya tuwe wamoja zaidi, japo kwa wakati ule ilionekana zingeweza kututenganisha maana yake ingewezekana kabisa hata shuleni watu wasielewane kila mtu akawa anakuja na lugha yake anaongea kwake, lakini nadhani kwa sasa tukubaliane kwamba muda umefika sasa wa kuenzi lugha zetu za asili kwa sababu ya athari tunazoendelea kuziona, mmomonyoko wa maadili, nadhani tukirudi huko nyuma kwenye lugha zetu za asili wazee wetu watapata nguvu tena ya kuweza kuwaonya vijana na watoto pengine wakaweza kusikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameunga mkono, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hili Azimio. Kwa kuwa leo ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu basi na mimi ninaomba nimshukuru sana Mungu aliyekiyeza kufika mahali hapa. (*Makofi*)

Pili, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Geita walioniamini na kunituma mahali hapa, zaidi nawashukuru akinamama wa UWT Mkao wa Geita kwa kunichagua kwa kura nyingi sana wakiamini kwamba nitakuja kuwawakilisha sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa namna ya pekee tena kwa kuwa nimepata nafasi hii. Kwanza kabisa niwaombe Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja hii asilimia mia moja, ninasema hivyo kwa sababu nilichokiona hapa kinalenga kutusaidia Watanzania kwa hali ya juu sana. Kwa kuchangia zaidi ningependa nijielekeze moja kwa moja kwenye kipengele kimoja kinachohusu muziki, hapa ninamaanisha muziki wa kisasa na muziki wa asili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sanaa inaleta maendeleo makubwa sana katika nchi yetu hasa tukianzia sisi wenyewe majumbani kwetu, lakini kwa kuwa bado tuna hali ngumu wanamuziki na hasa burudani ya muziki kwa kifupi na hawa watu wa ngoma za kiasili na kwa kuwa tuna nafasi nzuri hii ya kujiunga na hawa *UNESCO*, tukijiunga na *UNESCO* ninaamini kabisa tutaweza kubadilisha baadhi ya vitu ambavyo vinatukwamisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mataifa mengine yaliyoendelea wana nafasi nzuri sana hasa katika muziki na shughuli zingine mbalimbali. Wanamuziki wenzetu walioendelea huko duniani wanafanikiwa sana hata akitoa wimbo mmoja, wanafanikiwa kwa kufanya nini? Wanafanikiwa kwa sababu akitoa wimbo mmoja unapigwa ule muziki na ukipigwa anaweza kuwa analipwa *percent* fulani kutokana na hiyo kazi hata kama hajafanya *album* nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi naongea kwa mara ya kwanza na kwa sababu mtoto anapoanza kuongea huwa anaanza na neno “ba” baadae anakuja kuunganisha inakuwa “baba” inakamilika kuwa sentensi nitaomba nieleweke kwa kuwa ndiyo kwanza ninaanza kuongea kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba katika maandalizi haya ya kuingia katika huu mkataba niombe basi wazingatie kitu kimoja ambacho kitatusaidia sisi wasanii wa muziki pamoa na ngoma hizi za asili kwamba kila wakati inapotokea muziki umepigwa mahali popote au vikundi vyta ngoma vimetumbuiza mahali popote au umepigwa katika redio ama katika *television*, basi wakiongezee hiki kipengelee kwamba wawe wanapata *percent* fulani wale walioandaa hiyo kazi, ili iweze kuwa-*motivate* zaidi kuendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja, asante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hatuwezi kumuita mtoa hoja aanze kujibu hoja zetu au kufafanua mambo ambayo tumezungumza. Tunakusudia kwamba mchana tutaingia katika ule Muswada mwingine wa *UNESCO*, huo huo wa Azimio la *UNESCO* hivyo hivyo.

Kwa hiyo, tumpe nafasi Waziri aende akaangalie haya mliyozungumza, halafu tukirudi saa kumi na moja, yeye ataanza kujibu halafu ataingia na kwa Muswada huu mwingine ambaa umepangiwa hivi leo.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo ningependa pia kueleza kwamba Wabunge katika kipindi chenu cha Ubunge cha miaka mitano mnayo nafasi ya kupata *pass* ya kusafiria yenye hadhi ya kidiplomasia, kwa hiyo, kuna hawa watumishi wa Idara ya Uhamiaji wako hapa Ofisi ya Bunge, eneo la mapokezi katika Jengo la Utawala.

Kwa hiyo, wale ambaa bado hawana hati waweze kujieleza pale, waweze kuambiwa wanavyostahili. Ni vizuri kuwa na hizo hati kwa kipindi hiki ambacho

mnakuwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu inawezekana akatokea safari isiwe tena tunaanza kutafuta *pass*. Kwa hiyo, mtumie huduma hiyo. (*Makofi*)

Pia tulisema kubadilisha leseni tunayo pia ofisi hapa hapa, mnaweza kubadilisha leseni zenu hata za madereva wenu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo sina tangazo lingine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi nilikuwa nimesema sasa tutaingia kwa Waheshimiwa Mawaziri kujaribu kutoa ufanuzi kwa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge walizofanya. Lakini hatukushauriana na Waziri kama ataanza Naibu au anaanza moja kwa moja. Anaanza Naibu *okay*, Mheshimiwa Waziri kwa sababu kuna Muswada mwingine. Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, maswali na maelekezo mbalimbali waliyoyatoa na moja kwa moja nitambue Waheshimiwa waliochangia ajenda yetu ya leo.

Mheshimiwa Spika, nianze kumtambua Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wengine ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Modestus Kilufi na Mheshimiwa Vick Kamata. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Aina Mohamed Mwidau, pamoja na Mheshimiwa Pinda Chana ambaye hapo awali nilimtaja, lakini amechangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuishukuru sana Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa maelekezo mbalimbali na hasa katika kukuza utamaduni wetu. Niwahakikishie kwa maelekezo yote waliyoyatoa kwenye vikao vya Kamati lakini pia katika uwasilishaji wao wa leo tumeyazingatia na tutayatekeza. Lakini vile vile nitambue mchangano binafsi wa Mheshimiwa Jenista Mhagama kuhusu umuhimu wa kuhuishwa Sheria mbalimbali ili ziweze kwenda sambasamba na mkataba huu. Tumezingatia,

tutaufanya kazi ili kuboresha taratibu na kanuni za kulinda utamaduni usiosikika, hili tumelizingatia na umuhimu wa kukuza Kiswahili. Lakini vile vile kutumia nafasi hii kuinua ajira ndani ya nchi. Nimhakikishie Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba tumezingatia mchango wake na tutaufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kabwe Zitto, hoja yake ya utunzaji wa lugha za asili katika historia na maandishi, tumeuzingatia ni hoja ya msingi. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekuwa kikitufanya kazi hii kwa muda mrefu sio kwa kiwango kikubwa kinavyopaswa, tutaweka msisitizo ili kazi hii ifanyike kwa eneo kubwa zaidi na kwa taasisi nyingi zaidi. Lakini vile vile hoja ya Bajeti kuongezwa katika eneo hili la lugha la asili tumeizingatia ni hoja ya msingi tutaifanya kazi.

Hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kuhusu kurudisha utaratibu wa *ma-chief*. Wazo hili ni jipyä na tutalifanya kazi, tupime faida na madhara kwa kuzingatia madhara ya sasa na hoja zilizofanya ziondolewe wakati ule kama hoja hizo bado zipo au zimekwishaondoka. Tukiona umuhimu wa kufanya hivyo tutawashirikisha wananchi na viongozi na hasa Waheshimiwa Wabunge ili tufikie uamuzi wenye nasaba njema katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika aliongelea sababu zipi zilizosababisha kuchelewa kuwasilishwa kwa Muswada huu mpaka leo. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwamba moja ya hatua za awali kabisa tulizochukua ni kuhakikisha kwamba itifaki zote muhimu zenye maslahi kwa nchi zinafanyiwa kazi kwa haraka katika kipindi cha mwaka huu na kazi tuliyofanya leo ni moja ya kutekeleza mwelekeo huo. Kwa kweli ninachokiona kwa Mheshimiwa John Mnyika ni dhamira yake tu inafanana na yetu kwa hiyo tunakwenda pamoja vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa *African News Charter* nayo kuletwa Bungeni, nataka nimhakikishie Mheshimiwa John Mnyika kwamba huo ni tayari, ni uamuzi wa Serikali kwamba jambo hili lifanyiwe kazi mapema. Nimekwisha agiza kwa watendaji wakuu wa Wizara wiki iliyopita na mchakato wa kulifanyia kazi umekwishaanza. Suala la kuhuisha Sera ya Utamaduni linafanyiwa kazi kwa ukamilifu, tumekwishaanza mchakato wake, muda si mrefu mtapata taarifa kamili ya kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Assumper Mshama, ameongelea haja ya utunzaji na uendelezaji wa hati miliki na hati shiriki. Nataka nimhakikishie kwamba tunatambua kwamba jambo hili ni kwa maslahi kwa wasanii wetu na ni muhimu likazingatiwa. Tunalifanya kazi na tutaendelea kuimarisha katika hatua ambazo tumeshafika mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa kipindi cha Zamadamu ambacho kinapatikana kwenye *TBC*, tumekwishatoa maelekezo kwa *TBC* wiki mbili zilizopita kwamba wachukue hatua ya kukiboresha zaidi ili kiendane na utamaduni wetu. Lakini pia kiwe na faida kwa vijana wetu badala ya kuwa na madhara. Ni matumaini yetu ni

kwamba *TBC* watatekeleza maelekezo hayo, tukiona inashindikana marekebisho tutachukua hatua zaidi ya kuona kwamba hakileti madhara kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haji Faki Makame aliongelea jinsi ambavyo tamaduni zetu zimekuwa zikidumazwa, ndiyo msingi wa azimio lililopo mbele tu ambalo kimsingi tutakapokuwa tumeliridhia na kuanza utekelezaji wa ndani ya nchi maana ni yake tutakuwa tumeanza kuchukua hatua za kuondoa kudumazwa huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, yeye aliongelea kuchambua tamaduni zinazofaa na zisizofaa kwa mazingira ya sasa. Nasema hoja yake ni ya msingi, tutaifanyia kazi. Lakini vile vile aliongelea umuhimu wa kuwa na ufasaha wa lugha. Kwa kweli ni tatizo la msingi kwa watu wetu wengi. Kama ambavyo alisema yeye mwenyewe kwamba matukio ya makuzi yamemuathiri na yeye mwenyewe amekuwa akichanganya lugha sana, lugha hizi na kwa kweli kila mmoja wetu amepata athari hiyo. Naomba tu tuendelee kufanya jitihada kubwa ya kuboresha kuona kama lugha tunayotumia iwe tunayotumia badala ya kuchanganya lugha mbalimbali ambayo inaweza ikaleta matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya matambiko, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa aliongelea uwezekano wa kuiondoa hoja hii katika uwasilishaji huu kwa sababu inawezekana pengine usiwe na manufaa au ukawa na matatizo kama yale ya *albino*. Labda niseme tu kwamba waraka huu wa leo haukusudii kuanzisha shughuli mpya za matambiko. Tunaongelea vitu ambavyo tayari viro, tunachotakiwa ni kuvitunza na kuvienzi. Lakini kama ambavyo nilisema katika uwasilishaji wangu mapema asubuhi kwamba shughuli hizi zote za kiutamaduni zitazingatia haki za binadamu na sheria ambazo tunazo. Vitu ambavyo havizingatii haki za binadamu, ikiwemo hiyo ya mauaji na nini haviwezi kukubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mhesihmiwa Msigwa kwamba katika hili tuko pamoja, aondoe hofu ya uwezekano wa azimio hili kuleta madhara kwa utaratibu wa maisha ya watu wetu kwa kuvunja Sheria.

Mheshimiwa Murtaza Mangungu, yeye alisema tuainishe maeneo yanayofaa kuwa urithi kwa nchi yetu. Nasema hiyo ndiyo moja ya mambo ya msingi baada tu ya kuridhia mkataba huu na kuanza kuufanyia kazi ni kuainisha maeneo hayo. Lakini vile alitaka taarifa mbalimbali ziwe zinatolewa kwa usahihi ili kutokupotosha wananchi. Jambo hili ni la msigi, tumelichukua na wanaohusika wengine wamelielewa. Ni wazi kabisa kwamba watalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Moses Machali yeye aliongelea kufundisha Kiswahili katika ngazi mbalimbali za elimu yetu ili Kiswahili ndiyo kiwe lugha ya mawasiliano katika elimu yetu ya ngazi mbalimbali. Serikali haina pingamizi katika jambo hili, isipokuwa tu inatakiwa kuchukuliwa kwa umakini wa hali ya juu. Kwa sababu ni wazi kwamba katika lugha kubwa za Kimataifa ni pamoja na lugha inayotumika sasa ya Kiingereza katika shule zetu katika ngazi ya sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonyesha kwamba kiwango chetu cha kujua lugha hii kimeendelea kushuka siku baada ya siku. Nadhani ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kazi hii ya kuendelea kushuka kwa uwezo wa kutumia lugha hii ya Kimataifa kwa watu wetu inapungua. Tusitengeneze mazingira yanayofanya ndiyo tunaiua lugha hiyo. Katika matatizo ya msingi ambayo Watanzania wanayapata katika ushindani wa ajira ya Kimataifa ni kushindwa kuwa na lugha ya mawasiliano ya Kimataifa, kama Kiingereza na Kifaransa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine wanataka mtu ajue lugha zaidi ya mbili za Kimataifa ukiacha lugha aliyotokanayo nyumbani kama Kiswahili. Nataka niseme kwamba tunapochukua maamuzi ya namna hii lazima tuwe makini sana kuhakikisha kwamba hatuwi chanzo cha kukosa ajira kwa vijana wetu kwa siku za usoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Profesa Kahigi aliongelea Serikali kujipanga kiutekelezaji. Nataka nimhakikishie kwamba tumejipanga na kuhuisha Sera ya Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kuchangia kwenye Mfuko wa Utamaduni, niseme jambo hili ni la msingi na tunalifanyia kazi. Lakini vile vile Serikali itenye fungu kwa ajili ya utafiti wa lugha. Nalo hili jambo ni kubwa na la msingi, tumelipokea na tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kuhamishwa hamishwa kwa Idara ya Utamaduni, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Profesa Kahigi kwamba ni kweli imekuwa ikihamishwa lakini kuna kila ushahidi kwamba mahali ilipowekwa sasa ndiyo mahala pake na itaendelea kuwepo hapo hapo na tutafanya kazi vizuri tu kuhakikisha kwamba hatuangushi matarajio yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kisangi aliongelea umuhimu wa nyimbo, mashahiri na ngonjera zilizotumika wakati wa Uhuru kuwekwa katika kumbukumbu. Nasema hili nalo ni jambo kubwa na la faraja kwamba hatuwezi kuipoteza historia yetu ya mapambano ya Uhuru kirahisi. Tukitunza vitu hivi vitatusaidia, ni wazo jipya, zuri na la maana sana. Tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, aliongelea habari ya mashindano ya *u-miss* pamoja na watu kutoxaa mavazi yanayostahili. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Rashid Ali Omar kwamba msingi wa azimio hili siyo kuua tamaduni zingine, isipokuwa kutoa kipaumbele kwa tamaduni zetu na kuzienzi zaidi. Kwa hiyo, ni wito wangu kwa wanaohusika kama ambavyo Serikali imekuwa ikifanya siku zote kuona kwamba mashindano mbalimbali yanazingatia pia tamaduni zetu na hayawakwazi Watanzania ambao ndiyo wanakua sasa ili wao nao waje wawe wazazi na walezi wa baadaye wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyetu vya habari kutoa picha za namna hiyo au filamu za namna hiyo vimesikia na mimi natoa maelekezo kwa vyombo hivi vya habari

kujitahidi sana kuzingatia, pamoja na wajibu wa kuhabarisha tuna wajibu wa kulea watoto wetu na vijana wetu ili waendane na maadili bora ya Taifa letu.

Mheshimiwa Modestus Kilufi, aliongelea kushuka kwa maadili katika nchi yetu kiasi cha watu kutokuheshimiana kwa rika na watu kutojali yatima. Niseme tu hili nalo ni la msingi. Ni matokeo tu ya utandawazi tunaouongelea kwamba leo, labda niseme tu kwamba wakati mwingine pia sisi ambao tunatakiwa kupewa ile heshima wakati mwingine tunakuwa tunaikataa makusudi. Unafika mahali Mheshimiwa una miaka 40, kijana wa miaka 20 anakuamkia shikamoo, unamwambia aaah, mimi kijana bwana. Sasa ukishafanya hivyo kesho yake akikutana na wewe hatakuamkia na akikutana na mtu mwenye umri kama wako pia hatamwamkia. Lakini kuna mambo mengine mengi pia ambayo yamesababishwa na jambo hilo kwamba zamani mtu mzima akikosea unasema mimi nadhani ulichosema si sahihi, unaipoza lugha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku hizi haujali, unasema, akisema mtu mzima kitu unadhani kakosea hata huyu muongo huyu. Sasa inategemea kwamba jambo hili linasemwa wapi. Likikuzwa kwenye eneo ambalo ni jengo kubwa kwa mfano linatawanyika kwa kas na kuvunjiana heshima kunaendelea kukua katika jamii.

Kwa hiyo, niwaombe tu viongozi tuongoze kwa mfano na yale ambayo tunataka vijana wetu waige na kutufuata sisi wenyewe tutangulie kuyafanya, lakini pia ya kupendana na kujaliana katika jamii, kutunzana ni muhimu, ni sehemu ya utamaduni ya makabila karibu yote ya Kiafrika. Ni vizuri kuuenzi utamaduni huu, tuendelee kwa utaratibu huo.

Mhesihmiwa Vick Kamata, ye ye aliongelea malipo kwa wanamuziki kwa kuzingatia nyimbo mbalimbali zinazopigwa. Nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli kwamba kwa maeneo mengi ya nchi zilizoendelea, wanamuziki wetu na wasanii mbalimbali wamefanikiwa kwa sababu ya kazi zao kupimwa kwa vipimo sahihi katika maeneo mbalimbali na kupata ujira unaofanana na shughuli wanazozifanya. Niseme tu na sisi tumeanza kuchukua hatua. Moja ilikuwa hiyo ya kutunga Sheria na Hati Miliki na Hati Shiriki, lakini pia tumeendelea kuchukua hatua za kuiboresha na sasa hivi tunaifanya kazi tuko katika mazungumzo ya kitaasisi ya Wizara, Wizara kuona tunaboresha kiasi gani. Lakini niwahakikishieni kwamba kama Wizara tunakerwa sana na hali ya wasanii wetu kuendelea kuishi kwa taabu huku wakifanya kazi kwa jasho jingi ambalo halina tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pindi Chana aliongelea nini ni utamaduni wetu, tuna makabila mengi. Tujue mavazi yetu ni nini, chakula na nini.

Mheshimiwa Spik,a niseme tu tamaduni zote za makabila 120 tunazikubali na hasa kama nilivyosema awali ambazo hazina madhara kwa nchi yetu. Ni namna tu ya kuendelea kuzienzi na kuziimarisha. Lakini pia Mheshimiwa Pindi Chana alitaka tuviimarishe vyombo vinavyosimamia mambo ya kiutamaduni kama BASATA na Bodi

ya Filamu. Nimhakikishie kwamba ushauri wake tumeusikia na tunaufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Aina Mohamed Mwidau, ye ye aliongelea umuhimu wa kutunza utamaduni wa pande mbili za Pwani na Bara. Hoja yake ni ya msingi, tunakubaliana nayo na tunaifanya kazi.

Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga aliongelea hoja ya kutilia mkazo mavazi yenye maadili, kutilia mkazo mila zetu za awali ambazo zilikuwa zinafundisha vijana maadili mema, umuhimu wa vyombo vya habari kutangaza matangazo yanayohusu utamaduni na kuendeleza lugha za jamii mbalimbali. Michango yote aliyoitoa ni ya msingi na tunakubaliana nayo mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, ye ye naye aliuliza kwamba tunayo makabila 120. Katika mchakato huu wa kuimarisha tamaduni zetu ni khabila lipi ambalo ndiyo litakalotambulika kwamba tamaduni zake ndiyo tamaduni za Taifa? Nataka nimhakikishia tu kwamba makabila yote tutayatambua katika mchakato huu ikiwa ni pamoja na Wabena na Wapangwa, makabila yote 120 pamoja na wote wanaotoka Mbeya Mjini wote hawa wanahusika na mchakato huu. (*Makofi/Kicheko*)

Vile vile aliongelea habari ya vyombo kuzitunza na kuzitambua lugha za asili. Nakubaliana naye mia kwa mia kwamba ni jambo muhimu na la kweli tatalitekeleza katika mchakato huu tunaoendelea nao. Lakini pia aliongelea mambo ya jando na unyago kwamba sasa utamaduni huu umebadilishwa tu na kurudishwa ule utamaduni unaitwa *Kitchen Party*, lakini tulikuwa na utamaduni mzuri, lakini alisema ni vizuri ukazingatia rika. (*Makofi*)

Mimi sina pingamizi na changamoto yake, ni wajibu wa makabila yanayohusika kuona wanaendelezaje utamaduni wao huo bila kuathiri rika, lakini bila kuathiri makuzi ikiwa pamoja na elimu kwa vijana wao, kwa maana yapo makabila ambayo watu wakifika miaka 12, 13 wanapelekwa kwenye mambo ya unyago halafu hawatakiwi kwenda shule tena wanaambiwa asubiri mume. Sasa hii haikubaliki katika mazingira ya dunia ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi vile vile aliongelea umuhimu wa vyombo vya habari kutumia lugha zetu za asili katika matangazo yake mbalimbali. Labda niseme tu katika mambo yote aliyoasema hili ni jambo pekee sikubaliani naye na sababu yake ni rahisi tu kwamba ni kweli kwamba mwanzoni mapema kabisa nchi yetu ilipopata Uhuru tulikubaliana na sheria zikawekwa za kwamba kitumike Kiswahili kama lugha ya Taifa na ndiyo itumike kwenye vyombo vyetu vya habari. Msingi wake ni kujiepusha na hamasa za kubaguana na kilitenga Taifa kuliweka katika matabaka mbalimbali. Hakuna ushahidi wowote kwamba chachu ya mgawanyiko katika Taifa imeisha. Hakuna ushahidi wowote kwamba ukabila hautaweza kurudishwa kwa visingizio vya radio hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya lugha ni mazuri tu kama ina faida kwa jamii yake katika maeneo mbalimbali. Niseme tu kwa mfano Mheshimiwa Mbilinyi hakuna mtu asiyejua umuhimu wa kisu, kina matumizi mengi mbalimbali, mtu anafanya kukatia nyama, kukata nyanya, kukata mkate, lakini kisu hicho hicho hakiruhuswi kuingia nacho Bungeni kwa sababu unaweza ukakasirika kidogo mtu amekudhulumu habari fulani ya zamani ukaleta madhara kutokana na kisu kile ulicho nacho. Sasa nasema lazima uamue unatumia wapi. Kwa hiyo, nasema lugha hii ya Kiswahili ndiyo lugha muafaka kwa sasa na jambo lolote ambalo linaleta mwelekeo ambao linaleta dalili tu kwamba linawenza likalifikisha Taifa katika mgawanyiko, mparaganyiko na machafuko Serikali makini kama ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete lazima iendelee kuizua kwa nguvu zake zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kusema kwamba matumizi ya redio zetu na vyombo vyetu vya habari hayajawa mazuri sana. Ninyi mtakuwa ni mashahidi siku za hivi karibuni yapo magazeti kama mawili hivi ambayo yamekuwa yakichochea mivurugano kwa misngi ya dini; moja la kikristu na moja la kiiislamu, yanachochea migawanyiko kwa misngi ya dini. Lakini vilevile ipo redio moja inachochea migawanyiko kwa misngi ya dini. Sasa nichukue nafasi hii kusema kwamba hatutawaonya tena maana haya ni mambo ya msingi kwa Taifa, kauli hii ni ya kwanza na ya mwisho, tutachukua hatua kwa sababu hatuwezi tukaruhusu nchi ikagawanyika katika mazingira yoyote na kuleta uchafuzi katika jambo ambalo kila mtu mwenye akili timamu anajua kwamba hapa tukiliachilia jambo hili nchi inaparaganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa UNESCO wa Kulindwa kwa Urithi wa Kiutamaduni Usioshikika wa mwaka 2003 (Conversion for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage, 2003) liliridhiwa na Bunge*)

**Azimio la Bunge la Kuridha Mkataba wa UNESCO Unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 (Convention on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions, 2005)**

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 (*Convention on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions, 2005*).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa maelekezo na michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili katika kikao baina ya Kamati na Wizara yangu, tarehe 29 Machi, 2011. Napenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba michango yao na maelekezo yao tunaithamini na yote tutaitekeleza na kutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu mapendekezo ya Kuridhia Mkataba uliokusudiwa ambao ninaliomba Bunge lako liweze kuridhia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msukumo wa kuanzisha Mkataba wa *UNESCO* unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 (*Convention on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions*) ulitokana na athari za kukua na kuenea kwa haraka kwa utandawazi duniani na falsafa zake za kutaka ulimwengu uwe wenyе mfano mmoja, ukijumuishwa utamaduni wake. Hali ya namna hiyo iliyapa mataifa yenye nguvu za kiuchumi fursa ya kueneza tamaduni zao ulimwenguni, huku tamaduni za mataifa machanga na yanayoendelea zikidumazwa na kutishiwa kumezwu kabisa. Dunia nzima kuwa na utamaduni unaofanana ingechosha na kuchusha sana. Hata haja ya utalii wa kutembelea nchi nyingine ili kuona amali za kiutamaduni za huko isingekuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia hali hiyo isitokee duniani, *UNESCO* ilipitisha Mkataba unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanauai wa Kujieleleza Kiutamaduni kwenye Mkutano wake Mkuu wa 33 uliofanyika Oktoba, 2005 huko Paris. Nia na madhumuni ya Mkataba huu ni Kulinda na Kuendeleza Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni ili kuzuia baadhi ya tamaduni kumezwu au kukandamizwa na tamaduni nyingine kwa nguvu za kiuchumi au kisiasa. Hivyo basi, Mkataba huu unalenga kuzisaidia nchi wanachama kulinda na kaunufaika na tamaduni zake pasipo kunyanyaswa au kubaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila jamii hujieleza kiutamaduni kupitia ubunifu wa watu au makundi ya watu kwa njia mbalimbali kama vile hadithi, sauti, muziki, picha, michoro, filamu, sanamu, kusuka, kudarizi, ngoma, maigizo na vitabu. Njia hizi za kujieleza huzaa bidhaa na huduma mbalimbali za kiutamaduni ambazo ni za kipekee na kwa upande mwingine, ni utambulisho wa jamii husika. Viwanda vinavyohusika na njia hizi za kujieleza ndivyo huitwa tasnia za utamaduni.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu una sehemu saba zinazojumuisha Ibara 35. Aidha, kuna nyongeza ya Mkataba (*Annex*) inayohusu taratibu za usuluhishi. Vipengele muhimu vya Mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kulinda na Kukuza Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni;
- (ii) Kutengeneza mazingira mazuri kwa tamaduni kustawi na kuingiliana pasipo mikwaruzano;

(iii) Kuhamasisha mwingiliano mionganoni mwa tamaduni mbalimbali huku ikizingatiwa kuwa mabadilishano hayo ya kiutamaduni duniani yana usawa, yanajenga kuheshimiana na amani;

(iv) Kukuza heshima kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni na kufanya thamani yake itambuliwe kijamii, kitaifa na kimataifa;

(v) Kusisitiza umuhimu wa utamaduni katika maendeleo ya kiuchumi, hasa katika nchi zinazoendelea;

(vi) Kutambua sifa bainifu za kipekee za shughuli, bidhaa na huduma za kiutamaduni kama utambulisho muhimu wa Taifa mahususi; na

(vii) Kutoa fursa ya kushirikiana na kusaidiana kimataifa katika ulinzi na ukuzaji wa Uanuai na Kujieleza Kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, katika harakati za kulinda na kukuza Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni, haki na uhuru wa msingi wa binadamu na hata wa mataifa washirika wa Mkataba huu vitazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne ya Mkataba huu inatoa fasili au ufanuzi kuhusu “Uanuai wa Kiutamaduni.” Kwa minajili ya Mkataba huu “Uanuai wa Kiutamaduni” ni zile njia mbalimbali ambazo kwa tamaduni za jamii huelezeka. Njia hizi za kujieleza hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine na huwa katika maumbo tofauti tofauti ya bidhaa za kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, “Kujieleza Kiutamaduni” ni ile hali ya kutoa taarifa (au mafunzo) fulani mahususi kutokana na bidhaa za kiutamaduni zinazozalishwa na watu binafsi, vikundi vyta watu ama jamii. “Tasnia ya utamaduni” humaanisha viwanda ambavyo huzalisha na kusambaza bidhaa na huduma zinazowezesha jamii kujieleza kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Ibara za Tano hadi ya Kumi na Saba ya Mkataba huu zinaeleza haki na wajibu wa nchi washirika wa Mkataba huu. Nchi hizo zitawajibika kutekeleza yafuatayo, mionganoni mwa mambo mengine ni:-

Kwanza kuweka taratibu na kanuni za kulinda na kuendeleza uanuai wake wa kujieleza kiutamaduni. Taratibu na kanuni hizo zinaeleza kuhusu namna ya kuwasaidia wanaojihusisha na tasnia za utamaduni kupata rasilimali za kuendesha shughuli zao.

Pili, kutambua kuwa bidhaa za kiutamaduni ni za kipekee na tofauti na bidhaa nyingine za viwandani au zitokanazo na kilimo. Bidhaa za kiutamaduni zinabeba utambulisho wa jamii na biashara yake lazima iwe na taratibu tofauti. Hiki ni kipengele muhimu katika kusimamia uandaaji na usambazaji wa bidhaa na huduma za kiutamaduni ndani na nje ya nchi.

Tatu, nchi zilizoendelea kuzisaidia nchi zinazoendelea katika kulinda uanuwai wake wa kujieleza kiutamaduni kwa kutoa upendeleo maalum kwa bidhaa za kiutamaduni kutoka nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Ibara za Kumi na Nane na Kumi na tisa za Mkataba huu inaelezea kuhusu Mfuko Maalum. Mkataba huu umeunda Mfuko wa Kimataifa wa Uanuvi wa Utamaduni (*International Fund for Cultural Diversity*) kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Mkataba wenyewe. Nchi wanachama wa Mkataba huu zinaweza kuomba na kusaidiwa Mfuko huo kulingana na taratibu za uendeshwaji wake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22 hadi 24 zinaelezea juu ya vyombo vyaa maamuzi. Mkataba huu una vyombo viwili vikuu vyaa maamuzi, chombo cha juu kabisa ni Mkutano Mkuu wa wanachama wote na chombo cha pili ni Kamati ya Utendaji yenye wajumbe 18 ambaa watachaguliwa kutoka mionganii mwa wawakilishi wa Serikali za nchi wanachama. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wataongezeka kufikia 24 pindi nchi wanachama wa Mkataba zitakapofikia 50.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utatuvi wa migogoro, Ibara ya 25 ya Mkataba huu inaelezea utaratibu utakaofuatwa. Pakitokea mgogoro kati ya wanachama wa mkataba basi wahusika watajaribu kumaliza mgogoro huo kwa majadiliano na iwapo majadiliano yatashindikana basi wahusika wataomba usuluhishi wa mwanachama mwingine. Endapo usuluhishi huu hautatatuwa mgogoro basi wahusika watawasilisha mgogoro wao kwa Tume ya Upatanishi kama ilivyoelezwa katika Nyongeza ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, nia ni kumaliza migogoro kwa kupatana badala ya kufarakana. Hata hivyo, wakati wa kijiungu na Mkataba, mwanachama anaweza kueleza wazi iwapo hakubaliani na utaratibu wa kumaliza migogoro uliowekwa na Mkataba huu. Hii itakuwa na maana kuwa mwanachama huyo akiingia mgogoro na mwanachama mwingine atachukua hatua nje ya zile zilizoelezwa katika Mkataba.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kijiungu na Mkataba huu umeelezwa kwenye Ibara ya 26. Kila nchi mwanachama wa *UNESCO* anahitajika kuridhia Mkataba huu. Tanzania ni mwanachama wa *UNESCO* na ilishiriki katika mikutano ilivoandaa na kuitisha Mkataba husika. Kwa hiyo, haina budi kuuridhia kama ilivyokuwa wajibu kwa wanachama wote wa Mkataba huu. Ziko faida nyingi za kijiungu na Mkataba huu zikiwemo hizi zifuatazo:-

Kwanza Tanzania itaweza kushirikiana na nchi nyingine duniani kulinda utamaduni wake. Kwa mfano, wafanyabiashara wanaochukua sanaa za Tanzania kama vile michoro ya Tingatinga na vinyango vyaa Kimakonde na kuviuza kama sanaa za nchi nyingine au wale wanaouza sanaa za nchi nyingine zisizo na ubora kwa kutumia umaarufu wa sanaa za Tanzania wataweza kushughulikiwa kwa ufanisi zaidi kwa kutumia vipengele vyaa Mkataba huu.

Pili, Mkataba huu unatoa fursa ya kuchagua na kuchaguliwa kuongoza vyombo vya Kimataifa vinavyoundwa chini yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kujiunga na Mkataba huu, Ibara ya 26 inasema kuwa nchi wanachama wa *UNESCO* wanaweza kujiunga na Mkataba kwa kuridhia, kukubali, kuidhinisha au kupitisha kutegemea na matakwa ya Katiba zao. Aidha, chini ya Ibara ya 27, nchi ambazo sio wanachama wa *UNESCO*, zinaruhusiwa kujiunga kwa utaratibu wa “*accession*,” Tanzania ni mwanachama wa *UNESCO*. Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inataka Mikataba ya Kimataifa ijadiliwe na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo pia gharama ya kujiunga na Mkataba huu ambazo ni za aina mbili. Kwanza ni ile michango ya kila mwaka ambayo ni kiasi cha asilimia moja ya mchango wa mwaka wa Tanzania kwa *UNESCO* ambao ni Dola za Marekani 183 kwa mwaka. Gharama nyingine ni zile za utekelezaji wa Mkataba ndani ya nchi. Gharama hizi ni sehemu ya Bajeti ya Wizara na Mashirika yanayosimamia fani za utamaduni maana kazi zilizoainishwa na Mkataba huu ni sehemu ya programu za uendeshaji wa Sekta ya Utamaduni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara yangu ikiwa katika mchakato wa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kuridhia Mkataba huu, iliwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni na ushauri wao. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Maliasili na Utalii (Idara za Mambo ya Kale na Makumbusho ya Taifa) na Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Idara ya Nyaraka za Taifa), Ofisi ya Kanda ya *UNESCO* – Dar es Salaam, Tume ya Taifa ya *UNESCO*, Vyuo Vikuu, Asasi za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TaSUBA*), pamoja na wasanii binafsi wa fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wadau hawa walikuwa na maoni kama ifuatavyo:-

Kwanza Mkataba ni muhimu kwa Watanzania maana vipengele vyake vyote vinaonesha uhusiano uliopo kati ya maendeleo ya utamaduni na maendeleo ya nchi kwa jumla.

Pili, yaliyomo kwenye Mkataba huu hayana utata na yanafaa kuridhiwa. Isitoshe, michango inayotakiwa ni midogo ambayo Serikali ya Tanzania inaimudu. Kinachohitajika ni kubainisha maeneo yanayohitaji kulindwa na kukuzwa maana hii siyo shughuli ya kipindi maalumu tu bali ni ya kudumu. Mawazo yaliyomo kwenye Mkataba huu yamekuwepo kwa muda mrefu na sasa yamepata utaratibu wa kisheria wa

kuyasimamia Kimataifa. Tanzania haina budi kufikiria kwa makini namna itakavyosimamia urithi wake wa utamaduni na kunufaika na juhudhi hizi za Kimataifa.

Tatu, ubora wa Mkataba huu unajionyesha wenyewe. Tanzania inapaswa kuingiza maudhui ya Mkataba huu katika mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Mkataba huu, napenda kuchukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mkataba huu ulianza kutumika tarehe 18 Machi, 2007 kulingana na masharti yaliyomo katika Ibara ya 29 ya Mkataba. Hadi tarehe 15 Machi, 2011 nchi 116 zilikwishajiunga na Mkataba huu. Ilipofika Septemba 2, 2008 nchi 25 za Bara la Afrika zilikuwa zimekwishajiunga. Tanzania itakuwa mshirika wa Mkataba huu miezi mitatu baada ya kuwasilisha hati za kuridhiwa kwa Mkataba kwa Mkurugenzi Mkuu wa *UNESCO*. Hata hivyo, utekelezaji Kitaifa utaanza mara tu baada ya Mkataba kuridhiwa na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mikataba ya Kimataifa ya aina hii inapaswa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA**, mwaka 2005 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba unaohusu kulindwa na kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni;

**NA KWA KUWA**, nia na madhumuni ya Mkataba ni kulinda na kuendeleza Uanuai wa kujieleza Kiutamaduni duniani ili kuzuia baadhi ya tamaduni kumezwa au kukandamizwa na tamaduni nyingine kutoptana na nguvu za kiuchumi au kisiasa;

**NA KWA KUWA**, Mkataba huu unalenga kuzisaidia nchi wanachama kulinda na kunufaika na tamaduni zake pasipo kunyanyaswa au kubaguliwa kwa kujielezea kiutamaduni kupitia ubunifu wa watu au makundi ya watu kwa njia mbalimbali kama vile hadithi, sauti, muziki, picha, michoro, filamu, sanamu, kusuka, kudarizi, ngoma, maigizo na vitabu. Vile vile njia hizi za kujieleza huzaa bidhaa na huduma mbalimbali za kiutamaduni ambazo ni za kipekee na kwa upande mwingine ni utambulisho wa jamii husika;

**NA KWA KUWA**, kwa kuridhia Mkataba huu Tanzania itafaidika kwa kuweza kushirikiana na nchi nyingine duniani ambazo ni wanachama kulinda utamaduni wake, kuomba na kusaidiwa kutoka kwenye Mfuko Maalum uliououndwa chini ya Mkataba huu kwa ajili ya kulinda na kuendeleza tasnia za utamaduni wake pamoja na fursa ya kuchagua na kuchaguliwa kuongoza vyombo vya Kimataifa vinavyoundwa chini yake; na

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutoptana na kuwepo kwa Mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wake wa Tat, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka

2005 yaani “*the Convention on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions.*”

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. AGNES E. HOKORORO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ndio mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge lako Tukufu, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mtwara ambao kwa umoja wao walinipendekeza na hatimaye kunichagua katika vikao husika vyta Kikatiba kuwa Mbunge wao kuwawakilisha. Naamini nitaifanya kazi hiyo kama ambavyo wamenitura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, napenda sasa kusoma maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*), kuhusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuwi wa Kujieleza Kiutamaduni, *Convention on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions.*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, Kamati inapenda kutoa salamu za pole kwa wananchi walioathirika na kupoteza ndugu zao katika majanga mbalimbali yaliyotokea mwanzoni mwa mwaka huu. Majanga hayo ni pamoja na milipuko ya mabomu ya Gongo la Mboto, ajali ya basi iliyowahusisha wasanii wetu wa Bendi ya *Five Stars* na ajali nyingine nyingi za mabasi zilizopoteza maisha ya Watanzania. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilipata fursa ya kusikiliza madhumuni ya Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni, kuhusu Kukuzwa kwa Uanuwi wa Kujieleza Kiutamaduni uliowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, siku ya tarehe 29 Machi, 2011 na tarehe 30 Machi, 2011 katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kila jamii hujieleza kiutamaduni kuitia ubunifu wa watu au makundi ya watu kwa njia mbalimbali kama vile hadithi, sauti, muziki, picha, michoro, filamu, sanamu, kusuka, kudarizi, ngoma, maigizo na vitabu. Njia hizi za kujieleza huzaa bidhaa na huduma mbalimbali za kiutamaduni ambazo ni za kipekee na utambulisho wa jamii husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *UNESCO* unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuwi wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 (*Convention on the Protection and*

*Promotion of the Diversity of Cultural Expressions*), umetokana na athari za kukua na kuenea kwa utandawazi duniani na falsafa zake za kutaka dunia iwe yenyé mfano mmoja ukijumuisha tamaduni zake. Hali hii iliyapa mataifa yenyé nguvu kiuchumi duniani fursa ya kueneza tamaduni zao huku tamaduni za mataifa machanga na yanayoendelea zikidumazwa na kutishiwa kumezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo UNESCO ilipitisha Mkataba unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni kwenye Mkutano wake Mkuu wa 33 uliofanyika Oktoba, 2005 huko Paris.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Mkataba huu ni kulinda na kukuza Uanuai wa kujieleza kiutamaduni, kutengeneza mazingira mazuri kwa tamaduni, kustawi na kuingiliana pasipo mikwaruzano, kukuza heshima kwa Uanuai wa kujieleza kiutamaduni na kufanya thamani yake itambulike kijamii, Kitaifa na Kimataifa. Pia kuhamasisha mwingiliano miiongoni mwa tamaduni mbalimbali huku ikizingatiwa kuwa mabadilishano hayo ya kiutamaduni duniani yana usawa yanajenga kuheshimiana na amani, kusisitiza umuhimu wa utamaduni katika maendeleo ya kiuchumi hasa katika nchi zinazoendelea. Lingine ni kutambua sifa bainifu za kipekee za shughuli bidhaa na huduma za kiutamaduni kama utambulisho muhimu wa Taifa mahususi na kutoa fursa ya kushirikiana na kusaidia Kimataifa katika ulinzi na ukuzaji wa uanuai wa kujieleza kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali ya kuleta Azimio la kuridhia mkataba huu na hivyo inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuweza kuwasilisha Azimio hili lenye lengo la kulinda na kuendeleza Uanuai wa kujieleza kiutamaduni duniani ili kuzuia baadhi ya tamaduni kukandamizwa na hatimaye kumezwa na tamaduni nydingine.

Vilevile katika Ibara ya 7(1)(a) ya Mkataba huu Kamati inatoa pongozi kwa kuwa suala la jinsia limezingatiwa pamoja na makundi mengine mbalimbali katika jamii yamezingatiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha vyombo vya habari hapa nchini vinashughulikia zaidi kusambaza na kutangaza tamaduni za nchi yetu na si zile za kigeni kama ilivyo sasa. Hili linaweza kutekelezwa kwa kuvipa vipaumbele vikundi mbalimbali vya ngoma, sanaa pamoja na kuwapa moyo wasanii wale wanaoimba nyimbo mbalimbali zenye asili ya Kitanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mkataba huu unatekelezwa Kamati inashauri Serikali kuangalia sheria mbalimbali tulizonazo kwa sasa kama zinaweza kukidhi mawanda ya mkataba huu na kama zitakuwa zinakinzana ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 18 na 19 ya mkataba huu umeunda mfuko wa Uanuai wa Utamaduni (*International Fund for Cultural Diversity*) kwa ajili ya kusaidia

utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Mkataba wenyewe. Aidha, nchi wanachama wa mkataba huu wanaweza kuomba na kusaidiwa na mfuko huu kulingana na utaratibu wa uendeshwaji wake. Kamati inashauri Serikali kuboresha mfuko wa utamaduni na kuona kwa namna gani tunaweza kunufaika na kutokana na mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuwatambua wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Azimio hili kama wafuatavyo, wa kwanza ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumper Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashidi, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee na Mheshimiwa Livingstone Lusinde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia wa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati katika kutekeleza majukumu yake pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John kwa kuhudumia katika kipindi hiki chote tulipokuwa tukifanya kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani sana za dhati kwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu Ndugu Seth Kamhanda na watendaji wote na timu nzima ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kundaa Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile shukrani za pekee ziwaendee wadau mbalimbali walioshiriki kuboresha Azimio hili wadau hao ni pamoja na Chuo Kikuu cha Mzumbe, Makumbusho ya Taifa, *Lawyers Environmental Action Team* na wadau wote walioshiriki kutoa michango yao kwa namna mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio, asante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana, sasa nimuite msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, kuhusu Azimio hili. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, asante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa *UNESCO* wa Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni yaani *Conversion on the Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expressions.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mimi naomba nitume rambirambi zangu kama wenzangu kwa bendi ya *Five Star Taarab* ambayo ilitutoka hivi karibuni na pia kupitia Bunge lako Tukufu natoa rambirambi zangu kwa vifo vyta wafanyabiashara wawili maarufu wa Mjini Mbeya Marehemu Waziri na Marehemu Jimmy ambao wameacha pengo kubwa jijini Mbeya kwani walikuwa ni mfano kuigwa kwa vijana wa pale jijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Azimio la Kuridhia Mkataba huu ni mazuri sana kama yalivyoolezwa katika Ibara ya kwanza na ya pili ya Mkataba. Jambo la msingi ambalo Kambi ya Upinzani inasisitiza kwa Serikali ni kwamba imejiandaa vipi kiutekelezaji ili yale yote yaliyomo kwenye Mkataba yaweze kutekelezeka kwa manufaa kwa Watanzania na nchi kwa ujumla? Kambi ya Upinzani inatoa angalizo hilo kwa ukweli kwamba Tanzania imekuwa ni bingwa wa kuridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa lakini inashindwa kutengeneza mazingira ambayo yataifanya mikataba hiyo kuwa na manufaa kwa Taifa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano suala la uanzishaji wa sheria ya haki miliki yaani *copyright* ambayo kimsingi uanzishwaji wake ultokana na msukumo wa Shirika la Kibiashara la Kimataifa (*World Trade Organization - WTO*), ambalo ilizitaka nchi zote ambazo ni wanachama wake kuwa na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikubali kuwa na sheria hiyo ya haki miliki kwa kuwa yalikuwa ni matakwa ya *WTO* lakini ukweli ni kuwa hatukuwa tayari kama nchi kuwa na sheria hiyo na hilo limesababisha hadi leo pamoja na kuwa sheria hiyo ya hati miliki bado haina tija kwa walengwa ambao ni wasanii wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliowazi kuwa Tanzania kama nchi imekumbwa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wake hivyo kutengeneza mazingira mazuri yatakayoutafanya mkataba huu kutekelezeka bila matatizo maana yake ni kutengeneza ajira kupitia sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, haya yote yatafikiwa ikiwa Serikali itatambua na kuheshimu michango inayotolewa katika sanaa na utamaduni kuwa ni sehemu muhimu ya kibiashara yenye nafasi nzuri ya kutoa ajira na kuchangia katika Pato la Taifa badala ya kuonekana kama ni kitu cha kutoa burudani peke yake.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tunatakiwa tuwe na mikakati ya kulinda na kukuza Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni ili kuifanya thamani yake itambulikwe kijamii, Kitaifa na Kimataifa. Katika hili wenzetu wa nchi za Magharibi mfano Ufaransa, napenda kutoa mifano kwa sababu Ufaransa na Marekani ndiyo vinara wa *UNESCO*

wamefanikiwa sana kwani kwa mujibu wa sheria zao asilimia 80 ya utamaduni unaotangazwa katika vyombo vyao habari ni ule wa kwao. Sasa sisi katika mazingira ya sheria kama Ufaransa tunajipenyeza vipi ili tamaduni zetu zijulikane kwao kwani wao wakija kwetu hawana pingamizi lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na kuridhia mkataba huu ila inasisitiza tena Serikali kuzingatia yale yote ambayo tumekwishayasema hapo awali ili mkataba huu uwe na tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha, asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa mnaruhusiwa kujadili Azimio hili, mpaka sasa kuna majina mangapi mimi sijapata, naona walikuwa wanaendela *ku-comply* wengine siwaoni hapa ingawa wameomba, Mheshimiwa Capt. John Komba, sijui yupo atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, na mimi ingawa ni mmoja wa miongoni wa wajumbe wa Kamati hii lakini pia naomba nichangie kidogo kuhusu Azimio hili ambalo moja kwa moja naliunga mkono ili Wabunge tuweze kuridhia na sisi tukawa mmoja wa wale amba wameridhia katika dunia hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yetu ya sasa hivi sisi ni mabingwa kabisa wa kuiga mambo, sasa hivi tunaiga mpaka tuneshau utamaduni wetu wote, nikupe hii zamani ulikuwa unaweza kusikia mtangazaji labda wa redio Tanzania anasema hii ni taarifa ya habari kutoka Redio Tanzania Dar es Salaam msomaji John Komba, habari kwa ufupi. Sasa hivi unasikia hii ni *TBC* habari Komba na wewe amemaliza hapa sasa unaelewa nini hapa hii ni *TBC* habari Komba na wewe sasa huku ni kuiga ambako kwa kweli maadili yetu ya nje tunaiga vitu vya nje bila sababu. (*Makofi*)

Leo hii ukiangalia kwenye *TV* zetu zile habari na ama zile hadithi za zamani ambazo zilikuwa zinasimuliwa na watoto wanapenda kusikiliza na wanajua siku fulani ni siku ya kumsikiliza bibi au mama na mwana na hadithi za Ua jekundu, hadithi za nini leo hakuna. Leo utakuta habari ambayo ipo pale ni *my diary* kama alivyosema msemajji mmoja mchana matokeo yake mtu anaeleza ufuska wake badala ya kueleza ushujaa wa Watanzania ama ushujaa wa Afrika wa hapo nyuma na tukuze namna gani.

Kule kwetu Ruvuma kule mtu ukifanya kitendo cha hovyo, watu walikuwa wanakaa kwenye vikundi vya ngoma halafu wanatunga nyimbo kama wewe umefumaniwa kwa mfano basi wanatunga nyimbo ya kufumaniwa fulani unaimbwaa kijiji kwa kijiji kwa hiyo kitendo kile kinalaaniwa na fumanizi zinapungua. Leo hakuna, jambo hili limepotea leo kila ukimkuta mtoto hakuna nyimbo hizo anakuambia nimeenda *club*, hata kijiji kuna *club*, *club* ya nini labda *disco* ama *club* ya starehe au *club* ya nini. (*Makofi*)

Kwa hiyo, zile tamaduni za zamani zimepotea hata kwenye usanifu wa Kiswahili utakuta mtu anajitahidi, mtangazaji anajitahidi kabisa kukwepa Kiswahili na kuzungumza kiingereza *slang* cha Kimarekani hata Mmarekani mwenyewe anashangaa huyu anaongea nini unamwambia anaongea cha kwako anasema hiki sio cha kwangu hiki ni kitu kingine. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, utakuta anajitahidi kukwepa Kiswahili lakini anaweka Us wahili, Uingereza ama Umarekani ambao sijui unaitwa *Kiswangilishi* au namna gani matokeo yake utamaduni wa lugha ya Kiswahili unapotea. Kwa hiyo, mimi nilikuwa na michango hii ambayo tukiweza kurudisha nyimbo hizo za zamani, tukiweza kurudisha utamaduni wetu wa kutangaza kwenye redio zetu, tukiweza kurusha vipindi vyta zamani ambavyo vilikuwa vinamjenga mtoto kuanzia mtoto mpaka anakuwa mkubwa kwa kweli Azimio hili litakuwa limetusaidia sana katika kujenga maadili ya Kiafrika na Kitanzania kwa ujumla. Kwa haya, machache naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Azimio la Elimu Sayansi, Utamaduni lakini kabla ya kuchangia napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mgogoni kwa namna ambavyo waliweza kunipa ushirikiano wao ili niweze kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile pamoja na kuunga mkono Azimio hili niseme kwamba Tanzania inawajibu wa kulinda, kuheshimu na kuhifadhi utamaduni wake wa asili na endapo Watanzania tutakuwa na msimamo wa kulinda, kuheshimu na kuhifadhi utamaduni wetu wa asili basi hakuna nchi yoyote duniani ambayo haitatupa kipaumbele katika kulinda heshima na utamaduni wa Taifa letu. (*Makofi*)

Hata hivyo nimeona kwamba kuna kasoro ambazo zinatupelekea Watanzania kuiga tamaduni ambazo si stahili yetu kwa mfano leo unapoangalia kwenye luninga unaweza ukamuona mwanamama wa Tanzania akitumiwa kama chachu na kivutio katika mambo ya kuendeleza tamaduni za ngoma Tanzania, jambo ambalo wanaume wanaoendeleza bendi zile wao hawawezi kuva nguo zile ambazo wanawavisha akinamama. (*Makofi*)

Sasa niseme kwamba huku si kulinda maadili ya mwanamke wa Tanzania bali ni kuvunja heshima ya mwanamke wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tumesema kwamba kuna rasilimali nyingi ambazo zinaashiria kulinda tamaduni zetu kwa mfano kuna vijana wetu ambao ni wachongaji wa vinyago na tumesema kwamba vinyago hivi havichukuliwi kama ni sehemu ya rasilimali zinazotolewa na vijana wetu wa Tanzania au wazee wetu wa Tanzania, vinapelekwa nchi nyingine kulinda heshima na hifadhi ya nchi nyingine badala ya kubakia kwetu Tanzania, jambo kama hili ni kuwadhoofisha vijana hao au wachongaji hao au Watanzania hao na ni kupoteza heshima ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu tumesema kwamba kuna watu wetu ambao ni watungaji ama wa riwaya, vitabu vya mashairi, vitabu vya tenzi au vitabu vya ngonjera

lakini niseme kwamba hatuna uhifadhi wa dhati kama alivyosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba tunasema lakini hatutekelezi. (*Makofi*)

Sasa mimi naomba kwamba wale ambao wametunga vitabu vyao kwa njia moja au nyingine basi rasilimali zile ziwe zinapatiwa hati miliki ili mtu wa Taifa lingine asiweze kuichukua rasilimali ile akaitumia kama ni fani inayotokana na nchi yake.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba nakubaliana na Azimio hili na nasema kwamba tuna wajibu wa kuliunga mkono lakini hata hivyo tuliunge mkono kwa matendo na utekelezaji, tusiliunge mkono kwa maneno matupu ikawa likishasemwa basi libakie kwenye vitabu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, asante na mimi pia napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii pamoja na kwamba nilisoma maoni ya Kamati lakini ninayo mambo mawili ya kuongeza kufuatia azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa pamoja tukaona upo umuhimu wa kuridhia kwa mkataba huu ambao sisi kama Watanzania utatusaidia kupata utambuzi wetu kama Watanzania kutokana na utamaduni tulionao.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna mambo ya kiutamaduni ambayo tukiyaendeleza na kuyalinda yanaweza yakatutambulisha sehemu yoyote duniani. Kwa mfano, katika vitu ambavyo vimesemwa katika mkataba huu ni pamoja na sanamu na vinyago na mimi naomba hapa niongelee vinyago vya Kimakonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vinyago vya Kimakonde vinajulikana kama vinyago vya Kimakonde, lakini kutokana na uwezo wa Mataifa mengine kazi hii sasa inafanywa na nchi nyingine za Afrika pia wamekuwa wakitumia taaluma yao kutengeneza vinyago na kuviuza kama vinyago vya Kimakonde japokuwa wakati mwengine hawatumii miti ambayo ni ya Kimakonde kwa sababu Wamakonde wamekuwa wakichonga vinyago hivi kwa mti wa Mpingo kwa hiyo, ule uzuri wake unapotea. Lakini vinyago hivi vinavyokwenda kuuzwa katika nchi mbalimbali bado vinatangazwa kuwa ni vinyago vya Tanzania na ni vya Kimakonde. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naamini tukiridhia mkataba huu na kulinda sehemu hii kama sehemu ya utamaduni wetu wa Kitanzania tutawenza kufanya vizuri zaidi na tutawenza kuepusha wafanyabiashara wa nchi nyingine kutumia sehemu yetu hii ya utamaduni wa vinyago vya Kimakonde kwa jina lao la nchi zao badala ya sisi Watanzania ambapo Wamakonde wanatoka kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo mimi naamini ni muhimu tukailinda ni sehemu ya mavazi. Kwa muda mrefu sana nchi yetu hatuna vazi la Kitaifa, naamini kama ambavyo wote tunajua kwamba tuna makabila mengi na sisi Watanzania tuna utamaduni wetu, hatuna utamaduni wa kuvaas suti, ni utamaduni wa kizungu, lakini

tunayo mavazi ambayo sisi au mtu yejote yule atakapotoka nje ya mipaka ya Tanzania akisimama anatakiwa atambulike kama Mtanzania na hilo haliwezi kupatikana bila kuwa na vazi la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma wakati tunasoma wengine tukiwa wadogo wakati Marehemu Baba wa Taifa alikuwa anafanya shughuli za harakati za kuikombua nchi hii kuna picha tumeziona Baba wa Taifa alikuwa anavaa mgolole. Tulivyokuwa tunakuwa tulikuwa tunafikiria kwamba labda Tanzania tungkuwa na vazi hilo kama sehemu ya utamaduni lakini kama utambulisho wa Mtanzania katika nchi nyingine. Lakini tumeona vazi hilo linavaliwa na nchi nyingine sasa hatuwezi kujuu sasa hivi tukilichukua je, tutaonekana sisi tumeiga kutoka kwao na kumbe labda wao waliiga kutoka kwetu. Vazi hili linavaliwa katika makabila mengi, Wamasai wanalivaa na makabila mengi katika nchi hii wanalivaa hilo vazi. Ni vizuri sasa tukachukua hatua madhubuti za kulinda utamaduni huu kwa sababu kwa namna ya pekee sana itakuwa inatutambulisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingine ukienda ukikutana na mwanamama yejote kama ni katika uwanja wa ndege utagundua kwa mara moja na kwa haraka sana kwamba huyu ni Mnaigeria na ndiyo maana hata Mhindi akija Tanzania utajua huyu ni Mhindi, hii ni kutokana na vazi lake alilovaa. Kwa hiyo, ipo haja na sisi tukalinda utamaduni wetu kwa kuwa ni utambulisho muhimu sana kama Watanzania popote duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu mwengine wa kuridhia mkataba huu utatusaidia sana kuhuisha utamaduni wa asili kama vile nyimbo za mafundisho. Kwa mfano, huko nyuma kulikuwa na nyimbo za asili ambazo hata ukifungua redio unajua tu kabisa kwamba hii ni nyimbo iliyoiimbwa na Mzee Morris Nyunyusa lakini sasa hivi huwezi kuipata. Kwa hiyo, mimi naamini hata hizi nyimbo za asili ni vizuri kwa kupitia mkataba huu tukazilinda ili tuweze kulinda utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye suala hili la mkataba huu wa UNESCO.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuona umuhimu wa kuleta mkataba huu Bungeni ili tuweze kuuridhia. (*Makofi*)

Pamoja na pongezi hizo mkataba huu inaonekana uliingiwa muda mrefu yaani mwaka 2005 kule Paris - Ufaransa, ni takribani zaidi ya miaka mitano leo ndiyo unaletwa Bungeni kwa ajili ya kuuridhia kiasi ambacho ungeweza kupoteza umuhimu wake kwa sababu kitu ambacho ni muhimu si busara kukaa muda namna hii bila kuridhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkataba huu pia zaidi unazungumzia kulinda na kukuza tamaduni zetu. Lakini tamaduni zetu zipo ambazo kwa kiasi kikubwa zilishakandamizwa na kuathirika na nyingine hata kufa kutokana na hii nguvu ya Sayansi na Teknolojia kutoka kwenye Mataifa makubwa. Sasa hizi tamaduni ambazo zimeshakufa nadhani mkataba huu pia ulitakiwa uone umuhimu wa suala la kufufua kwa sababu kulinda ni kwamba tulinde kitu ambacho kipo na kukikuza. Sasa hizi tamaduni ambazo zilishakufa zinatakiwa zifufuliwe kwa sababu zilikuwa ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano utaona utamaduni wetu leo huu wa njia ya muziki kwa zamani tulikuwa tunaona wanamuziki wanaanza kuchonga magitaa yale ya kienyeji wanapiga wanakuja na *melody* nzuri sana na tulikuwa tunatambulishwa na utamaduni huo, lakini leo utakuta hata kwaya za dini hatuoni mtu anapiga gitaa pale tunasikiliza nyimbo tu. Utakuta vikundi vingine sasa hivi vinaibuka hatuoni watu wanapiga magitaa ila nashukuru juzi kulikuwa na *Kili Music Award* walitambua umuhimu na mchango wa mwanamuziki mmoja anaitwa Said Mabera kwa kucharaza gitaa na mimi nampongeza sana kupitia Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo siyo kuridhia mikataba kama wenzangu walivyosema, mikataba mingi tunairidhia lakini dhamira ya dhati wakati mwingine inatuangusha katika kutekeleza mikataba hii. Kule Wilayani tuna Afisa Utamaduni na Michezo lakini utakuta zaidi wanaelekea kwenye michezo zaidi, kwenye utamaduni wanajisahau na wao ukiwaliza kwa nini suala la utamaduni halitiliwi mkazo kwenye vijiji, kata, tarafa na Wilaya wanasema hawana fedha.

Mheshimiwa Spika, nashauri huu mfuko maalum ambao umeingia kwenye mkataba ushuke mpaka kule vijijini maana yake mifuko mingi imekuwa ni mjini Dar es Salaam na kumekuwa na watu wengine ambao wakishasikia kuna fedha na mifuko ndipo huanza kuunda vikundi haraka haraka vya utamaduni ili waweze kuchukua fedha hizi na leo wamesikia kuna mfuko maalum humu Bungeni tusishangae kesho tukaona vikundi vinaanza kusajiliwa. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, fedha hizi zishuke ziende vijijini na unakuta sisi Wabunge mara nyingi tunapenda sana kuibua na kuendeleza masuala ya ngoma kule vijijini. Kwa mfano, pale Jimboni kwangu katika kata ya Kisorya kuna kikundi cha ngoma cha Garikubwa na pale Busambara kuna Kiujabu lakini wakati mwingine wanakosa hata ngoma, imebaki sasa ni kazi ya Wabunge kufadhili vikundi hivi kuhakikisha kwamba tamaduni zetu hazipotei. (*Makofi*)

Wabunge tumekuwa na maeneo mengi sana ya kufadhili, naomba Mheshimiwa Waziri kama tuna nia ya dhati na tumeridhia mkataba huu na na kuunga mkono fedha hizi zije zishuke ziende mpaka kule vijijini wenzetu Wasukuma kule walikuwa na Mbina na hata kule kwetu zilikuwepo wakati wa mavuno watu wanacheza ngoma ambazo ndizo tamaduni zetu lakini wakati mwingine walikuwa wanakatishwa tamaa kwamba ni wakati ambapo wanapika pombe kwa hiyo, wanatumia chakula kwa hiyo, wanakaribisha njaa, lakini ilikuwa ni sehemu ya udumisha tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, suala hili la utandawazi limeingia kwa nguvu sana katika kukandamiza na kuhakikisha tamaduni zetu hazifiki mbali, naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na maelezo waliyoyatoa juu ya kuchukua hata hatua nyingine za kisheria naomba kuwe na mkakati maalum ambao utasaidia hawa wenzetu ambao wanatumia muda wao mwingi kufanya muziki, ngoma na maonesho ili waweze kusaidiwa na mikakati ya nia njema ambayo itakuwa inatoka kwenye Wizara yako. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwenye sehemu ya madhumuni niliona kuna dhumuni moja pale mwishoni nadhani ni la saba, naomba kwa ruhusa yako nilisome; ni kwamba “madhumuni ya mkataba huu ni kutoa fursa ya kushirikiana na kusaidiana Kimataifa katika ulinzi na ukuzaji wa uanuai wa kujieleza kiutamaduni.”

Kwa hiyo, nadhani dhumuni hili na lenyewe liangaliwe kwa kina kwa sababu linahusisha suala la kushirikiana katika ulinzi, sasa isije ikawa tunaridhia tunadhani ni katika kulinda na kukuza hizi tamaduni lakini kuna suala hili la ulinzi ambalo halikuelezwa kwa kina ni namna gani tutakavyoshirikiana katika mkataba huu juu ya hii fursa ya ulinzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema nampongeza Waziri kwa kuleta mkataba kuridhiwa kwa muda muafaka na nimalizie pia na mimi kwa hawa wasanii wa *Five Stars* ambao walipoteza maisha na mimi nawapeni pole. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Azimio hili la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni kuhusu kulindwa na kukuzwa kwa anuai kwa kujieleza kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, nimevutika na mimi nichangie azimio hili baada ya kuona maudhui na hasa maudhui mawili ambayo ni ya mkataba kulenga kulinda nchi wanachama kuhusu utambulisho wa jamii husika. Kwa hili kwanza ningefurahi sana kwa sababu kwanza ni mategemeo yangu kwamba Azimio hili Tanzania imesaini kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ikiwa ni hivyo na upande wa pili wa Jamhuri ziko tamaduni ambazo zinapaswa kuenziwa kama ni utambulisho mkuu wa Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Afrika nzima zipo tamaduni kwa mfano katika Azimio hili yametajwa mambo mengi kama hadithi, muziki, ngoma, michoro na maigizo. Katika hili suala la ngoma makabila mengi au nchi nyingi za Afrika yanalingana lakini uko mchezo mmoja tuseme ni ngoma haulingani Afrika nzima, hakuna pahali hata pamoja isipokuwa Tanzania na Tanzania yenyewe ni Pemba na Pemba yenyewe ni wapi?

**MBUNGE FULANI:** Ni Kiwani!

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, tutaendelea! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchezo wa ng'ombe ni utambulisho na utamaduni mkubwa kwa Tanzania, bahati mbaya jamii hii ya watu wa Pujini Pemba hivi sasa mchezo huu tumeudharau, ikiwa leo Tanzania tunapitisha Azimio hili, tuna *ratify* Azimio hili leo na mimi najisikia faraja kwamba sasa mchezo wa ng'ombe amba ni utamaduni mkubwa hakuna nchi yoyote Afrika na katika dunia ni nchi mbili tu nyingine ambayo *style* yake tofauti ni *Portuguese* na *Spain*, leo ikiwa tunaridhia Azimio hili nakuhitaji Mheshimiwa Waziri tuone mchezo wa ng'ombe kama utambulisho wa utamaduni wa Tanzania amba hakuna popote Afrika utarudi katika anga zetu hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchezo huu utailetea fahari kubwa sana Tanzania kwa sababu *style* yake ni tofauti na hiyo ya *Spain* na ikiwa Azimio hili moja katika maudhui yake ambayo Mheshimiwa Waziri ameyataja ni kwamba Ibara ya 18 na 19 ya Azimio hili ni kwamba Mfuko wa Kimatifa *for cultural diversity* tunaomba sasa tukifanikisha huo Mfuko wa Kimataifa uende pande zote za Jamhuri kwa sababu kule kuna tamaduni nyingi.

Mheshimiwa Spika, mchezo wa Msewe ni utambulisho mkubwa sana na Kiumbizi ambacho inapatikana Makunduchi Unguja na tena kule Pujini Pemba na Mahumbwa. Leo ikiwa michezo hii ambayo ina tofauti kubwa sana na tamaduni za michezo mingi ya Tanzania Bara ikiwa tutaikuza tunaweza kupata faida kubwa kiuchumi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba kwamba Mheshimiwa Waziri kwamba mimi nitaliunga mkono vizuri sana Azimio hili leo na wewe uwe shahidi siku moja tukuchukue tukakae pale Tibirizi uone mchezo wa ng'ombe na baadaye tuuneze duniani. (*Makofi*)

Mimi naelewa katika hili la kushirikiana Kimataifa kuna *cultural festivals* ambazo zinafanyika Texas. Naomba Mheshimiwa Waziri ulifuatilie na wewe ulisoma kule Texas na wale wana tamaduni za michezo na wanaomba na wanapeleka hata tiketi na kila *facility* wanatoa ili wapate kundi la watu wa utamaduni fulani kutoka Tanzania wakaoneshe kule Texas, Marekani. Kwa maana hiyo Azimio hili naomba tuliunge mkono kwa sababu wako watu wana hivi vipaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vipaji vingine ambavyo vinapatikana kule Kisiwani Pemba, kuna Kibati. Hapa Dar es Salaam, yuko kijana mmoja kwa umaarufu anajiita Dokta Issa, tena anakutungia nyimbo za papo kwa papo na akakusema na akakusifu hasa katika shughuli kama kampeni, kama harusi, na tena kwa lugha ya Kiingereza. Lakini hana uwezo wa kwenda nje kujitangaza, yupo kijana mwengine vilevile Pemba tunamwita Maalim Tabu na yeye vilevile akipata uwezo na kikundi chake utamaduni huu wa Kibati utaenea.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja kubwa Wizara yako kuitia wafadhili mbalimbali inashughulikia ma-miss zaidi kuliko tamaduni nyingine. Hili ni kosa, vipaji

tunavyo, watu tunao, wasishughulikie ma-miss tu waka-*finance* na wale watu tutafute vipaji, wako wa kila aina Kaskazini Unguja wako, Makunduchi wako, Pemba wako kwa hiyo Azimio hili tukilipitisha leo na tunalipitisha ni kwamba tuisahau Makamu wa Rais, Marehemu Dkt. Omari Ali Juma walikuwa wakikuburudisheni sana kwa *Maulid* ya Homu ambayo anachukua vikundi vilevile. Leo tumesahau, tumeviacha kwa hiyo, tuvitumie vikundi hivi na sisi tufaidike na vitaitangaza Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninaomba kuunga mkono azimio hili. (*Makofi*)

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Nami napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Azimio hili. Kwanza na mimi ninapenda niseme kwamba Azimio hili ni zuri nami ninaliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningependa kuongelea kuhusu wasanii mbalimbali ambao wanakwenda kuwakilisha nchi yetu katika Mataifa mbalimbali. Wapo wasanii ambao wanakwenda kwenye mashindano mbalimbali nje ya nchi, wengine wanaleta tuzo lakini unakuta Taifa haliwapi heshima ya aina fulani kwa sababu wale wanapotuwakilisha nje na wakaja na tuzo, licha ya kwamba wao labda wanaweza kupata kipato lakini pia wanajenga heshima kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Kwa mfano, wakati fulani kulikuwa na mchakato wa kutunga Wimbo wa Afrika Mashariki. Sisi katika mkoa wetu wa Kagera tunaye kijana ambaye alishiriki katika mchakato huo na aliweza kwenda mpaka akawa mshindani wa pili. Naamini inawezekana kweli katika mchakato huu labda walikuwa wanapewa marupurupu mbalimbali kidogo au ya kuwafaa. Lakini je, Taifa kama Taifa limeweza kuwatambua vipi Watanzania ambao waliweza kushiriki katika ushindani wa kutafuta wimbo huu japokuwa haujatoka, lakini waliweza kutumia nguvu zao, taaluma zao na wakaweza kabisa kufikia katika kiwango hicho? Ingekuwa vyema wasanii kama hawa wangkuwa wanatuzwa siyo lazima kutuzwa kwa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipindi fulani nilikuwa naona kwamba kwa mfano wachezaji wa *Taifa Stars* walikuwa wanaitwa kwenye Bunge wanahehimiwa na wanapongezwa. Mimi naamini kwamba watu kama hawa ambao wanalijengea heshima Taifa pia wangeweza kupewa tuzo kama hizo ili kuwajengea moyo na kuwapa vipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona katika maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ameweza kusema waziwazi kwamba ni vyema kabisa tukawa tunawapa vipaumbele vijana wetu au wasanii mbalimbali hata kama ni wacheza ngoma ili waweze kupata nguvu ya kuendelea katika kutangaza Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ningependa kuongelea kuhusu mavazi. Kumekuwa na mjadala kwamba vijana wetu wanavaa mavazi yasiyoweza kutambulisha Taifa, lakini mimi ninafikiri jambo hili tumelirithisha hata katika familia zetu kwamba maadili wakati mwingine yanaanza ndani ya familia. Unaweza kuona ni jinsi gani mtoto wa kike au hata wavulana wanayo mavazi yao wanavaa suruali wanaita “kata K” yaani anatembea mpaka

hata nguo za ndani zinaonekana lakini anapita mbele ya baba kwa sababu sasa hivi wazazi ndani ya familia tumejiona tuna usomi, tumejiona tuna uwezo na tunaishi kiuzungu, uzungu kwa hiyo, watoto wanapita mbele yetu hatuwakemei na wakati mwingine hatuwarudi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Taifa linakwenda hivyo kuanzia ngazi ya familia mpaka unafika wakati huu sasa inakuwa ni ngumu kuthibitika kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara kwamba kuna tamaduni nyingine zimekuwa. Tamaduni nyingine zimekuwa kwa kweli Taifa litapaswa kufanya kazi kubwa liweze kuzifufua ikiwa ni pamoja na tamaduni za mavazi ambazo kwa kweli wakati mwingine zinatia aibu Taifa.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tuunge mkono na mimi ninaunga mkono Azimio hili lakini kwa kuvisisitiza Serikali kwamba basi ifanye utekelezaji, tuhakikishe kwamba mambo yote tunayoongea hapa Serikali iyachukulie hatua na iyaweke katika mchakato mzuri wa kuyatekeleza ili tuone kama Taifa hili linaweza kuепuka majanga mengine ambayo mimi ninayaita majanga kama ya kwenda utupu, kufanya mambo mengine ambayo kwa kweli yanalidhalilisha Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kufanya kazi kubwa na hata mengine tunaweza kuyaweka hata katika mitaala ya shule, tunaanza na watoto wetu kuanzia shule za awali mpaka shule za msingi mpaka sekondari unakuta watoto wanajijenga mapema au wanajengwa na nchi yao kwamba kuvala hivi, kutembea hivi siyo kitu kizuri. Kwa hiyo, watoto wanaanza pamoja na familia zao, wazazi wao lakini hata walimu shulenii wanawarekebisha, kama walimu wanawarekebisha basi na wazazi wenyewe wawakubalie.

Sasa hivi nilikuwa naangalia kwenye televisheni kuna tangazo moja la Haki Elimu ambapo mtoto anafukuzwa shule kwa sababu alikuwa na simu shulenii na mzazi anachachamaa kabisa. Hii wanatupa taarifa kwamba ndivyo tulivyo ndani ya familia zetu kwamba mwalimu anapomkemea mtoto kuhusu tabia yake wewe mzazi unakuja juu kwa sababu una uwezo wa kumnumulia mtoto simu, basi mtoto na ye ye anabenua mdomo anawaambia walimu wengine bwana wanataka *u-head mistress* ni kwa sababu sisi tunakubaliana na mambo haya ndani ya familia zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina uhakika kama kwa kweli tukijirudi na sisi ndani ya familia na Taifa kwa ujumla kuanzia katika shule zetu basi nina uhakika mambo mengine tutayapunguza kwa kadri tunavyokwenda na tukipingana na utandawazi ambao kwa kweli nao unatuweka katika hali ngumu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mawili, matatu. Kwanza kabisa naomba kusema wazi kabisa kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina sababu mbili, kwanza madhumuni yaliyoelezwa na Muswada huu yanasema ni kulinda na kuendeleza uanuai wa kujieleza kiutamaduni unaotishiwa kumezw na utamaduni wa nchi zilizoendelea kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Maana yake ni kwamba hata tukizungumza hapa kuhusu kuboresha tamaduni zetu kwa namna zozote zile ikiwa hatuimarishi uchumi basi utamaduni wetu utabakia pale kutishiwa na nchi zenye uwezo mkubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, maana ya pili ni kwamba wakati tunazungumzia kuimarisha utamaduni wetu unaoweza dakika yoyote kutishiwa na nchi yoyote yenye uwezo wa kiuchumi, basi kwanza tuhakikishe tunaweka mikakati yetu vizuri kwa kuanza kuendeleza uboreshaji wa uchumi. Hii ndiyo nguzo yetu kubwa itakayotusaidia mbele ya safari kuona kwamba tunatetea uanuai wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili sasa katika kufanya hivyo ikiwa mkakati wa msingi huo tunauendeleza ni lazima sasa mkakati uende katika utekelezaji wa sisi wote. La kwanza kabisa ushauri wangu ni kwamba Serikali tuna nafasi ya kuelezea haya yote tuliyoyaeleza ya uanuai wetu wa kiutamaduni katika njia ya kijiji, kata na njia ya Kitaifa. Pale haya yatakapokuwa wazi kwa utaratibu wa Serikali, basi tutakuwa na uwezo wa kuyatekeleza kwa usahihi kwa sababu tumeyaweka wazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika ngazi ya kijiji kuna tamaduni ziko pale za kudumu ambazo ndizo tulizozaliwa nazo, ikiwa sisi wenyewe viongozi wanasiwa tutaendelea kuzihimiza na kuziheshimu ngoma zetu na urithi wowote ule wa kiasili na wakiona sisi kama viongozi na wale wataendeleza kuheshimu na kuu-*promote* kwa sababu kutoka ngazi ya juu wanaona tunaendelea kuheshimu.

Mheshimiwa Spika, na la pili sisi wenyewe hata katika Bunge tunaweza tukasema kielelezo cha utamaduni wetu kama Bunge la Tanzania tuwe namna gani na sisi basi tutakuwa tumetoa alama ya kielelezo cha kuheshimu mwelekeo wa utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni suala la Serikali ambayo ndiyo yenye mamlaka wakati wote ikiwa madarakani. Kwanza ni kwamba iendelee basi kuweka mkakati ulio dhahiri wa kuona kwamba kwa kiwango gani wale amba wanaendeleza usanii, muziki na sanaa za aina yoyote hapa nchini wanaendelea kuwekewa Hati Miliki zinazoweza kulinda kazi zao. Ikiwa wao watashughulika *single handly* wao wenyewe bila kuwa na mkono wa Serikali uliowazi kuwasaidia, vielelezo hivi vyta utamaduni wetu havitakuwa na nguvu. Kwa hivyo, nashauri Serikali kuitia Wizara yetu walete mkakati amba kwa uwazi kabissa utahakikisha kulinda na kuweka udhibiti wa Hati Maliki za vijana wote amba wanafanya shughuli hizi za usanii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ukisoma lile Azimio wanasema kuna *cultural industries* ambazo zitasaidia, kwa hili wakati tunazungumza kuendeleza uanuai wa utamaduni wetu ni lazima basi tutafute namna gani *tuta-promote* kwa kuendelea kuzalisha tamaduni zilizokuwepo na kuziboresha kama *social industries* zitakazokuwa

*progressive*, halafu pili kwa sababu hizo ni *products* ni kwa kiwango gani sisi tulio viongozi tunawatafutia hawa soko la kuweza ku-*market* hizo *products* ambazo zinatokana na *social industries* zinazoendelea kujihusisha katika juhudini za kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu *social industry* ambayo ni *time consuming* kwa hivi nao wako katika kazi au tuko katika kazi ionekane ni kazi ambayo ina mapato. Kwa hiyo, ni lazima zitafutiwe soko ambapo ye yote atakayekuwa anajihuhsisha na shughuli yoyote ya kiutamaduni asionekane kwamba yuko katika wakati wa kupoteza muda. Iwe ni kazi ambayo ni dhahiri kabisa inayoonekana na yenyewe inalipa kama tunavyoji-*engage* katika *social* au *economic activities* zingine.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mchango wangu na mimi ningependa Serikali ushauri huu ninaouweka mbele yao waone namna ya kuweza kuufanya kazi. Asante sana. (*Makofî*)

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, na mimi ningependa kutoa shukrani za dhati kwa nafasi hii nzuri ya kuweza kuchangia azimio hili. Lakini awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunirudisha Bungeni kwa mara ya pili, nasema Mungu atukuzwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikishukuru chama changu cha CCM kwa kupitia UWT Mkoa wa Morogoro kwa kuweza kunichagua kwa kura nydingi na kuweza kuingia Bungeni ili niwawakilishe. Napenda ni wahakikishie kwamba hakika sitawaangusha, tufanyekazi uchaguzi umeisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi pia ningependa niungane na wenzangu kuunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia kwa mia kwa sababu lina faida kubwa katika Taifa letu. Hatujungi tu kwa sababu ya kufuata mkumbo eti kwa sababu sisi ndiyo tumbeki Mataifa mawili tu Tanzania na Rwanda, hapana faida iliyo katika Azimio hili ni kubwa. Kiuchumi tunaweza kupata mikopo, ajira, uongozi na sisi tukasikika na tukalinda tamaduni zetu, kwa hiyo hakika faida ni kubwa na hivyo ningeomba Bunge Tukufu liweze kuridhia Azimio hili kwa maana lina faida kwa Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba pia niweze kutoa ushauri katika mambo machache ambayo wengine wameyagusa lakini siyo vile nilivyoguswa mimi. Wamesema lakini mimi sikuona kama nimeridhika labda nikisema na mimi pia iwe imetia mkazo katika hayo mambo ili kila mtu achukue kwamba Azimio lililo mbele yetu lina faida. (*Makofî*)

Kwanza kabisa ningesema kwa habari ya umuhimu wa wasanii wetu. Usanini siyo burudani tu kama wengine walivyosema, usanii ni utajiri ndiyo ulioweza kuwatoa wakina Michael Jackson, akina James Bond mpaka sasa tunaangalia sinema zao, nyimbo mbalimbali za Elvis Presley mpaka sasa hivi bado tunazisikia, kwa kweli ni wengi ambao sanaa imewatoa na sisi tukisisitiza na kuwatia moyo vijana wetu na kujaribu kusaidia kulinda haki zao katika usanii huu hakika kabisa na wao wataweza kuwa na nafasi nzuri ya kuinua kipato chao kwa kazi zao wanazozifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba pia niweze kuchangia kwenye yale mavazi ya watoto wa kike wanenguaji katika sanaa. Wengine wamesema lakini mimi inaniumiza zaidi kama mzazi ninapoona kwamba vijana wa kiume wamevalishwa vizuri lakini wale vijana wa kike wanavalishwa nguo za nusu uchi halafu tena wanenengue, fikiria hapo inakuwaje. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kama hakika tukiweza kuwasaidia kwanza kwa kuwaelimisha, kuwashauri, wao ni vijana wanaenda na mkumbo tukiwasaidia hakika wataweza. Nilikuwa naangalia *TOT* kikundi kile cha ndugu yetu Mheshimiwa Kepteni Mstaafu John Komba, nilikuwa naona wanavaa nguo nzuri au wale wanaocheza taarabu wanavaa nguo nzuri hata kama kuna mnenguo kidogo lakini unaona una heshima fulani, unaridhika. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kama tutawasaidia vijana wetu watakuwa wanaburudisha siyo tu vijana hata sisi watu wazima tutafungua *TV* kuwaangalia, lakini mara nyingi unazima au unasema zima, zima, zima ukiona kuna mavazi ya kutisha.

Mheshimiwa Spika, lingine pia la muhimu nilikuwa naona katika hilo hilo vazi la Taifa. Nilikuwa naangalia katika sisi tulio watu wazima tunakumbuka siku za Uhuru Baba wa Taifa alikuwa amevaa nguo fulani kama ya Ghana. Ni kitenge kizuri lakini unavaa kama lubega hivi, ilikuwa inaonekana kama ni vazi letu la Taifa. Wanawake nao walikuwa wanavaa vitenge fulani vyenye mkato kwenye maungio ya kiuno halafu baadae unashusha sehemu mbili za urembo fulani zikafunika makalio kukawa na heshima nzuri tu ile sketi yake ikawa nzuri na blauzi ikafunika kabisa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naona ilikuwa inavutia, sasa sijui waliotupiku ni Waghana, sasa mimi naona hilo vazi linavaliwa na Waghana lakini naona sisi tangu miaka ile ya 1960 hili vazi tulikuwa tunalivaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa kweli kuwa na *identity* ya mavazi katika Taifa. Tunapokwenda Uganda ukiona walivyovaa, ukiona Wahindi wanavyovaa, Waghana au Wanageria inajulikana hawa wanatoka mahali fulani. Lakini Watanzania tumejaribu kanga haiji, nini, hebu tujaribu kabisa wabunifu wengi wapo wanaoweza kubuni vazi zuri la mwanamke wa Kitanzania na sisi tukatambulika kama tuna vazi letu zuri. Naona yule Mheshimiwa wa *Peacock Hotel* anajitahidi, huwa anavalisha wale wafanyakazi wake mavazi ya Kitanzania, vitenge, wanapiga magoti kienyeji na nini, ukiingia unasikia angalau hapa kuna mahali penye Utanzania Tanzania kidogo na panafurahisha kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo nilikuwa naona hapa niungane na wenzangu waliochangia kuhusu vazi la Taifa, tulichukulie kwa umuhimu kwa sababu mara nyingi tumesema lakini matendo yanakuwa ni machache. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, kwa sababu mimi pia ni mmojawapo tuliochambua hilo Azimio nitoe pongezi kwa Wizara hiyo kwa kuleta Azimio hili kwa wakati muafaka na vile vile

nikizingatia pia kulikuwa na msemaji mmoja alisema tungependa utangazaji wa makabila. Nilikuwa nafikiria kama alivyosema Waziri wakati anatoa hoja hii alisema kwamba kama kweli jamani kila mtu atasema mimi niweke kabilia yangu, nifungue redio kwa kabilia yangu, niseme kipindi fulani kwa kabilia yangu, sasa tutakuwa tunarudisha yale yale mambo ya ukabila ambayo tumeshayapita hapo nyuma.

Kwa hiyo, nilikuwa naona ni vizuri tu tuendelee na Kiswahili chetu mbona kizuri tu na wengi wameingia kwenye Kiswahili na ndio tunatambulika hivyo kwamba sisi tuna lugha yetu nzuri ya Kiswahili ambayo inatuunganisha haileti ubaguzi, haifanyi hili ni kabilia dogo na hili ni kabilia kubwa lakini wote tunajiona kama tuko sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya machache nasema ahsante kwa kunipa nafasi Mungu awabariki. (*Makofi*)

**MHE. DKT. KWEBE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza nami vile vile napenda kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa safari ndefu ya mchakato wa uchaguzi ambayo kwa busara na hekima Wanaserengeti walinchagua kuwa Mbunge wao, nawashukuru sana. Lakini pia kwa heshima kubwa hiyo walichagua Chama cha Mapinduzi ambayo ni utamaduni wa Wilaya ya Serengeti hawajawahi kwenda pembedi bali kuendelea kuchagua Chama Tawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya kuchangia hoja naomba nirejee sehemu ambayo imechukua maudhui ya Azimio hili ambayo ni; “Kamati ilibaini kuwa kila jamii kujieleza kiutamaduni kupitia ubunifu, watu au makundi ya watu kwa njia mbalimbali kama vile hadithi, sauti, muziki, picha, michoro, filamu, sanamu, kusuka, kudarizi, ngoma, maigizo na vitabu. Njia hizi za kuijendezea huzaa bidhaa na huduma mbalimbali za kiutamaduni ambazo ni za kipekee na utambulisho kwa jamii husika.” Mwisho wa kunukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia maudhui haya nitajikita katika maeneo hayo nikianza na usemi wa Marehemu Baba wa Taifa ambao alituasa kwamba anayekosa utamaduni ni sawa na mkosa kwao. Tukijaribu kuangalia hali halisi ya utalii katika nchi yetu hatujatumia fursa nzuri ambayo ipo. Wenzetu wengi wanaokuja kufanya utalii Tanzania wanaishia katika mbuga za wanyama, lakini maeneo ya msingi ambayo wangeweza kupata picha ya utamaduni wa nchi yetu tumeacha sehemu ya *cultural tourism*. Sehemu hii ya utalii wa kiasili ni pamoja na kusomwa na wao kuiga haya ya kwetu kwa sababu kuna siku moja watu mbalimbali kutoka Bara la Afrika tulikuwa Ujeruman kanisani pale na kulikuwa na kipindi kwamba kila mmoja wetu basi waimbe nyimbo kutoka Taifa lao. Kuna ndugu wengine ambao walikaa Afrika ya Kusini, mama yule wa Kijeruman aliapanda midadi akaanza kukimbia kanisani kwa sababu ya *melody* nzuri za muziki ambayo tunayo katika Afrika. Kwa hiyo, unaona kwamba wenzetu wanatamani haya ya kwetu, lakini cha kushangaza basi na sisi tumbaki kudakia kuiga yale ya ng’ambo ya kibeberu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba suala la *cultural tourism* lisitisizwe kwa sababu linasaidia kuendelezwa utamaduni wetu. Ushahidi kwamba katika mkutano mkubwa wa wadau mbalimbali uliofanyika Arusha wa Sullivan wote tunakumbuka kikundi kimojawapo cha utamaduni kutoka Wilaya ya Serengeti walipata fursa ya kushiriki na walikaa *front bench* kwa jinsi ambavyo walikwenda wakajiandaa vizuri katika ushindani wa kitamaduni. Kikundi kile cha ngoma tunakiita maarufu kule nyumbani Mityambwe ni kikundi cha aina yake lakini wanaendelezwa vipi hawa? Kama wameweza kuingia katika sura ya dunia kupitia mkutano mkubwa kama ule wa Sullivan ni fursa kama hizo ambazo zinabidi kuendeleza wasanii wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukijaribu kuangalia kwamba utamaduni unaishia vipi mtoto anavyofundishwa kile kinachoingia kinakaa katika akili yake kinajengeka vizuri. Hatuoni utamaduni katika shule za msingi, shule za sekondari na maeneo mengine ambayo ni fursa tuliyonayo ya kuweza kujenga na kuendeleza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, sisi tukiwa wadogo nakumbuka siku zile shule za msingi kulikuwa na vikundi mbalimbali nya ngoma, tamaduni mnashindana zawadi zinatolewa, lakini haikuwa suala la mchezo kushindana tu ile ni njia mojawapo ya kuendeleza utamaduni kile ambacho tunacho kielelezo cha Utaifa wetu. Kwa hiyo, naomba suala hilo la michezo kiutamaduni katika shule za msingi na maeneo mbalimbali lihimizwe na liimarishwe.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia Maafisa Utamaduni wetu katika Halmashauri zetu wamekata tamaa. Wamekata tamaa kivipi? Pale ambapo kunakuwa na fursa ya msafara wa kiongozi fulani basi pale ndio vinatafutwa vikundi nya ngoma, Afisa Utamaduni kutokana na fedha kidogo imepatikana kwa kuchanga ndio anaambiwa bwana katafute vikundi viwili, vitatu hivi waje hapa kwa ajili ya ugeni wa Kitaifa au ugeni fulani, ama wakati wa Kampeni au wakati wa Mbio za Mwenge ndipo pale tunawakumbuka Maafisa Utamaduni. Hawa ni sawa na askari, unampeleka vitani ambaye hana silaha. Wawezeshwe ili kusudi waache kukaa ofisini na waache kutegemea hizi fursa za sikuu za Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kutangaza utalii naomba lijumuise maeneo yote yale ya msingi ambayo nimeyatamka ikiwemo suala la *cultural tourism*. Suala hili ukijaribu kuangalia jinsi utalii wa nchi yetu unavyotangazwa ni ile kualika kuja kuangalia mbuga za wanyama suala ambalo linaturudisha nyuma, tutumie fursa ambazo zipo. Lakini suala la utandawazi naomba kutofautiana kidogo na wasemaji wengi ambao wamelizungumza, hili linasaidia kudhalilisha utamaduni wetu tulionao. Hii ndugu zangu ni fursa ya kupitia utandawazi huo huo na sisi tujijenge kutumia utandawazi kwa sababu ndio mojawapo ambayo ipo ya kileo ili kusudi na sisi utamaduni wetu upitie katika mtandao huo huo na hili litatusaidia kujijenga na kujimarisha katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi. Unajua wakati mwengine unafika mahali huwezi ukaelewa, unaweza ukakutana, samahani kwa kutumia mfano huu anaweza akawa ni dada ameshona nguo ukipita upande wa kulia utaona hiyo nguo ni ndefu kweli

kweli mpaka inagusa ardhi, lakini ukipita upande wa kushoto unashangaa kuna utupu, hivi ile nguo ni fupi au ni ndefu? Suala hili la mavazi ni suala la heshima ya hali ya juu. Siku moja tulikuwa katika *shopping mall* ama *shoprite* kule Durban, nilishangaa nilikuwa nimevaa shati ya batiki kumbe kuna Mhindi mmoja mfanyabiashara anazunguka dunia nzima nikashangaa ananijia nikadhani huyu anataka kufanya biashara na mimi nikanunue bidhaa kwenye duka lake, lakini akasema bwana hiyo shati mimi hata kabla sijaongea na wewe nina hakika *you must be coming from Tanzania*. Kwa sababu ya uzoefu wake na aliipenda ile shati akataka hata kuinunua. Sasa nikamwambia ndugu yangu ukinunua hii shati mimi nitavaa nini? Akasema tutabdalishana mimi nitakupatia shati nyingine nzuri, nikamwambia hapana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni kuonyesha kwamba mavazi ni suala ambalo linatupa heshima, linatujengea heshima lakini Watanzania wa leo walio wengi hawafahamu vazi lipi la Kitaifa. Mimi naishauri Wizara ijaribu kuangalia hili kwa makini kabisa. Suala la mavazi, vazi la Kitaifa lijulikane ili kusudi hata ukienda sehemu yoyote wanajua huyu ni Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo nilikuwa nayo naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu. Pia napenda nikupongeze ukiwa mwanamke wa kwanza katika Tanzania kuchaguliwa kuwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mada nzima ya Azimio hili ambalo linachangiwa ningependa tu kuishauri Serikali iweze kurejesha sherehe zote za Serikali na vikundi mbalimbali vya asili ili viweze kupata nguvu na kuweza kufadhiliwa na kushindanishwa na kupata zawadi mbalimbali ikiwemo pia na michezo shulenii ili kuepuka zoezi zima la watoto kujihusisha na vitendo vya uovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza Wizara nzima, Waziri pamoja na Wanakamati wenzangu ambao tulishiriki kwa Azimio zima kuweza kujadili mpaka azimio hili kuweza kuingizwa katika Bunge. Naomba turidhie ili tuweze kudumisha utamaduni wetu, mila zetu ila tu ningeomba Serikali iweze kuunda sheria kali zichukuliwe pale ambapo utamaduni ambao unaweza kuingia katika nchi yetu au kuigwa ambao utamomonyoa tena maadili yetu ambayo tunataka kuyarudisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, asante sana pamoja na waliotangulia kuchangia azimio hili au hoja iliyoko mezani.

Kwanza napenda nichukue nafasi hii kuchangia mada moja ambayo inahu fasihi ya Kiswahili katika kuendeleza utamaduni wa asili wa Mtanzania. Nafahamu kabisa kwamba waandishi wa vitabu hasa wa fasihi, riwaya, tamthilia na ushairi umetoa

mchango mkubwa sana kuendeleza utamaduni wa Mtanzania kwa sababu wenyewe wamejikita katika vipindi mbalimbali vya kihistoria tangu enzi za ukoloni, enzi za Uhuru mpaka sasa hivi. Lakini tatizo kubwa tunalolipata ni moja kwamba vijana wetu au sisi watu wazima usomaji wa vitabu umekuwa ni tatizo kubwa sana na hivyo inakuwa ni kazi ngumu kuuelewa utamaduni wetu. Lakini naamini kabisa kwamba tukiwa na mikakati maalum kuendeleza utamaduni huu katika Mfuko ule wa Utamaduni au Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo tuwe na Kitengo cha tafsiri ambacho kitawezeka kutafsiri lugha mbalimbali za makabila, nyimbo mbalimbali katika lugha ya Kiswahili hii itasaidia zaidi kuimarisha utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na yote hayo kuna kitu ambacho tunapozingatia utamaduni lazima tukiweke mbele kwamba athari za utandawazi zimechangia sana kuua utamaduni wa Mtanzania, lakini lazima tukubaliane nacho na vile vile utamaduni wetu wa asili, kuna ule utamaduni ambao umeshapitwa na wakati na utamaduni mwingine haujapitwa na wakati. Kwa mfano, katika jimbo langu ninalotoka kuna majigambo yanatokana na kipindi cha tohara.

Sasa wanaharakati nikisema jambo hili kwamba kuna suala la kukeketa, wale wasichana wanapokeketwa wanajigamba na wanatamba wanaona ni vizuri zaidi na watu wanafurahi. Lakini wanaharakati wasije wakaninukuu vibaya lakini naamini kabisa kwamba kuna tamaduni ambazo kwa kweli zimeshapitwa na wakati, inabidi tuziangalie kwa makini sana na kuna tamaduni ambazo inabidi tuziendeleze, hii itatusaidia zaidi katika kufanikisha mambo ambayo tunayarithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa tutaweza kufanikisha haya, lazima mambo mengi ambayo yamehifadhiwa katika lugha zetu za asili tutayaweka katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo kuna suala la lugha ya kufundishia shulenii, hili ni tatizo kubwa sana kwa utamaduni wetu wa asili. Tunapoongelea utamaduni tuamini kabisa kwamba kuna mila, desturi, uchumi hata na siasa iko ndani ya utamaduni. Sasa tukiendelea kufundishia lugha zile za kigeni bado hapo tutakuwa tunatkuza utamaduni wa kigeni. Hilo ni tatizo ambalo kwa kweli inabidi tuangalie lugha gani tuitumie katika kufundishia, maana lugha ndio utambulisho wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi sana tunaweka katika Kiingereza na mambo mengi sana tunaweka Kiswahili lakini sasa tuangalie je, ili tuutetee utamaduni wetu wa Mtanzania ni lugha ipi tuitumie katika kufundishia shulenii. Jambo hili litatusaidia zaidi na naamini kabisa kwamba tukifanya hivyo tukaweka *system* nzuri kwamba kujifunza lugha ni kuzuri lakini elimu ya Tanzania tuitoleee lugha ipi? Lugha ya Kiswahili kutoka darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu au ni lugha ya Kiingereza kutoka darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu? Hiyo nafikiri itaweza kutusaidia. Tufikiri zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile naamini kabisa kwamba wale waandishi wa vitabu ambao wameandika vitabu vyao katika lugha ya Kiswahili ili tuweze kuwaendeleza na kuwasaidia tuangalie namna ya kuvitafsiri vile vitabu katika lugha zingine za Kiingereza. Watalii wengi wanapokuja au wageni wengi wanapokuja wanashindwa kujifunza utamaduni wetu hususan wanapoomba vitabu vilivyoandikwa katika Tanzania hii

wakiomba kwamba riwaya fulani kwa mfano kuna riwaya moja inaitwa Kuli. Siku moja nilikwenda kule Ujerumani nikakuta wanaitafuta sana imetafsiriwa kwa Kijerumani. Lakini ukikuta kwa Kiswahili au imetafsiriwa kwa Kiingereza inakuwa ni tatizo. Sasa tuangalie Mfuko wa Utamaduni kama unaweza kusaidia kuendeleza baadhi ya waandishi ambao wameandika vitabu vyao kwa lugha ya Kiswahili ili viweze kutafsiriwa kwa lugha zingine tutaweza kukuza kipato chao.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine waliotangulia kuchangia kuhusu vazi la Taifa. Kuna matatizo makubwa sana, hatuna utambulisho wowote ule kwamba tunavaa nguo ya aina ipi?

Mheshimiwa Spika, kuna nguo nyingi, wengine wanavaa nguo lakini hiyo inaingiliwa na utamaduni ambao ni wa kigeni, hatuwezi kubishana nao kwa sababu wanasema kwamba hayo mambo yanakuja na wakati yanaondoka. Hata vile vile tunavyoangalia hata nywele tulizonazo tuone hizo nywele kama ni za asili au zinatokana na nini, mambo kama hayo yote ni ya kujiuliza maana naamini kabisa kwamba tukisema tunaridhia tu utamaduni wa asili bado kutakuwa na tatizo kubwa sana katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba tuchukulie changamoto utandawazi katika utamaduni wetu hatuwezi kuuepuka hilo ni jambo ambalo kwa kweli kuliepuka ni kazi ngumu sana. Lakini nasisitiza kwamba kuna nafasi kubwa sana ya fasihi ya Kiswahili katika kuendeleza utamaduni wetu wa asili. Tuangalie namna ya kuwasaidia wale waandishi wanaoandika vitabu vyta riwaya, mashairi na tamthilia ili waweze kujikwamua kupitia fani yao ya fasihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asante sana na naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii ambayo sikuitegemea kama nitaipata. (*Makofi*)

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniingiza ndani ya Bunge hili na vile vile nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea basi nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa jimbo langu la Manyovu kwa kunipa kura nyingi na nawaahidi kwamba tutashirikiana nao, sitawaangusha, tutajadili matatizo na neema zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili naomba nichukue nafasi hii kushukuru Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuleta Azimio hili ambalo hakika lina manufaa mengi na mengi yameelezwa na pili nishukuru Wabunge wenzangu kwa kuyaeleza na kuyaainisha kwa kila mtu alivyoweza na mimi kabla ya kuchangia naomba niahidi kwamba nauunga mkono Azimio hili lipite kwa asilimia zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu uko ndani ya Tanzania yetu sio namna ya tunavyoridhia huu Mkataba na nchi nyingine. Ndani yetu ile *capacity* ya kuhakikisha kwamba utamaduni wetu tumeulinda kabla ya wale hawajatulindia mkataba wetu, hapo ndipo ninapopata matatizo.

Wizara yetu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inabidi kwa kweli ijidhatiti na ili kama wenzangu walivyosema hata ukiangalia Ofisi za Utamaduni za Wilayani au za Kata kwa kweli zimekufa. Kwa hiyo, tungeomba Waziri anapoeleza anataka kulinda utamaduni na yeye awe na utamaduni wa kulinda ofizi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile wasanii, ukienda katika ngazi za vijiji wasanii wametuimbia mambo mengi sana. Wakati wa kampeni au wakati wa sherehe au wakati wa sheria za Uhuru au sherehe mbalimbali viongozi wetu wanapokuja. Lakini ule ujira tunaowalipa mfano mimi kwenye Jimbo langu kuna vikundi vilikuwa vinaniimbia au vinahamasisha watu kuchagua, ukishawalipa laki moja wanapogawana wako labda 15, unakuta wamepata shilingi 6,000/= kila mmoja, inakuwa ni kitu hakiwatoshi kabisa na muda wanaotumia kujifunza zile nyimbo mpaka waweze kujua ni muda mwingi sana. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kutumia *fund* hii kama tutaweza kuwa na fedha basi hizi fedha ziweze kuteremka kwa vijana wetu, wazee wetu na bibi zetu wanaoimba ndani ya vijiji vyetu ili na wao waweze kufaidi. (*Makofi*)

Vilevile kuna kutowatambua, kuna watu wanaimba ngonjera huko vijijini, wanaimba vizuri kabisa lakini ofisi yetu na chini ya Wizara yetu nafikiri iongeze nguvu kwenye maeneo yale. Lakini la pili ndani ya Wizara yetu hatusikii tamko linaloongelea mavazi. Hapa sasa hivi tunapiga kelele kama vile tunauambia Mkataba wa huu wa UNESCO lakini Wizara inasemaje juu ya mavazi ambayo yamo humu humu kabla ya huu mkataba hatujauridhia lakini sisi wenyeve tuna matamko yapi? Ni vizuri nayo tuanze kuwa wakali kwa kile ambacho tunaamini kwamba ni kizuri kinafaa kwa vizazi vyetu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ukiuangalia umeweza kulinda na kukuza lakini hauelezi kukomesha zile tamaduni mbovu. Ndugu yangu Nyangwine pale Musoma wana utamaduni wa kupiga mke mpaka umpige ndiyo ufurahi. Sasa sijui na ule inabidi tuulinde na tukuze, sasa nafikiri kwamba huenda huu Mkataba kuna vitu vingine vinahitaji kuchambuliwa. Tunakuza upi, tunaacha upi? Sasa ndani ya Mkataba huu haikueleza itakavyokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mengi yameshaongelewa na wenzangu na mimi sitaki kutumia nafasi hii kueleza mengi, leo Mwenyezi Mungu amenipa nafasi ya kuongea katika Bunge lako Tukufu wananchi wangu wategemee nitaanza kuongea, nimetumia muda mwingi kujifunza na sasa nimeanza kuelewa taratibu za Bunge letu, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inapendeza sana katika Azimio hili walioomba kuchangia walikuwa 19 kwa sababu wengine walikuwa wanajifunza wamenisaidia, wamebaki kama Wabunge sita tu. Sasa kwa sababu tunaahirisha kikao saa mbili kasoro robo napenda kwa hatua hii nimwite Waziri aweze kutoa ufanuzi au kujibu hoja zenu. Mheshimiwa Waziri karibu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutambua waliochangia kwani jumla ya wachangiaji ni 27, waliochangia kwa mdomo ni 14 na waliochangia kwa maandishi ni 13. Nianze kwa kumshukuru Msemaji wa Kamati Mheshimiwa Agnes Hokororo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Kepteni John Komba, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatale, Mheshimiwa Kebwe Kebwe, Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine na Mheshimiwa Albert Obama. (*Makofî*)

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Suleiman Saidi, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Khamis Seif, Mheshimiwa Khatib Kai, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Haji, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamsi, Mheshimiwa Zarina Madabida na Mheshimiwa Lucy Owenya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutambua wachangiaji hao, naomba nianze kupitia baadhi ya hoja. Kwanza ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii tunakubaliana nao na tutaufanya kazi na hasa katika kujenga mazingira mazuri ya kutekeleza kivitendo Azimio hili. Aidha, Serikali itajitahidi kuongeza nguvu za utendaji ikiwemo fedha za Mfuko wa Utamaduni Tanzania, kwa sasa Serikali inalipa mishahara ya watumishi wa utamaduni na imeongeza ruzuku kwa asasi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alitaka kujua kama Serikali imejiandaa kikamilifu, nataka nimhakikishie kwamba Serikali imejiandaa kikamilifu katika utekelezaji wa Mkataba huu kwa maana ya ndani ya nchi yetu. Lakini vilevile nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbilinyi anasema Hati Miliki na Hati Shiriki hazijawa na tija za kutosha kwa wahusika kwa maana ya wasanii wetu.

La kwanza nikubaliane nae kwamba ni kweli tija ya kutosha bado haijapatikana lakini tunaweka juhudhi za pekee kuhakikisha kwamba tija hiyo inaonekana mapema inavyowezekana. Lakini nimhakikishie kwamba kufikiwa au kusainiwa kwa mikataba ile hakukutokana na shinikizo la nje, mikataba yote ya Kimataifa ambayo Serikali yetu inaingia hakukutokana na shinikizo la nje.

Mheshimiwa Spika, mikataba yote ya Kimataifa ambayo Serikali yetu inaingia, inaingia kwa hiyari, hakuna Mkataba ambao Serikali inaingia kwa shinikizo na wala hakuna Mkataba ambao Bunge linaridhia kwa shinikizo la nchi yoyote. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba Uhuru wa nchi yetu na Mamlaka ya Bunge letu havijawahi kupuuzwa hata mara moja kuhusu mtu alazimishe tutekeleze anayoyataka yeye. (*Makofî*)

Lakini umuhimu wa sanaa kuchangia katika ajira tunauelewa na tunaufanyia kazi, lakini vilevile umuhimu wa kukuza utamaduni wetu nje ya nchi yetu ni wazo muhimu sana na lenyewe litafanyiwa kazi. Naomba niwashukuru waliongelea umuhimu wa vyombo vyetu vya habari katika kukuza tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyetu vimesikia na sisi tunatoa wito vyombo vyetu vishiriki katika kuona kwamba utamaduni wetu unaendelea kuhifadhiwa kwa sababu Taifa lisilokuwa na utamaduni ni Taifa mfu na vyombo vyetu sidhani kama vitanufaika kuishi katika Taifa mfu. Waliongelea kulinda, kuhifadhi na kuheshimu tamaduni zetu hii ni changamoto kubwa kwa kila Mtanzania, Serikali kwa upande wake itatimiza wajibu wake lakini kila Mtanzania ni muhimu naye aone namna ya kushiriki katika kulinda utamaduni huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mavazi tunayoyatumia katika nchi yetu, la kwanza kuhusu mavazi yenye heshima na yanayoakisi utamaduni wetu wa Kitanzania na niwapongeze sana na kuwashukuru ambaao wamesema malezi haya namna ya kuvala yanaanza katika ngazi ya familia, tuwaombe wazazi wa Kitanzania, Watanzania wote watu wazima wenye familia washiriki katika changamoto hii kubwa kwa Taifa letu. Tunalo tatizo kubwa sana la aina ya mavazi, mnaona vijana wanatembea kama ambavyo mmesema wenye na nguo ambazo hazifichi staha ya binadamu. Mtu anakwenda kushona suruali anaulizwa unavaa namba ngapi, unavaa namba 30 lakini anamwomba fundi aweke namba 40 ili tu iwe inateremka sasa huu ni utamaduni ambaao lazima upigwe vita na watu wajue jambo hili si jema.

Sasa mtu akivaa vile halafu akipita unamwambia mambo yako bomba, umependeza, utamaduni huo wa hovyo unaendelea kukua. Kwa hiyo, tukishirikiana wote ni wazi kwamba utamaduni huu utafika mahali watu wataona hauwezi kwenda. Lakini kupitia kwenu niviombe vyombo vyote vya habari, hasa vya televisheni vione aina ya matangazo vinavyotoa na venyewe vishiriki katika kukuza utamaduni wetu na mavazi yenye staha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa wale waliochangia umuhimu wa kutunza wachongaji wetu, watu wenye vipaji mbalimbali vya kutengeneza vitu ambavyo vinaakisi utamaduni wetu. Nataka nikubaliane nao kama ni changamoto ya Serikali, Serikali za Mitaa viongozi na wananchi wote tushirikiane katika kufanya jambo hili. Serikali kwa upande wake itatimiza wajibu wake ipasavyo. Kuhusu watunzi wa riwaya, mashairi, tenzi, ngonjera, kuwa na hati miliki iko katika Sheria kwa sasa hivi kitu kilichopo ni utekelezaji wa hiyo Sheria kufahamika zaidi. Huu ni wajibu wa Serikali tutaendelea kuufanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu aina ya vitu vyetu kutumika nje bila kutambua kwamba vimetoka katika nchi yetu hii ni moja ya maeneo ambayo yameshajihisha kuukubali Mkataba huu na kuusaini, itatusaidia siku tunazokwenda mbele. Kuhusu Vazi la Taifa, mchakato wa kulisipata Vazi la Taifa unaendelea mapema mwaka huu nilitoa maelekezo kwa Idara ya Utamaduni kwamba mchakato huu ndani ya Wizara uwe umekamilika ifikapo mwezi Juni mwaka huu, baada ya kukamilika kwenye Wizara tutawapeni taarifa za hatua zinazoendelea. Nina hakika Idara ya Utamaduni itatekeleza

maelekezo yangu kama nilivyoagiza. Kwa hiyo, jambo hili halijapuuzwa hata kidogo limepewa uzito hata unaostahili na kwa kweli nataka sasa tulimalize.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa kutengeneza mazingira ya kutoruhusu utamaduni wetu ugandamizwe, nadhani hili ndiyo msingi wenyewe wa Azimio hilo, kwamba kama nilivyosema asubuhi kwamba hatuzuii utamaduni mwingine kufika, lakini usiumize na kuuvuruga utamaduni wetu, utamaduni wetu mara zote uwe juu ya tamaduni zinginezo. Kwa hiyo, jambo hili ni la msingi tutaendelea kulisimamia. (*Makofi*)

Kuhusu umuhimu wa vyombo vya habari na sherehe za Taifa kushiriki katika kukuza utamaduni kama nilivyosema awali ni jambo la msingi tunakubaliana nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Lugola ya kufufua tamaduni zilizokufa nitoe wito kwa jamii zinazohusika kulifanya kazi jambo hili kwa sababu tamaduni ziko katika ngazi mbalimbali kutoka ngazi za mitaa, kata na tarafa. Kwa hiyo, jamii zinazohusika zione umuhimu wa kufufua tamaduni hizo. Lakini pia umuhimu wa kuwa na mikakati maalum ya kuchangia vikundi vya utamaduni ili viweze kukua. Sisi kama Serikali tutafanya nitoe wito kwa taasisi na asasi mbalimbali pia kufanya hivyo lakini pia Halmashauri za Wilaya zitenge fedha kwa ajili ya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo mbalimbali ya jadi kama mchezo wa ng'ombe unaopatikana Pemba naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Waziri wa Michezo na Utamaduni kule Zanzibar wanafahamiana kwa karibu sana na Mheshimiwa Mnyaa kwa hiyo, niseme mimi na ye ye tutashirikiana pamoa tuone tunafika wapi na wazo hili. Lakini pia niwahakikishieni kwamba hoja ya Mfuko huu kujali pande zote za Muungano ni hoja ya msingi wala haihitaji maelezo makubwa sana, ni hoja ambayo iko wazi. Ni lazima tutafanya hivyo na umuhimu wa maonesho yetu ya tamaduni kufanyike nje nimekwisha kuelezea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuenzi wasanii wetu amba wanafanya mambo mazuri au wanatuwakilisha vizuri katika Jumuiya ya Kimataifa ni hoja ya msingi inawezekana ikawa na ulegevu wa hapa na pale, naomba nichukue nafasi hii kuwashakikishieni Wabunge kwa nafasi ya pekee katika kutekeleza Mkataba huu lakini vilevile kutambua tunawajibu wa kukuza utamaduni wetu. Hili nalo tutalipa kipaumbele cha namna ya peke yake.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mavazi nimeshaisemea. Lakini hoja ya viongozi kuongoza kwa mfano katika kulifikia jambo hili ni hoja ya msingi, naomba tulizingatie wote lakini pia umuhimu wa kukuza soko kwa ajili ya wasanii wetu amba wanakuza utamaduni katika jamii ni jambo la msingi, sisi kama Serikali tunalichukua na wadau tunaomba walichukue. Umuhimu wa sanaa kama chanzo cha maisha bora kwa Watanzania wote nalo ni jambo la msingi kabisa ambalo ni muhimu wote tukalifanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge wengine wameongelea suala la *cultural tourism* (Utalii wa Kiutamaduni) ni jambo la msingi katika kutekeleza mkataba huu lakini pia katika kukuza utamaduni wenyewe. Ni jambo ambalo tutalipa kipaumbele, tutaomba na wadau wengine katika maeneo mbalimbali watoe kipaumbele kwa jambo hili. (*Makofi*)

Hoja ya Maafisa Utamaduni kutokuwa na nguvu ya kutosha kutekeleza majukumu yao jambo hili ni la kweli tunalifanya kazi, tunalifanya marekebisho muda si mrefu. Umuhimu wa kujitambulisha na mavazi yetu nalo ni jambo la msingi sana. Kama ambavyo Mheshimiwa Kebwe alisema kwamba walimtambua kwa sababu ya vazi lake na ni vizuri tukitengeneza mazingira ya mavazi ambayo watu wakikuona wanasema huyu ni Mtanzania. Vazi la heshima ambalo linamtambulisha mtu na utu na haki za binadamu ambazo zinajali kuangalia maslahi ya wengine pia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya umuhimu wa kuwa na mashindano ya utamaduni na kutoa zawadi na yenyewe ni hoja ya msingi sana. Nitoe pongezi za pekee kwa taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikisimamia mashindano mbalimbali ya kiutamaduni lakini niziombe sasa ziingie pia kwenye utamaduni wa jadi badala ya kujikita tu kwenye tamaduni zingine ili mashindano hayo na zawadi yaweze kuhamasisha kukua kwa utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuwa na kitengo cha tafsiri ya lugha za asili nayo ni hoja muhimu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekuwa kikifanya jambo hili kama ambavyo nimesema asubuhi. Tunachotaka sasa ni kuongeza uwezo lakini pia asasi zingine zijishirikishe katika jambo hili. Lugha zetu lazima zitunzwe ili ziweze kuwa na kumbukumbu lakini muhimu pia kwa Taifa lijalo. (*Makofi*)

Kuhusu umuhimu wa kutafsiri vitabu vyetu vya kiswahili kwa lugha zingine hoja hii ni ya msingi, tunaomba wale watanzi wenyewe pia waone umuhimu wa jambo hili ili kwamba tabia na makuzi yetu yaweze kufika një kupertia mfumo huu wa hadithi na masimulizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya wasanii kunufaika na kazi zao nimeshaisemea, hoja ya wasanii kutambuliwa ni muhimu lakini pia nisemee kwa kifupi kuhusu tamaduni ambazo Mheshimiwa Albert Obama alilisemea, utamaduni wa watu kupiga wake zao. Katika mambo ambayo nimeyasema moja ya jambo la msingi nimesema tamaduni tunazokusudia kuzitunza na kuzienzi ni zile ambazo hazikiuki haki za binadamu. Tabia za kupiga wake zetu ni tabia zinazokiuka haki za binadamu, kwa hiyo, haziungwi mkono na Mkataba huu na wala haziungwi mkono na Serikali. Kwa kweli wenyewe tabia hizo wajihisi tu ni jambo la aibu kupiga mke wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba niwahikikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zote ambazo wamezitoa zimezingatiwa na hoja zote zitafanyiwa kazi lakini kwa namna ya pekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wamechangia kwa kina katika hoja hii ya leo na kutoa michango ambayo imekuwa na msaada mkubwa kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba tuendelee kuwa na ushirikiano, niwahakikishie Wizara itafanya kazi kwa karibu na nyie na kuzingatia kila ushauri mtakaoutoa ndani na nje ya Bunge mradi uwe na maslahi kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Mkataba wa UNESCO kuhusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai ya Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 (The Convention on Protection and Protection of the Diversity of Cultural Expressions of 2005) liliridhiwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa UNESCO unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005 umepitishwa na Bunge hili. (*Makofi*)

Sasa shughuli tulizokuwa nazo kwenye ratiba ya kazi za leo tumezimaliza. Lakini nina tangazo dogo hapa; Mheshimiwa Jenista Mhagama Katibu wa *caucus* wa Chama cha Mapinduzi anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CCM kwamba baada ya kutoka hapa wakutane kwenye Ukumbi wa Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine napenda kuwashukuru kwa siku ya leo kwa kazi nzuri mliyoifanya na hivyo mkapumzike tukutane kesho asubuhi. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 1.20 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 6 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi*)

